# Nipashe

Jumanne Novemba 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580067

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Adaiwa kufariki dunia baada ya kuvuliwa hirizi na polisi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Assad: Sina kinyongo, nakwenda kufuga kuku

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MKUU WA MAGEREZA AFANYA MABADILIKO**

MKUU wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Phaustine Kasike, amefanya mabadiliko madogo ndani...

**UKURASA WA 4**

**USHAHIDI WA MBOWE KORTINI WAIBUA MAZITO**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amedai mahakamani kwamba...

**ALIYETISHIA BASTOLA AFIKISHWA KORTINI**

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



Distributed by ippmedia

Rais John Magufuli, akimwapisha Charles Kichere kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# JPM ampa maagizo mazito CAG mpya

Amtaka aheshimu mihimili mitatu na kutobishana nayo, amtuma kuisafisha ofisi yake... Endelea ukurasa wa 2


**MICHEZO** YANGA KIMYAKIMYA, ZAHERA SASA ATETEWA UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

## HABARI KITAIFA

# Assad: Sina kinyongo, nakwenda kufuga kuku

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema hana kinyongo na mtu yeyote na sasa anajiandaa kurejea nyumbani kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji wa kuku.

Pia mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu, amesema amesamehe wote waliomkwaza na kuomba asamehewa na kila aliyekwazwa naye, huku akisisitiza hajawahi kumtengenezea mtu jambo la kumuudhi katika maisha yake.

Prof. Assad aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kuulizwa na Nipashe alipohudhuria mkutano wa sita wa Taasisi za Fedha za Kiislamu barani Afrika.

Juzi, Rais John Magufuli alimteua Charles Kichere kuwa CAG, akichukua nafasi ya Prof. Assad ambaye ilielezwa kuwa muda wake wa miaka mitano kuhudumu katika ofisi hiyo nyeti ulikuwa unafika kikomo saa sita usiku wa kuamkia leo.

"Hili suala (swali aliloulizwa kuhusu uteuzi mpya wa CAG) halihusiani na 'summit' (mkutano), ni suala la kibinadamu, nataka kusema, mimi katika mahusiano yote na watu wote, sijawahi kumkosea mtu kwa kudhamiria, sijawahi hata siku moja kumtengenezea mtu kumuudhi," alisema.

Aliongeza kuwa kama kuna watu ilitokea akawaudhi, basi ni kwa sababu ya kusimamia misingi ya kazi.

"Nakumbuka niliwafukuza kazi kama watu wanne kwa sababu kulikuwa na wizi na ushahidi ulikuwapo na mmoja alikuwa ni rafiki yangu kabisa, alikuwa ananisaidia.

"Nilimfukuza kwa sababu kulikuwa na ushahidi wa wizi, watu kama hao wanaweza kunichukia kwa sababu ya kusimamia misingi," alisema Prof. Assad.

Mwanataaluma huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema

INAENDELEA UK 8



Mtuhumiwa Shabani Hamisi (wa pili kulia), akiteremka kwenye gari, huku akiwa chini ya ulinzi wa askari kanzu, baada ya kufikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, kwa kosa la kutishia kwa bastola. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu alia uhaba majaji

**Na Romana Mallya**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amesema upungufu wa majaji nchini umesababisha majaji waliopo kila mmoja kubeba mzigo wa mashauri 518 badala ya 220 kwa mwaka.

Jaji Juma aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati Rais John Magufuli akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni wakiwamo majaji 12.

Alisema kuapishwa kwa majaji hao 12, kumeongeza idadi ya majaji nchini kufikia 78.

"Kati ya majaji 78, tukiwaondoa majaji wawili ambao wana majukumu maalum, nguvu kazi yetu kwa sasa ni majaji 76 na hadi mwisho wa mwaka huu, wengine wawili watastaafu, hivyo nguvu kazi itashuka tena hadi majaji 74," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na idadi iliyopo sasa ya majaji nchini, kila jaji atakuwa na mashauri 518 badala ya 220 kwa mwaka.

"Rais Magufuli bado tutaendelea kurudi kwako na kutaka nyongeza ya nguvu kazi," Jaji Mkuu alisema.

Jaji Juma aliwataka majaji wawe na utashi wakati wakifanya kazi zao kwa kuwa wafasi zao, hawatakuwa na polisi wa kuwaangalia, bali wao wenyewe kujichunga kwa mujibu wa sheria.

"Tuhakikishe hukumu zinatoka kwa wakati angalau siku 21 na siku 30 mwenendo wa hukumu uwe umetoka," alisema.

Katika hafla hiyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwaeleza majaji hao kuwa Rais Magufuli alipotembelea Gereza Kuu la Butimba mkoani Mwanza, aliona hali ilivyo mbaya kwa baadhi ya mahabusi kukaa muda mrefu kusubiri kesi zao.

"Wabunge tunapata nafasi ya kutembelea baadhi ya magereza katika maeneo yetu, mimi hutembelea Gereza la Kongwa, tunakutana na mambo, baadhi yanaweza kukutoa machozi, wapo watu waliorundikwa huko, basi kesi ziende kwa wakati na wenye haki wapate haki zao.

"Mna majukumu makubwa, kupewa jukumu la kunyonga mtu ni shughuli pevu, au kufunga mtu maisha, majaji tunawaogopa sana, mna nguvu, tunatumaini mtatutendea haki hasa wanyonge wasiokuwa na mawakili, wasioweza kujieleza vizuri katika tara-

INAENDELEA UK 8

## SHUKRANI

Familia ya RICHARD SEMGALAWE MRISHO wa NHC Michungwani Muheza Tanga wanapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote walioshirikiana nao katika mazishi ya mpendwa wao **Mwl. LUIZA HERIETH MRISHO** tarehe 31/08/2019 na kwenye misa ya kumbukumbu tarehe 11 na 12 Octoba, 2019 katika Kanisa la Mt. Raphael Mdote Muheza Tanga. Shukrani za pekee wanazitoa kwa Padre NGODA wa St. Raphael Mdote, Padre LINZA wa Lusanga kwa Yesu, Dr. MSETI wa Ocean Road Hospitali, Dr. KIBOKO na Dr. KIANGI wa hospitali ya Mzena Dar es salaam. Wapendwa ni vigumu kumshukuru mtu mmoja mmoja lakini kwa tangazo hili tunaomba kila mmoja anayelisoma basi amwambie na mwenzake kwamba familia ya MRISHO wanashukuru sana kwa kushirikiana nao katika msiba huu.



Mwl. LUIZA HERIETH MRISHO

Mwenyezi Mungu ailaze Roho yake MAHALA PEMA PEPONI.

**"Bwana ametoa nae ametwaa jina la Bwana lihimidiwe AMINA.**

# JPM ampa maagizo mazito CAG mpya

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametoa angalizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, akimtaka aheshimu maelekezo atakayopewa na mihimili ya serikali.

Kiongozi huyo wa nchi pia amemkumbusha CAG huyo mpya kuwa nchi ina mihimili mitatu tu ambayo ni Bunge, Mahakama na Serikali na hapaswi kubishana nayo.

Akizungumza jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, Rais Magufuli alimtaka Kichere kutekeleza maagizo ya mihimili hiyo na asifikirie kuwa kuna mhimili wa nne.

"CAG mpya nakutakia kazi njema, usije ukaenda huko ukajifanya nawe ni mhimili, mihimili ni mitatu tu na umeiona hapa, kuna Mahakama, Bunge na Serikali. Na katika kiapo chako nilikuwa nakisikiliza, nafasi yako ni Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa hiyo mwenye serikali yupo.

"Kafanye kazi zako za ukaguzi vizuri bila kuonea watu, unapopewa maagizo na mihimili mingine kama Bunge katekeleze, usibishane nao, ukipewa maagizo na mhimili kama Mahakama, kaitekeleze, wewe ni mtumishi," alisema.

MALIPO MARA MBILI

Rais Magufuli pia alimtaka Kichere kuhakikisha anaisimamia vizuri Ofisi ya CAG, akibainisha kuwa baadhi ya watendaji wake, wanapotumwa kwenda kukagua balozi, wanalipwa wakiwa Tanzania na wakifika ubalozini wanaomba fedha, hivyo kulipwa mara mbili.

"Sitaki nikutajie majina yao, nenda ukawachambue

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Mchuuzi wa vikapu, Pius Ndauwa, akitafuta wateja katika eneo la Posta Mpya, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Afariki dunia ghafla baada ya polisi kumvua hirizi kituoni

**Na Romana Mallya**

MKAZI wa Uhemeli Ndala Nzega mkoani Tabora, Michael Pascal, anadaiwa kufariki dunia baada ya askari polisi kumvua hirizi.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi Barnabas Mwakaluka, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, alisema tukio hilo lilitokea Jumamosi.

Akisimulia kuhusu tukio hilo hadi umauti ulipomkuta kijana huyo, Kamanda Mwakaluka alisema Pascal alikuwa anaendesha pikipiki maeneo ya Kashishi akiwa amempakia Ramadhan Khamis, na kwamba askari polisi wa usalama barabara aliyekuwa doria eneo hilo alimsimamisha kwa ukaguzi, lakini alikaidi.

"Aliposimamishwa na askari wa usalama barabarani na kukaidi, askari polisi aliomba msaada kwa watu hawa ambao wote ni wakazi wa Ndala, ndipo alipokamatwa na kupelekwa kituo cha polisi," alisema Kamanda Mwakaluka.

Alisema baada ya kufikishwa kituo cha polisi, utaratibu ni kwamba ili wawekwe mahabusu lazima wapekuliwe.

"Katika upekuzi, Pascal alikutwa na hirizi nyingi mwilini, wakati polisi wakizitoa hirizi hizo hali yake ilibadilika na kukimbizwa Zahanati ya Kashishi, na ilipofika saa tatu usiku alifariki dunia," alisema.

Alisema baada ya kifo hicho ndugu zake walitaarifiwa na walifika kwenye zahahati hiyo na jana (juzi) mwili huo ulihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora kwa uchunguzi zaidi.

"Nini ambacho kimesababisha kifo, anayeweza kukujibu ni mtaalamu wa afya ambaye anaweza kuthibitisha kifo cha Pascal chanzo chake kilisababishwa na nini. Leo (jana) ndugu wamekabidhiwa mwili ili waendelee na mazishi," alisema Kamanda Mwakaluka.

**"Aliposimamishwa na askari wa usalama barabarani na kukaidi, askari polisi aliomba msaada kwa watu hawa ambao wote ni wakazi wa Ndala, ndipo alipokamatwa na kupelekwa kituo cha polisi," alisema Kamanda Mwakaluka.**

Distributed via ippmedia

## Mkuu wa Magereza afanya mabadiliko

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Phaustine Kasike, amefanya mabadiliko madogo ndani ya jeshi hilo kwa kuwahamisha na kuwapandisha maofisa.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, Mrakibu Mwandamizi (SSP) Amina Kavirondo, ilisema katika mabadiliko hayo, aliyekuwa Mkuu wa Parole, Kamishna Msaidizi (ACP) Lupina Lyimo, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Magereza Mkoa wa Manyara.

Aidha, aliyekuwa Mkuu wa Magereza Mkoa wa Manyara, ACP Masoud Kimolo, amehamishiwa makao makuu ya jeshi hilo kitengo cha utawala.

SSP Kavirondo katika taarifa hiyo alisema Mrakibu wa Magereza (SP) Hamza Abdallah, ameteuliwa kuwa Msaidizi wa Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kutuliza Ghasia Magerezani (KMKGM).

Kabla ya kupandishwa na kushika wadhifa huo, Abdallah alikuwa mkufunzi katika kikosi hicho.

Taarifa hiyo ilimnukuu Kamishna Jenerali Kasike kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuimarisha utendaji kazi ndani ya jeshi hilo na kuongeza ufanisi.

## Aliyetishia kuua kwa bastola afikishwa kortini

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Shabani Hamisi, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, akikabiliwa na shtaka la kumtishia kwa bastola, Venance John.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo jana baada kukamatwa na Jeshi la Polisi siku chache kutokana na kuonekana kupitia video iliyosambaa katika mitandao ikimwonyesha anamtishia silaha John ambaye ni dereva wa lori la mchanga.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Mkunde Mshanga, alimsomea mashtaka yake katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Frank Moshi.

Mshanga alidai kuwa Oktoba 30, mwaka huu, katika eneo le Mbezi Mabwepande, Shabani alimtishia John kwa bastola.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alikutwa na bastola aina ya Beleta yenye namba ya usajili 102969 na kwamba kwa makusudi alimtishia John huku akijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Mshtakiwa alikana tuhuma hizo na upande wa Jamhuri ulidai hauna pingamizi la dhamana dhidi yake.

Jamhuri ilidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu alimtaka mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua kutoka taasisi zinazotambulika, vitambulisho vya taifa na watakaotia saini bondi ya Sh. milioni mbili kila mmoja.

Mshtakiwa alitimiza masharti hayo na hakimu amepanga kesi hiyo kutajwa Novemba 13, mwaka huu.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Adili Auction Mart** kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

### MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO

| S/N | Jina la Mdaiwa/ Mdhamini | Jina la Mmiliki | Dhamana inayouzwa | Mahali ilipo Dhamana | Mkoa | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bright Future Distributor Limited | Idrissa Kassim Mangapy | Nyumba ya Makazi | Kichangani - Majohe | Dar es Salaam | 19/11/2019 |
| 2 | Moshi A Mkumba | Moshi A Mkumba | Nyumba ya Makazi | Mvuti | Dar es Salaam | 22/11/2019 |
| 3 | Asha William Shayo | Melania Faustin Luhelamawe | Nyumba ya Makazi | Bangulo - Pugu | Dar es Salaam | 19/11/2019 |
| 4 | Elizabeth J Kisaka | Elizabeth j Kisaka | Nyumba ya Makazi | Liwiti- Tabata | Dar es Salaam | 20/11/2019 |
| 5 | Khamis a Hemed | Khamis a Mandindi | Nyumba ya Makazi | Bombambili - Kivule | Dar es Salaam | 19/11/2019 |
| 6 | Renatus Gabriel Muganda | Renatus Gabriel Muganda | Kiwanja | Kigogo - Kisarawe 11 | Dar es Salaam | 21/11/2019 |
| 7 | Line E Ngesi | Line E Ngesi | Kiwanja | Vumilia Ukooni - Mwanonga | Dar es Salaam | 21/11/2019 |
| 8 | Emmanuel M Mapunda | Emmanuel M Mapunda | Kiwanja | Viziwaziwa - Kongowe | Pwani | 23/11/2019 |
| 9 | Sultan Hamis Kambangwa | Sultan Hamis Kambangwa | Nyumba ya Makazi | Kazole - Mkuranga | Pwani | 24/11/2019 |
| 10 | John Joseph Masikane | John Joseph Masikan | Nyumba ya Makazi | Buza | Dar es Salaam | 22/11/2019 |
| 11 | Mohamed A Mwandola | Mohamed A Mwandola | Nyumba ya Makazi | Mkondogwa - Chamazi | Dar es Salaam | 22/11/2019 |
| 12 | Kiyaka S Mutakyawa | Beatrice Geras Mtakyawa | Nyumba ya Makazi | Upendo - Ubungo | Dar es Salaam | 20/11/2019 |

### MASHARTI YA MNADA

1) Mnunuzi anatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki atakilipa ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.

2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa Nne(10:00 A.M) asubuhi hadi saa Nane (02:00 P.M) mchana.

3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.

4) Dhamana itauzwa "kama ilivyo"

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:-

Mkurugenzi Mtendaji
Amana Bank Limited
P.O.BOX 9771
Dar es Salaam, Tanzania

Tel + 255(022) 2129007/8
Fax 255 (22)2129013

**Adili Auction Mart**
Simu 0717 084658

215499802

## HABARI KITAIFA

# Jafo agoma Jiji Dodoma kuongezewa fedha

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amegoma ofisi yake kuongeza Sh. milioni 241.9 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mfano iliyoko Ipagala kwa kuwa fedha za kazi hiyo zilishatolewa.

Hatua hiyo imetokana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuomba kiasi hicho cha fedha, huku tayari Tamisemi ikiwa imeshatoa fedha zote Sh. milioni 706.4 lakini ujenzi haujakamilika.

Akikagua maendeleo ya ujenzi huo jana, Jafo alisema serikali imetoa fedha hizo na matarajio yake ni kuona shule inakamilika lakini ameona hali ni tofauti.

Kwa mujibu wa Jafo, kuna maeneo mengine kama Morogoro wamepelekewa kiasi hicho cha fedha na ujenzi umekamilika na wamemwomba aende akazindue.

"Mkurugenzi hapa tumewapa Sh. milioni 700 matarajio yangu shule ikamilike lakini ajabu hapa mnataka mwongezewe kiasi kingine cha fedha. Hii haiwezekani. Kwa nini mmepanga kufeli kabla? Niseme ukweli hapa sijaridhika, mnafanya vizuri katika miradi mingine lakini hapa hamjanifurahisha,"alisema Jafo.

Alisema matofali waliyotumia ya nchi sita hakukuwa na sababu ya kulaza kwa kuwa hakuna jengo lingine juu na matofali yamepimwa na kuridhika na ubora wake kuwa ni wa hali ya juu.

"Hapa mimi niwaeleze ukweli mmeniboa, Tamisemi imetoa hii uniform (sare) maeneo yote ninyi Dodoma mmekuja na option (mbadala) nyingine tofauti. Wenzenu wengine wanalia hawajapelekewa fedha ninyi mnataka muongezewe. Hapa niwaambie mmejiingiza kwenye gharama zisizo na sababu. Mpaka Novemba 30 mkamilishe ujenzi," alisema.

Alitoa maelekezo ya kuchora michoro kwenye madarasa kama matunda au namba ili kutambulisha kama darasa la awali na hiyo itamvutia mtoto kwa mazingira lakini pia kuwa sehemu moja ya kujifunza.

Awali, akisoma taarifa ya ujenzi, Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Charles Mabeho, alisema kati ya fedha walizopewa na serikali kwa ajili ya ujenzi, Sh. milioni 677.4 zimetumika na zilizobaki ni Sh. milioni 29.

Alitaja matatizo yaliyopo kuwa ni tatizo la mtandao wa malipo kufungwa na kuchelewa kufunguliwa, mafundi wa vyoo kuomba kazi ya ujenzi kwa gharama ya juu na kuilazimisha halmashauri kutangaza upya kazi hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema kilichotokea ni fundisho kwao katika utekelezaji wa miradi kwenye maeneo mengine kwa kuwa kabla ya kufikia uamuzi uliochukuliwa ilipaswa kuwasiliana na Tamisemi kwanza.

"Naomba nikiri kosa maana umepewa fedha, umepiga hesabu ukaona huwezi kujenga madarasa kwa kiasi hicho cha fedha. Ni lazima utoe taarifa kwa aliyetoa fedha hizo. Hospitali ya Uhuru ilitokea hiyo lakini wataalam wakakaa na kushusha gharama kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa," alisema

Naye Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema changamoto waliyoipata hapo ilikuwapo pia kwenye ujenzi wa jengo la sekondari Dodoma hali iliyowalazimu kutoa Sh. milioni 60 ili kuongezea.

"Gharama hizi zimetokana na kulaza matofali lakini tunaahidi kukamilisha ujenzi huu. Tuna bajeti ya ndani takribani Sh. bilioni nane, hivyo tuta 'top' (ongeza),"alisema Kunambi.



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe (kushoto) na viongozi wenzake, wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ushahidi wa Mbowe waibua mazito

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amedai mahakamani kwamba upinzani umeshambuliwa katika matukio mbalimbali ikiwamo wanachama wake kuuawa, kujeruhiwa na kutekwa na mpaka leo hakuna taarifa wala watuhumiwa waliokamatwa na kushtakiwa mpaka sasa.

Kadhalika, amedai chama chake kina lengo la kukibomoa chama tawala na kishike dola kuwaongoza Watanzania kwa kuwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanaongozwa na vyombo vya usalama likiwamo Jeshi la Polisi.

Mbowe alitoa madai hayo jana wakati akijitetea katika kesi ya uchochezi inayowakabili na wenzake wanane katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Akiongozwa na Wakili wa utetezi Peter Kibatala, Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, alidai kuwa pamoja na mambo mengine watu kadhaa akiwamo mwandishi wa habari Daudi Mwangosi aliyeuawa na askari polisi, jeshi hilo awali lilitoa taarifa kwa jamii kwamba ameuawa na Chadema.

Alidai kuwa baadhi ya viongozi wa chama chake akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Mkoa wa Geita, Alphonce Mawazo, aliuawa na mwili wake ulihifadhiwa katika hospitali ya Bugando, jijini Mwanza.

Alidai kuwa jeshi la Polisi lilizuia chama kufanye mazishi mpaka walipofungua kesi ya kuomba kibali cha kufanya mazishi hayo na kuruhusiwa na Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza lakini mpaka leo hakuna taarifa ya uchunguzi wa tukio hulo.

"Mheshimiwa hakimu msaidizi wangu, Ben Sanane, inasemekana alitekwa na vyombo vya dola miaka miwili na nusu iliyopita. Mwanasheria Mkuu wa Chadema, Tundu Lissu, alishambuliwa na watu wasiojulikana lakini mpaka leo hakuna aliyekamatwa kuhusiana na tukio hilo," alidai shahidi huyo wa kwanza wa utetezi.

Alidai kuwa chama chake kilijitahidi kuomba wachunguzi kutoka nje waje nchini kusaidia kuwabaini watu wasiojulikana lakini vyombo vya dola vilikataa.

Pia alidai kuwa jeshi hilo lilizuia mkusanyiko wa kufanya maombi kumwombea Lissu baada ya kupata majeraha makubwa na kwamba serikali na bunge havikushiriki kwa chochote katika kumsaidia matibabu mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki.

Akielezea uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kinondoni, alidai kuwa kiutaratibu mawakala wanatakiwa kupata nakala za utambulisho wa viapo siku saba kabla ya uchaguzi lakini kwa uchaguzi huo, kati ya mawakala 611 wa Chadema ni mawakala wasiozidi 60 ndio walipata nakala hizo.

Alidai kuwa miongoni mwa waliopata nakala hizo ni pamoja na Wakala Mkuu wa majumuisho, Meya wa Ubungo, Boniface Jacob.

Alidai kuwa kitendo cha mahakama kukosa utambulisho mpaka siku moja kabla ya uchaguzi, hakijawahi kutokea na kwamba alimlalamikia Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye alimjibu kwa maandishi kwamba haikuwa sahihi kukosa barua hizo.

kesi hiyo imepangwa kuendelea leo kusikilizwa ushahidi wa utetezi Mbowe.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo unaongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu Faraja Nchimbi, Joseph Kipande, Pendo Makondo, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali Jacqueline Nyantori na Salum Msemo.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vicent Mashinji; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko;, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; na Mbunge wa Kibamba, John Mnyika.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washitakiwa wanakabiliwa na mashitaka 13 likiwamo la kula njama kwa madai kuwa Februari 1 na 16, mwaka jana, Dar es Salaam walifanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz



Vijana wakishusha shehena ya miwa kutoka kwenye lori kwa ajili ya kuuzwa katika Soko la Tandale, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mchungaji mbaroni madai kukutwa na meno ya tembo

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Polisi Mkoani Dodoma linawashikilia watu watatu, akiwamo Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Ashery Mkombola (44) kwa tuhuma za kukutwa na meno ya tembo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mchungaji huyo ambaye ni mkazi wa kijiji cha Mungui, alikamatwa akiwa na meno mawili ya tembo yenye uzito wa kilogramu 15 sawa na tembo mmoja akiyasafirisha kwa pikipiki aina ya Fekon yenye namba za usajili MC 772 AYK akitokea Mungui kwenda Pwaga.

Alisema uchunguzi unaendelea na kuna taarifa za washiriki wengine katika uhalifu huo wanaofuatiliwa ili wakamatwe.

"Ninaagiza wajisalimishe haraka. Pia wasalimishe silaha wanazotumia katika uhalifu huo kwa kuwa msako dhidi yao ni mkali watakamatwa popote walipo." alisema Muroto.

Katika tukio lingine Kamanda Muroto alisema maeneo ya stendi kuu ya mabasi ya Nanenane walikamatwa watuhumiwa wawili wanaume wakiwa na vipande 16 vilivyokatwakatwa sawa na meno sita ambayo ni tembo watatu.

Alisema mbinu waliyotumia ni kuficha katika dumu la lita 20 lililokatwa juu na kutumbukizwa ndani ya mfuko wa 'shangazi kaja' na juu yake kuweka mkaa.

Kamanda Muroto alisema majina ya watuhumiwa yanahifadhiwa na uchunguzi zaidi unaendelea kuwapata washiriki wengine na silaha zilizotumika katika uhalifu huo.

Pia alisema katika msako unaoendelea, wamekamatwa watuhumiwa 10 kwa makosa ya kuvunja nyumba usiku, mchana na kuiba na kwamba wapo waliokamatwa kwa kuhifadhi mali za wizi.

Alizitaja mali zilizokamatwa kuwa ni televisheni 13 za 'Flat Screen', simu moja, redio moja na kompyuta ndogo mbili.

Muroto aliwataja waliokamatwa kuwa ni Amani Ally (26), Juma Saidi (32), Jumanne Ernest (21), Jafari Juma (25), Joseph Donald (30), Mena Ramadhani (52), Lekresia Mchiwa (36), Fatuma Mchiwa (35), Catherin Mtaturu (52) na Charles Mjema (52).

Distributed via ippmedia

# Amnyonga mkewe kisha naye kujinyonga

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKAZI wa Kijiji cha Mwanima, Kishapu mkoani Shinyanga, John Paulo (27) amedaiwa kumuua mkewe Pendo Nela (20) kwa kunyonga shingo kisha na yeye kujiua.

Tukio hilo lilitokea majira ya saa 3:00 usiku wakati wanandoa hao wakiwa wamelala, ndipo walipoanza kulumbana na kisha kupigana na kusababisha mauaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alisema jana kuwa baada ya mwanamume huyo kumuua mke wake, alikimbilia kijiji cha jirani cha Mwakolomwa na kujinyonga kwenye mti kwa kutumia kamba ya chandarua.

"Tulipata taarifa ya tukio hili jana (juzi) na askari walifuatilia na kukuta tayari mwanamke huyo ameshapoteza maisha huku mume wake naye akiwa amejinyonga kwa kutumia kamba ya chandarua kwenye kijiji jirani alikokimbilia," alisema Abwao.

"Chanzo cha tukio hili ni wivu wa kimapenzi. Mwanamume alikuwa anamtuhumu mke wake kuwa si mwaminifu kwenye ndoa yao. Miili yao imehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Kishapu," aliongeza.

Aidha, kamanda alitoa wito kwa wanandoa wanapokuwa na migogoro ya kifamilia, washirikishe wazazi wao, wazee maarufu na viongozi wa dini badala ya kuanza kulumbana na kufikia hatua ya kupigana na hatimaye kusababisha mauaji, hatimaye kuwaacha watoto wakibaki yatima.

**"Tulipata taarifa ya tukio hili jana (juzi) na askari walifuatilia na kukuta tayari mwanamke huyo ameshapoteza maisha huku mume wake naye akiwa amejinyonga kwa kutumia kamba ya chandarua kwenye kijiji jirani alikokimbilia," alisema Abwao.**


COPS AUCTIONMART & COURT BROKERS LTD.

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **CRDB BANK PLC** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa wake kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini, mnada utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya siku 14 kuanzia tarehe ya Notisi/Tangazo hili.

| Na. | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Azizi Issa Chakupewa | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 184, Kitalu 'PP' yenye CT Na.39856 MTW, LO Na. 114199, iliyopo eneo la Likotwa **LINDI** Mjini. | 21/11/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 2 | Nelson Ignas Beno | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 98, Kitalu 'FF' yenye CT Na.4087 MTW LO Na. 188803, iliyopo eneo la Mlandege Manispaa ya **LINDI.** | 22/11/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 3 | Joseph James Msanjila | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 418, Kitalu 'RR' iliyopo Manispaa ya **LINDI.** | 21/11/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 4 | Swaleh Mohamedi Komba | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 338, Kitalu 'B' yenye CT Na.9900 MTW, LO Na. 596508, iliyopo eneo la Mitwero Manispaa ya **LINDI.** | 22/11/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |
| 5 | Swaleh Mohamedi Komba | Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 59, Kitalu 'XX' yenye CT Na.2537 MTW, LO Na. 344630, iliyopo eneo la Nachingwe, **LINDI** Mjini. | 22/11/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo (as is where is basis)
2. Mteja anatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya kiasi kilicho salia ndani ya siku 14, hatarudishiwa kiasi cha fedha alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI
5. Kijana yeyote aliye chini ya miaka 18 hatoruhusiwa kushiriki mnada.
6. Kwa yeyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**COPS AUCTION MART & COURT BROKERSLTD**
**S.L.P. 12508 DAR ES SALAAM.**
**Simu: +255 (0)22 2861 565, Cell: +255 753 885 050, +255 788 899 099**
**www.copsauctionmart.com**
**Au:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**CRDB BANK PLC**
**S.L.P 266 LINDI**
**Simu: +255 (0)23 220 2385**
**http/www.crdbbank.com**

215499902



## KUMBUKUMBU



**MATILDA M. MAYAYA.**
**(23/03/1946 – 05/11/2018)**

TAREHE 05/11/2019 MAMA YETU UMETIMIZA MWAKA MMOJA TANGU UITWE NYUMBANI KWA BWANA.

INGAWA HAUPO NA SISI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA KATIKA SALA NA MAOMBI. ULIKUWA NGUZO YETU IMARA KATIKA MAISHA YETU. BUSARA NA HEKIMA ZAKO ZITAENDELEA KUTUONGOZA KATIKA MAISHA YETU DAIMA. HAKIKA PENGO ULILOLIACHA HALITAZIBIKA KAMWE.

UTAKUMBUKWA DAIMA NA MUMEO, WATOTO, WAJUKUU NA NDUGU ZAKO WOTE PAMOJA NA MAJIRANI ZAKO.IBADA YA KUMBUKUMBU ITAFANYIKA KATIKA KANISA LA LUTHERAN IGUNGA TAREHE 25/12/2019
PUMZIKA KWA AMANI MBINGUNI KWA BWANA.

**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA, JINA LA BWANA LIHIMIDIWE. AMINA.**

215495402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera awamu ya 5 imefanya yaliyotukuka

**SERIKALI** ya Rais John Magufuli, inapomaliza kipindi cha miaka minne, Tanzania inashuhudia mambo makubwa yaliyoleta mafanikio kwenye sekta zote kuanzia uchumi hadi ulinzi na usalama.

Ujenzi wa miundombinu kama reli ya kisasa, viwanda, ununuzi wa ndege zinazofanya safari za ndani na za kimataifa, kuboresha sekta ya jamii ikiwamo elimu ni mambo yanayoiweka Tanzania kwenye orodha ya mataifa yanayobadilika kwa kasi.

Tunawapongeza Rais Magufuli, Makamu wake, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa. Tunaona kuwa kila Mtanzania anapoulizwa swali kuhusu utendaji wa awamu ya tano anajibu moja kwa moja kwa kutaja kazi zinazofanywa na viongozi hawa.

Tunapenda kuipongeza serikali kwa mafanikio mengi kuanzia kutatua changamoto za ardhi na kumaliza migogoro mingi iliyokuwa inatatiza sekta hii na kusababisha usumbufu mwingi mikoani, vijijini hata miongoni mwa wawekezaji.

Awamu ya tano imekuwa kielelezo cha mafanikio kwenye uwajibikaji uliotukuka na kuhakikisha kuwa viongozi wanafanyakazi kwa mujibu wa kanuni na sheria za utumishi wa umma.

Aidha, kwa namna ya kipekee tunapenda kugusia hatua za hivi karibuni za kuzishughulikia moja kwa moja changamoto kubwa zinazowatatiza wananchi wa vijijini na mijini kwenye maeneo ya miundombinu pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa maji.

Tunapoungana na Watanzania kuadhimisha miaka minne ya Awamu ya Tano, tunaipongeza hatua ya kipekee ya kuanzisha Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) ambaye amepewa jukumu muhimu la kujenga na kukarabati barabara za mijini na vijijini ambazo siku za nyuma zilikuwa zinashughulikiwa na halmashauri.

Uwapo wa Tarura ni mafanikio makubwa kutokana na ukweli kuwa ujenzi wa barabara, madaraja na makalavati ambayo pengine kutokana na urasimu kazi hazikufanikiwa kama ambavyo Tarura sasa imesimama kidete.

Tunaipongeza awamu hii kwa kuhakikisha kuwa pamoja na barabara kuu na za kitaifa kuiunganisha mikoa na nchi jirani, wilaya zote, vijiji na mitaa mijini na vijini hazijasahaulika zinaunganishwa na kuimarishwa jukumu linalofanywa na Tarura.

Watanzania wana kila sababu ya kufurahia na kusherehekea mazingira na maeneo wanayoishi kwa sababu barabara zimeboreshwa na kuziwezesha jamii kusonga mbele kwa kurahisishiwa usafirishaji uwe wa watu, mazao na pembejeo na hilo sasa si tatizo tena.

Kila mmoja anayependa maendeleo na anayefahamu kuwa Tanzania ya sasa si ya kutegemea uhisani bali ni ya kutumia rasilimali zake kwa ajili ya maendeleo ya raia wake.

Ndiyo maana tunazidi kuipongeza serikali kuwa na jicho la tatu kwenye sekta ya maji. Kuundwa Mamlaka ya Maji Vijijini ambayo haiingiliana na Mamlaka ya Maji Mijini kama DAWASA kwa Jiji la Dar es Salaam ni hatua kubwa ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Kwa miaka minne tumeshuhudia umakini wa serikali katika mapambano dhidi ya rushwa. Bila kupiga vita rushwa, nchi haiwezi kupata maendeleo kwa kuwa rushwa ni adui mpya wa Taifa baada ya maadui watatu waliotajwa baada ya Uhuru ambao ni maradhi, ujinga na umaskini.

Safu hii haitoshi kueleza mafanikio yote ya miaka minne, lakini tumalizie kwa kupongeza utoaji wa elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari, hivyo kuwezesha watoto wengi wa maskini wakipata fursa ya kusoma.

Hongera awamu ya tano kwa kuongeza uwajibikaji na utumishi uliotukuka kwa kuhakikisha wenye dhamana wanatimiza wajibu na kuwatumikia Watanzania

Hongera Rais Magufuli, Samia na Majaliwa. Mungu azidi kuwabariki na kuineemesha Tanzania

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kidato cha nne, imalizeni safari yenu kwa mafanikio

**JUMLA** ya watahiniwa 485,866 wakiwamo wavulana 229,838 na wasichana 256,028 wameanza mtihani wa kuhitimu kidato cha nne, ikiwa ni mwisho wao wa kupata elimu bure kulipa ada.

Distributed via ippmedia

Hii inatokana na utaratibu uliowekwa na serikali wa kutoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne na sasa hatua inayofuata ni wazazi kulipa ada mara watoto wao watakapofaulu kuendelea na masomo.

Ni jambo jema kwa wanafunzi kuzingatia kile ambacho wamejifunza wakiwa shuleni na kukifanyia kazi.

Ninasema hivyo, kwa sababu kumekuwa na taarifa kwa nyakati tofauti ya baadhi yao kuchora vitu vya ajabu, kufutafuta au kuchora picha wanazojua wenyewe kwenye karatasi za mitihani.

Ndipo hapo Muungwana anaposhangaa kuona mwanafunzi wa sekondari akiamua kufanya uhuni wa aina hiyo, hali inayoonyesha kwamba hajui umuhimu wa elimu.

Wanafunzi wanaohitimu sasa ni wale ambao wamefaidika na utaratibu wa serikali wa kutoa elimu bure, ulioanza mwaka 2016 wakati wao wakiwa kidato cha kwanza, hivyo fursa hiyo isiishie kidato cha nne.

Serikali imeshaweka wazi kwamba inaendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika elimu na kwa sababu hiyo na ndio maana mwaka 2019/20 imetenga bajeti ya Sh. bilioni 288.485 kutekeleza mpango wa elimu bila malipo.

Ikumbukwe kuwa tangu mpango huo wa elimu bure uanze mwaka 2016, serikali imeshatumia Sh. bilioni 937.54 kugharamia elimu ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini.

Juhudi hizo ni za kuunga mkono na wanafunzi kwa kufanya vizuri katika mitihani badala ya kufanya madudu kama ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (Necta).

Kutokana na umuhimu wake, elimu imekuwa na kaulimbiu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulinganishwa na ufunguo na nyingine nyingi kwa kutambua kwamba mafanikio kwa kila mtu mara nyingi huletwa na elimu.

Ndiyo maana wazazi na walezi wote wanapaswa kuwahimiza vijana wao wasome kwa kutambua kuwa wao ni taifa la kesho ama nguvu kazi ya taifa hili kwa baadaye.

Jambo la muhimu ni wadau wote wa elimu wakiwamo wazazi na walezi kuhakikisha wanawahimiza watoto wote walioandikishwa kufanya mtihani huo wanafanya bila kukosa.

Kwani wanafunzi wa kidato cha nne wanapofanya mtihani wanatakiwa wajitambue wao ni nani na wanatarajia nini baadaye kuliko kufanya madudu ya kukusudia.

Vilevile watambue kuwa elimu ni msingi mkubwa wa maendeleo binafsi pia taifa kwa ujumla, hivyo waamue kwamba miaka yao minne waliyokaa shuleni haipotei bure na badala yale waitendee haki kwa kufanya mitihani ya taifa kikamilifu.

> **Ndipo hapo Muungwana anaposhangaa kuona mwanafunzi wa sekondari akiamua kufanya uhuni wa aina hiyo, hali inayoonyesha kwamba hajui umuhimu wa elimu.**

Wafanye wakitambua kuwa viongozi wa taifa la kesho wanatokana na wao, na bila kuzingatia hilo wanaweza kujikuta kwamba miaka yao minne shuleni haikuwa na tija.

Kama anavyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kuwa viongozi na watendaji wote washiriki kwenye usimamizi na uendeshaji wa mitihani hiyo, basi watimize wajibu.

Waziri anawataka wafanye kazi zao kwa weledi, maadili na kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa mitihani hiyo kama ilivyoelekezwa na Necta.

Kwa utaratibu huo anaoelekeza waziri, ni wazi kwamba tatizo la kuwapo kwa baadhi ya wanafunzi wanaofanya vituko vya makusudi kwenye mitihani wanaweza kupungua kama siyo kumalizika kabisa.

Ingawa kuna urithi wa vitu mbalimbali ambavyo mtoto anaweza kupata kutoka kwa wazazi wake, urithi mkubwa na wa maana ni elimu na ndiyo imekuwa ikisisitizwa na wadau wa elimu.

Hivyo ni wajibu pia kwa kila mwanafunzi kuitendea haki elimu anayopata, tangu anapoanza shule hadi kwenye mitihani ili iweze kuwa na manufaa kwa maisha yake ya baadaye anapoingia uraiani.

# HABARI KITAIFA

## Hii kero Mikese hadi lini?

***Ndugu Mhariri***

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je, kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*

*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

***Ahsante ni sisi wanakitongoji, Ukomanga-Fulwe, Mikese.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA**



Vijana wakiwa katika maonyesho ya mitindo mbalimbali ya mavazi.**PICHA: MTANDAO**

## Mavazi ya staha muhimu dunia hii ya utandawazi

Distributed via ippmedia

**Na Raphael Kibiriti**

MAVAZI ni moja ya vitambulisho vya taifa lolote lile, jamii, kabila na hata makundi mbalimbali katika jamii.

Na ndiyo maana ya maneno kama vazi la taifa, vazi la michezo, sare za mahitaji mbalimbali na hata kuna baadhi ya watu hujiwekea utambulisho binafsi kupitia mavazi.

Uzuri au ubaya wa kitu, ni tafsiri mbalimbali ambazo zinafanya nafsi ya mtu kujieleza, mara nyingi mavazi katika namna ya kipekee yana nafasi kubwa zaidi ya kuwasilisha ujumbe.

Pamoja na uzuri wa kitu au mambo, unaopatikana kupitia mavazi, katika sura ya pili matumizi mabaya au upotoshaji wa namna yoyote katika matumizi yake, yamezua matatizo makubwa katika jamii, hata kufarakanisha wanafamilia.

Sasa malalamiko yametawala, kiasi cha kwamba hata kwenye nyumba za ibada, ambako kunaheshimiwa kwa namna ya kipekee, matumizi mabaya ya mavazi moja kwa moja huwasilisha ujumbe wa kutoheshimu sehemu hizo.

Kimsingi, tafsiri ya mavazi ya heshima hutegemea imani, mila na desturi ya jamii husika.

Hivyo, mavazi ya heshima ni yale yanayozingatia mila na desturi za jamii katika hatua mbalimbali zilizoko, hadi ngazi ya taifa.

Vazi linaloendana na mahitaji ya jamii na miongozo ya ngazi hizo husika, yana maana kubwa sana.

Mathalani, katika sehemu nyingi staha ya mwanadamu ni kuvaa nguo inayohifadhi baadhi ya sehemu za maungo ya miili yao, ambazo kwa mujibu wa imani na desturi, si mahali pa kuachwa wazi.

Kwa kutumia kigezo hicho hicho, ndiyo inazaa marufuku kwa baadhi ya mavazi, ama yasivaliwe kabisa au hayapaswi kuvaliwa katika baadhi ya mazingira na maeneo mbalimbali, mfano hai ukiwa ni kutoruhusu mavazi ya michezo kuvaliwa na wafanyakazi katika sehemu wanakotumikia.

Tafsiri hiyo inaenda mbali zaidi kwa kina mama kuambiwa mavazi yanayobana, mafupi yanayoacha magoti na sehemu za mwili wazi, hali kadhalika kitovu na kifua.

Mwaka 1971, chama cha TANU ambacho kilikuwa kimeshika hatamu za uongozi wa nchi wakati huo, kilitoa waraka maalumu wenye mwongozo kuhusu mavazi.

Madhumuni ya waraka huo, yalikuwa kuimarisha heshima ya taifa, kwa mujibu wa imani ya jamii yake, ikilenga kuhakikisha kuwa watumishi katika sehemu za kazi wanadumisha staha ya heshima wawapo kazini.

Tukichukua kinachojiri leo mbele ya umma kuhusu mavazi na kilichoagizwa kwenye waraka huo wa Tanu, tofauti ni ya kutisha. Mitindo ya mavazi hivi sasa inaporomosha thamani ya jinsia zote mbili katika jamii. Kwa kifupi hali ni tete.

Pengine hali ingekuwa ni mbaya zaidi, lakini tunapaswa kuzishukuru asasi za kidini, sehemu ambako imani ya umma imeshikiliwa.

Kwa watoto wa kike, imekuwa sehemu ya maisha yao kuvaa nguo fupi zinazoonyesha umbile la miili yao.

Kwa tafsiri yao, wanajihisi wanakuwa warembo zaidi na wanakubalika katika jamii yao ya Kitanzania, kwa kukumbatia utashi huo wenye mzizi kwenye utandawazi.

Ni jambo linalowagharimu wengi katika jamii, baadhi wakifukuzwa au kuzuiwa kuingia kwenye ofisi na nyumba za ibada au hata kutokukubalika katika makazi binafsi.

Jumuiya ambayo msingi wake ni mkusanyiko wa watu kwa lengo maalumu ina tafsiri pana, pia huendana na haja ya mtu mmoja mmoja au kikundi kutaka kukubalika nayo.

Inaweza kuwa kwenye kituo cha basi, sokoni, hospitali, nyumba za ibada, shuleni au vyuoni.

Moja ya tiketi muhimu katika kujumuika nayo ni vazi linalokubalika, kama nguo ndefu kwa kinamama ambayo ina kawaida ya kumbandika alama ya kimantiki kuwa mvaaji ni mstaarabu.

Katika mavazi kuna neno kujisitiri ambalo maana yake ni kuficha kitu mahali ili kisionekane.

Lakini kwa karne ya sasa wanaume kwa wanawake, wamekuwa wakivaa mavazi yasiyo na staha kwenye jamii.

Mjadala una rai kwa jamii ya sasa kujirekebisha kimavazi kwa kuvaa nguo zenye staha, na kujikita kwenye maadili kama jinsi mababu zetu walivyokuwa wakiishi, kwa kufuata mila na desturi za taifa letu.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# JPM ampa maagizo mazito CAG mpya

INATOKA UK 2

mwenyewe, Ofisi ya CAG siyo safi kama mnavyofikiria, nenda kachambue, ukapange nafasi za watu wako, ili 'mauchafu' haya ukayasafishe.

"Ninajua una sifa nzuri na huwa hatufanyi makosa tunapoteua, kidato cha nne ulitoka na daraja la kwanza, kidato cha sita ukatoka na daraja la kwanza, hii ni kuonyesha wewe ni kipanga, si kilaza.

"Ukaenda kuchukua shahada ya sheria, shahada ya uhasibu ukatoka na ufahulu wa daraja la pili la juu, ukachukua shahada ya umahiri na umefanya kazi mahali tofauti, tunakuamini na pia una heshima.

"Umetolewa kwenye Kamishna Mkuu wa TRA, hukusema neno, wewe ni mnyenyekevu, mpole, ukaenda kufanya kazi huko, hukutamka neno, wapo ukiwateua wanafikiri ni nafasi zao, unampa u-DC (Mkuu wa Wilaya), ukimtoa anaanza kulalamika, sasa mbona hukulalamika wakati nikikuteua? Kafanye kazi," alisema.

**MAMLAKA YA UTEUZI**

Rais Magufuli alisema katiba na sheria zinaeleza kuwa CAG anaweza kukaa madarakani kwa miaka mitano ya mkataba wake au mwaka mmoja.

"Kwa sababu taratibu za kukutoa zipo na zinafanywa na Rais, lakini sikutishi nenda kafanye kazi, katika maisha ya duniani huwezi ukapewa mamlaka ya kuteua halafu usiwe na mamlaka ya kutengua, ukishindwa hivyo, hufai kuwa Rais na hufai kuwa kiongozi, nenda kasimamie kazi yako vizuri.

"Mwenzako aliyekuwapo amemaliza kipindi chake cha miaka mitano na kinaisha leo (jana) saa sita usiku, kuanzia kesho (leo) uende pale ofisini kufanya kazi, ukamtangulize Mungu na kutimiza wajibu wako, kayatoe 'mauchafu' yaliyopo hapo. Mengine watakueleza Wizara ya Fedha ambayo wanayafahamu vizuri zaidi," alisema.

**VIBALI HEWA**

Rais Magufuli alimweleza Kamisha wa Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Francis Mbindi, kuwa kwenye ofisi hiyo kuna vibali hewa na wapo wanaoletwa Tanzania kufanya kazi ambazo zingefanywa na Watanzania.

"Marata (aliyekuwa Kamishna wa Kazi, Gabriel Marata) alifanya kazi yake vizuri ndiyo maana nimekaa muda mrefu naangalia nani wa kumpa, nimeangalia kote nikaona hapa panafaa mwanajeshi mwenye taaluma zote, kwa sababu umesoma vizuri na umefaulu ukaenda vyuo vya kijeshi hadi Marekani.

"Umefanya kazi nzuri Jumuiya ya Afrika Mashariki, una cheo kizuri, ni Kanali, sasa kawanyooshe pale Wizara ya Kazi. Wakati Marata yupo pale kulikuwa na malalamiko mengi, nataka yakaongezeke zaidi, ukilalamikiwa maana yake unafanya kazi.

"Kasimamie ofisi ile, isije nikakupeleka pale mwanajeshi halafu kazi zikawa za ovyo, utakuwa umewaaibisha wanajeshi pamoja na CDF (Mkuu wa Majeshi), vibali vya ovyo, wapo wanaovitoa pale kwa kushirikiana na wizara nyingine, kavisimamie," aliagiza.



Mafundi wa kampuni ya Nyanza Road, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Kitunda Kivule nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam jana, kutekeleza agizo la Mkuu wa mkoa huo, kuzitaka kampuni zote za ujenzi kutimiza wajibu wao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jaji Mkuu alia uhaba majaji

INATOKA UK 2

tibu za kisheria, mtawaangalia katika jicho la kipekee," alishauri.

Spika Ndugai pia alitumia fursa hiyo kumkaribisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, na kumweleza kuwa Bunge linaanza kazi leo.

"Bunge kazi yake ni kupitisha bajeti na baadaye serikali inatumia na matumizi hayo CAG ndiyo jicho letu, tunakutegemea kama jicho letu, maana jicho ndiyo kila kitu kwa mwanadamu, ukikosa jicho, siyo rahisi kujua unaelekea wapi.

"Wewe ni chombo muhimu na kushauri kuona namna gani matumizi mbalimbali yanavyokwenda, namna ya kurekebisha, kwa namna hiyo bungeni zipo kamati mbili, ipo Kamati ya mahesabu ya serikali na kamati ya mahesabu ya serikali za mitaa na nyingine," alisema.

Alimweleza Kichere kuwa kazi ya ofisi aliyopo sasa ni nzito lakini akaahidi kuwa Bunge litamsaidia ili imani ya Rais Magufuli aliyoionyesha kwake ailinde.

**"Wewe ni chombo muhimu na kushauri kuona namna gani matumizi mbalimbali yanavyokwenda, namna ya kurekebisha, kwa namna hiyo bungeni zipo kamati mbili, ipo Kamati ya mahesabu ya serikali na kamati ya mahesabu ya serikali za mitaa na nyingine," alisema.**

# Serikali yazuia kampuni kupewa zabuni ya maji

**Na tiganya Vincent, SIKONGE**

SERIKALI imepiga marufuku Kampuni ya Monmar and Sons ya Mkoani Tabora kupewa kandarasi ya ujenzi wa mradi wa usambazaji wa miundombinu ya maji katika vijiji vinne vya Kata ya Kitunda wilayani Sikonge kutokana na kutoridhishwa na ubora wa kazi zake katika baadhi ya maeneo nchini.

Mradi huo ambao ulikuwa ni kujenga chujio la maji, ujenzi wa tenki la maji na ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa maji kwa gharama za awali ulikuwa ugharimu Sh. milioni 900, lakini baada ya Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa, kufanya hesabu unatakiwa kutumia milioni 700.

Waziri huyo alifanya uamuzi huo jana mjini Sikonge wakati wa ziara yake ya siku moja ya kusikilizia matatizo ya maji ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi. Alisema katika maeneo mengi ambayo Kampuni hiyo ilipewa miradi katika Mkoa wa Tabora na Katavi ukamilishaji wake umekuwa sio wa kuridhisha kwa kuwa imekuwa ikijengwa kwa kiwango cha chini na kuonekana na dosari muda mfupi baada ya kuzinduliwa.

Makame alisema mfano ni ujenzi wa tenki la maji katika Kijiji cha Songambele wilayani Sikonge ambalo linavuja na kusababisha upotevu wa maji. Aliutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kumchukulia hatua ikiwamo kumtaka kujenga upya tenki hilo na kumpa taarifa ndani ya wiki moja.

Aidha Prof. Makame alisema Wizara ya Maji itatoa Sh. milioni 250 za awali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo wa kusambaza maji kutoka katika Bwawa la Igumila kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakazi wa Kata ya Kitunda.

Aliwataka kutumia mafundi jamii wakati wa utekelezaji wa mardi huo ili kupunguza gharama za awali ambazo walikisia kutumia Sh. milioni 900. Naye Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri, alisema ni lazima ndani ya kipindi alichoagiza Waziri wa Maji kuhusu kufanyia marekebisho kasoro katika mradi wa Kijiji cha Songambele yanafanyika la sivyo atalazimika kumkamata la kumsweka ndani.

# Assad: Sina kinyongo, nakwenda kufuga kuku

INATOKA UK 2

anafikiri kusamehe ni jambo muhimu kwa watu wote.

Alipoulizwa kuhusu mipango yake ya maisha baada ya kuondoka katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Prof. Assad alisema: "Sina 'position' (nafasi) yoyote kwa sasa, nipo kwenye kitu kinachoitwa maandalizi ya kustaafu, nimekaa nyumbani nikiwa nina (umri wa) miaka 58," alisema.

Prof. Assad alisema kwa kuwa taratibu za nchi haziruhusu CAG kufanya kazi yoyote ya serikali baada ya kuondoka katika nafasi yake hiyo, atalazimika kurejea nyumbani kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji.

"Ninakwenda kufuga kuku, tuna mashamba tumeyaanzisha, nina mambo mengi ya kufanya," alisema.

Nipashe pia ilimuuliza msomi huyo kama ana ushauri kwa CAG mpya, akaeleza kuwa leo wakati wa kukabidhi ofisi, atatoa ushauri kwa mwanafunzi wake huyo.

"Kesho (leo) nitakutana na Kichere Dodoma, nitampatia ushauri wangu, yule ni mwanafunzi wangu, nilimfundisha," alisema Prof. Assad.

Desemba Mosi, 2014, Ikulu ilitangaza kuwa Rais Jakaya Kikwete alikuwa amemteua Prof. Assad kuwa CAG na uteuzi wake ulikuwa umeanza tangu Novemba 5, mwaka huo.

Kabla ya uteuzi huo, Prof. Assad alikuwa Profesa Mshiriki, Idara ya Uhasibu, UDSM na alichukua nafasi ya Ludovick Utouh, ambaye alistaafu kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma. Ilielezwa kwenye taarifa ya Ikulu siku hiyo kwamba, Prof. Assad ni msomi, mwenye weledi, ujuzi na uzoefu mkubwa wa uhasibu na udhibiti wa fedha ambaye ana Shahada ya Uzamivu wa Uhasibu (PhD in Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Southampton, Uingereza mwaka 2001 na Shahada ya Uzamivu katika Udhibiti wa Fedha (MA in Financial Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Dublin City, Jamhuri ya Ireland mwaka 1991.

**HABARI KITAIFA**

## Maji kunufaisha watu 40,000 kijijini

**Na Said Hamdani, LINDI**

TATIZO la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa matumizi ya binadamu kwa wakazi 4,072 wa Kijiji cha Kilangala B, Tarafa ya Mchinga Wilaya na Lindi, limepatiwa ufumbuzi kufuatia Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC) kupeleka mradi wa kisima kimoja cha maji.

Kisima hicho kilichogharimu Sh. 27,300,000 hadi kukamilika kwake, kimechimbwa na mkandarasi J&M Tast Enginering Limited miezi sita iliyopita.

Wakionyesha furaha wakati wa uzinduzi wa kisima hicho, wakazi wa kijiji hicho, Salima Isumaili, Mwanahamisi Juma, Huseni Salum na Selemani Yusufu walieleza kufarijika kupata huduma hiyo, wakisema kumewapunguzia tatizo la kutembea mwendo mrefu wa zaidi ya kilomita sita kufuata maji vijiji jirani.

Aidha, wakazi hao wamevitaja vijiji ambavyo walikuwa wakipata huduma hiyo kupitia visima vya asili na kwenye mabwawa ni Kilanga Masasi ya Leo, Simu, Kilangala'A', Lichilu na Namadengo.

Wakazi hao walieleza kwamba licha ya umbali, pia upatikanaji wake umekuwa ni wa shida kutokana na kiwango kidogo cha maji kilichopo, hali iliyowafanya kuchukua muda mrefu kuyasubiria.

Waliishukuru TPDC kwa kutusikiliza kilio chao kwa kuwa kwani limetupunguzia tatizo la kutembea mwendo mrefu kufuata huduma hii vijiji jirani.

Pia walisema licha ya kutembea mwendo mrefu, maji hayo sio ya uhakika kwa usalama wa matumizi ya binadamu kwani yanatokana na visima vya asili au mabwawa, ambayo matumizi yake huchanganyika na wanyamapori na mifugo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, akizungumza na wananchi wakati wa uzinduzi wa mradi huo, alisisitiza kutunzwa kwa mradi huo ili uwe endelevu katika kuwapunguzia tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Dk. Mtarajio alisema kupelekwa kwa mradi huo ni moja ya kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli katika kuwaondolea wananchi changamoto zinazowakabili, ikiwamo upatikanaji wa huduma hiyo.

Hadija Mringo, Ofisa Tarafa wa Mchinga, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliishukuru TPDC kwa kupeleka kijijini hapo mradi wa maji, huku akiahidi kuutunza ili kuwasaidia wananchi hao.

# RC ala nyama ya panya, ahamasisha ulaji wake

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, ameonyesha kwa vitendo udumishaji wa mila na desturi za baadhi ya wakazi wa mkoa huo kwa kula kitoweo cha panya hadharani.

Aidha, Byakanwa aliwataka wakazi ambao wanakula kitoweo hicho sasa kula hadharani na hakuna sababu ya kula kwa kujificha kwani nyama ya panya inajenga afya.

Tukio hilo la Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kula panya alilifanya jana mkoani hapa akiwa na waandishi wa habari alipokuwa akizungumzia kuhusu mila na desturi katika mkoa huo kwa lengo la kudumisha mila hizo.

Alisema ni mwenyeji wa Mkoa wa Kagera, na kwamba wakazi wa mkoa huo wana mila zao ikiwamo kula vyakula vya mila na utamaduni kama panzi aina ya senene, hivyo kila sehemu kuna aina ya vyakula vya asili.

Alisema ameamua kula panya ili kuhamasisha wale wote ambao wana utamaduni wa kula panya wasifikiri kama kitoweo hicho hakitambuli bali kinatambulika kama vyakula vingine vya asili.

Byakanwa alisema ingawa yeye mwenyeji wa Kagera, lakini kwa sasa ni kiongozi ambaye anawaongoza watu ambao baadhi yao mila na desturi wanatumia panya kama chakula.

"Mimi leo nimekula panya na ukiniuliza kama ana radha gani nitakuambia kuwa ni mtamu sana, hivyo sasa nawaomba wale wote waliokuwa wanakula kwa kujificha wale hadharani," alisema Byakanwa.

Alisema panya ni chakula kama ilivyo vyakula vingine na ndio maana wataalamu wa afya wanaeleza kuwa nyama ya panya ina virutubisho kama vilivyo kwenye nyama zingine za ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Alisema kuanza sasa akiwa mkoani Mtwara ataendelea kula panya ili kuhamasisha mila na desturi za baadhi ya watu wa kusini wanaokula panya.


Distributed via ippmedia

Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakikagua mita za wateja katika eneo la Mji Mpya, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Tanesco waliendesha zoezi la kukagua mita kubaini wezi wa umeme ambapo jumla ya wateja 13 walikamatwa kwa kuiba umeme. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mawimbi ya runinga kupeleka huduma intaneti

**Na Mwandishi Wetu, KONDOA**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ameelekeza mawimbi ya runinga yatumike kupeleka huduma ya intaneti vijijini ili jamii iweze kutumia mawimbi hayo kupata huduma ya mawasiliano ya intaneti.

Kamwelwe aliyasema hayo wakati akikagua mnara wa mawasiliano, Kondoa Mjini ambao umefungwa vifaa maalum kwa ajili ya kubeba mawimbi ya runinga na kupeleka kwenye kifaa kingine ambapo mawimbi hayo yanabadilishwa na kuweza kutumika kutoa huduma ya intaneti kwenye jamii ya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa, Shule ya Sekondari ya Ura na Chuo cha Ualimu cha Bustani zilizopo wilayani Kondoa, Dodoma.

Kamwelwe alipita kukagua mnara huo na teknolojia hiyo kabla ya kufunga kongamano la nne la mtandao wa intaneti kwenye jamii lenye kauli mbiu isemayo "Kuunganisha Wananchi Kimtandao".

Kongamano hilo lililofanyika kwa muda wa siku 6 kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ambalo lilianza Oktoba 28, 2019 na kumalizika Novemba 2, 2019.

Wakati Kamwelwe akikagua mnara huo, Mkufunzi Msaidizi wa UDOM, Jabhera Matogoro, alimweleza kuwa mawimbi kwa ajili ya runinga yanasafiri umbali wa kipenyo kizichozidi kilomita 20 ambapo baadhi ya maeneo hayafikiwi na mawimbi hayo ambapo kiasi kikubwa cha mawimbi yanabaki bila kutumika ipasavyo.

Matogoro aliongeza kuwa watoa huduma wanapatiwa leseni ya kurusha mawimbi hayo kwenye wilaya au mkoa husika ambapo imebainika kuwa kiasi kidogo cha mawimbi hayo ndio kinachotumika kwa ajili ya kurusha matangazo ya runinga na mawasiliano ya simu za mkononi.

Alifafanua zaidi kuwa katika utafiti wake, amebaini mawimbi hayo yanaweza kubadilishwa kwa kutumia vifaa maalumu kwa kuzingatia ukuaji na maendeleo ya teknolojia ambapo mawimbi ya runinga yanaweza kutumika kupeleka huduma ya intaneti katika jamii husika.

"Lengo kuu ni kuunganisha jamii na wananchi ambao hawajaunganishwa na mtandao wa intaneti kwa kutumia mawimbi ya runinga," alisisitiza Matogoro.

Kamwelwe alimpongeza Matogoro na kubatiza utafiti wake jina la "Teknolojia ya Matogoro" (Matogoro Technology) kwa kuwa amebuni teknolojia hiyo ya kutumia mawimbi ya runinga kupeleka huduma ya intaneti kwenye jamii na kumwahidi kuwa serikali itahakikisha teknolojia hiyo inatumika na kuenea sehemu mbalimbali nchini.

Naye mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Ally Mbena, amemshukuru mtaalamu wa UDOM kwa kuchukua hatua za kutatua changamoto za kijamii na huu ndio usomi.

# CCM Rorya yafunda wanachama wake

**Na Ahmed Makongo, RORYA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) katika Wilaya ya Rorya, mkoani Mara, kimetoa wito kwa wanachama, wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, wote kwa pamoja washikamane pamoja na kuvunja makambi yao yaliyotokana na kura za maoni ndani ya chama hicho.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa CCM katika Wilaya ya Rorya, Charles Ochele Obutu, wakati akizungumza na gazeti hili na kusema kuwa CCM wilayani humo imejipanga vizuri na watahakikisha wagombea wake wanashinda kwa kishindo katika uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa sababu wagombea wote walioteuliwa, chama hicho kimewaona wanazo sifa za kuwa viongozi kwa sababu wanakubalika kwa wananchi.

"Tumejipanga vizuri na tutahakikisha tunapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa serikali za mitaa, tumeteua wagombea wote wenye sifa na wanaokubalika kwa wananchi," alisema Obutu.

Aliwataka wanachama wote wa chama hicho kuwa kitu kimoja na kuwanadi wagombea wote wanaogombea kwa tiketi ya chama hicho waweze kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo wa serikali za mitaa.

Alisema kuwa katika wilaya hiyo kuna vijiji vitano ambavyo wagombea wake walikuwa wameshinda katika kura za maoni, lakini waliachwa na kuchukuliwa wagombea wengine kutokana na sababu mbalimbali ambazo chama hicho kiliziona ni za msingi na zina umuhimu wake wa kipekee.

Alifafanua kuwa kabla ya wagombea hao kuteuliwa chama hicho kilifanya uchunguzi wa kina na kujiridhisha kwamba walioteuliwa wanazo sifa zinazostahili kuwa viongozi watakaokiwakilisha vizuri, katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Aidha, aliwataka wagombea waliokuwa wameshinda katika kura za maoni kupitia chama hicho, lakini wakaachwa kwenye uteuzi uliofanywa na vikao halali vya chama hicho wasivunjike moyo na badala yake washirikiane na walioteuliwa ili chama hicho kiweze kupata ushindi wa kishindo.

Wakati huo huo, aliwataka wanachama wa chama hicho kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura, ili waweze kuchagua viongozi wanaowataka na ambao watawaletea maendeleo.

# Vyama vyambana Shibuda kuitisha mkutano wa baraza

**Na Enock Charles**

UMOJA wa vyama vya siasa vipatavyo 11, umemtaka Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, John Shibuda, kuitisha mkutano wa vyama vya siasa ili kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Akizungumza na vyombo vya habari mwenyekiti wa umoja wa vyama hivyo visivyokuwa na uwakilishi bungeni na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia (DP), Abdul Mluya, amesema ni muhimu kwa vyama kukutana sasa kabla ya kuingia katika uchaguzi ili kuponya majeraha ya kisiasa yaliyojitokeza katika mchakato wa kuchukua na kurejesha fomu za wagombea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Kanuni kama zilivyo ni nzuri shida ni wasimamizi wa kanuni hizo maana hakuna mahali kanuni zinataka msimamizi kugoma kupokea fomu au kutupilia dirishani kwa hio ni vyema kurekebisha kasoro hizi," alisema Mluya.

Vyama vilivyokutana ni pamoja na Chama cha Kijamii (CCK), Alliance for Democratic Change (ADC), Demokrasia Makini, Tanzania Labour Party (TLP), United Democratic Party (UDP) na Chama cha Demokrasia (DP).

Hivi karibuni, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) pamoja na Chama cha ACT-Wazalendo vilitoka hadharani kila kimoja kwa wakati wake kulalamika ukiukwaji wa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa unaodaiwa kufanywa na wasimamizi au wasimamizi wasaidizi wa serikali za mitaa maeneo mbalimbali nchini.

Mojawapo ya mambo yanayolalamikiwa ni pamoja na wasimamizi au wasimamizi wasaidizi kukataa kutoa fomu kwa wagombea wa vyama vya upinzani, kukataa kupokea fomu zilizojazwa zinaporejeshwa kwa wasimamizi au wasimamizi wasaidizi, baadhi ya ofisi za serikali za mitaa kufungwa na hivyo kukwamisha zoezi la utolewaji wa fomu, wagombea kupewa fomu pungufu kinyume na kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kwa mujibu wa ratiba, uteuzi wa wagombea ambao hufanywa na msimamizi wa uchaguzi katika kata husika unatarajiwa kufanyika kesho kwa nafasi za uenyekiti wa kijiji/mtaa, ujumbe wa halmashauri ya

kijiji/mtaa kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

Uchaguzi huo unatarajiwa kuhusisha watu milioni 19.7 nchi nzima sawa asilimia 86 waliojitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wanaume wakiwa ni

9,529,992 na wanawake wakiwa ni 10,151,267 ikiwa ni ongezeko la watu milioni 8 waliojiandikisha mwaka 2014 ambapo walijiandikisha watu 11,882,086.




Wananchi wakiangalia ajali iliyohusisha gari na pikipiki, katika eneo la Victoria, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. Hakuna aliyejeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi Pemba watakiwa kuvitunza vivutio vya utalii

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MKUU wa Mkoa Kusini Pemba, Hemed Suleiman Abdallah, amewataka wananchi wanaoishi karibu na vivutio vya utalii kutunza maeneo hayo ili wageni waingie kwa wingi, jambo ambalo litasaidia kukua kwa uchumi.

Alisema Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika sekta ya utalii kutokana na mazingira yake yalivyo kuliko nchi nyingine duniani ambazo zinajishughulisha na sekta hiyo.

Aliyasema hayo Furaha Wilaya ya Chakechake Pemba alipokuwa akizungumza na viongozi pamoja na wananchi walipotembelea mto unaoanzia vitongoji hadi Furaha ikiwa ni moja ya kivutio kinachokuza utalii.

Hemed aliwahakikishia wananchi hao kuwa Zanzibar bado ina fursa kubwa sana katika sekta ya utalii na kuwasaidia sana katika maeneo yao. "Niwaombee wanaouzunguka mto huu pamoja na wananchi kwa ujumla kuendelea kutunza mazingira katika maeneo yote, maana hilo litatusaidia kutangaza utalii wetu," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi wa maeneo hayo kutoa ushirikiano kwa viongozi wao, na kuwa eneo hilo likifanikiwa kiutalii, faida kubwa itapatikana kwao na wala hakuna faida ya kugombana.

"Wananchi wa Furaha na Vitongoji mwendelee kudumisha amani, ushirikiano pamoja na kulinda hifadhi zetu, ili tuweze kufanikiwa," alieleza Hemed.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Hadid Rashid Hadid, aliahidi kushirikiana na wananchi wa Furaha na Vitongoji katika kuhakikisha mto huo wanautuzwa na kinakuwa kivutio kikubwa kwa watalii katika mkoa huo.

"Katika ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, tulimsomea taarifa zetu katika suala zima la vivutio vya utalii hasa katika mto huu wa asili katika suala zima la kuendeleza utalii wa ndani, alifahamisha mkuu huyo.

Mapema Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khatib Juma Mjaja, alieleza kuwa jambo hilo ni msisitizo kutoka kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, kutaka kuona sekta ya utalii inapiga hatua.

"Hili ni moja wapo ya mikakati ambayo wizara ya habari, utalii na mambo ya kale imejipangia kufanya kwa mwaka 2019/2020, kwani yapo mengi ambayo tunaweza kuyafanya," alieleza Mjaja.

Hata hivyo, Mjaja alisema Wizara ya Habari iko tayari kupokea ushauri au muongozo kwa ajili ya kuibua na kuendeleza utalii katika maeneo yote ya kisiwa cha Pemba. Kwa upande wao wananchi wa maeneo hayo walieleza kuwa watahakikisha wanalinda vivutio vyote vya utalii katika maeneo yao, ili kukuza kipato chao katika familia.

Kisiwa cha Pemba kina vivutio vingi vya utalii, ingawa vinahitaji kutangazwa ili wageni wavutiwe kufika na kuviangalia.

# Wafanyakazi Naura wamwangukia JPM

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

ZAIDI ya wafanyakazi 100 wakiwamo 22 waliofukuzwa kazi hivi karibuni bila kulipwa stahiki zao na uongozi wa hoteli ya Naura Spring ya jijini hapa wamemwomba Rais John Magufuli kusikia kilio chao.

Ombi hilo linatokana na kukosa msaada kwa uongozi wa mkoa baada ya mkurugenzi wa hotel hiyo, Randy Mrema, kudaiwa kuwaweka mfukoni.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki, baadhi ya wafanyakazi hao waliodai kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 10, walisema uongozi wa hoteli uliwaandikia barua ya ukomo wa ajira ifikapo Oktoba 31, mwaka huu, kwa kile kilichodaiwa ni kampuni kushindwa kujiendesha.

"Kutokana na hatua hiyo walipaswa kuandaa malipo yetu ikiwamo mishahara ya miezi minne tunayoidai, makato ya mfuko wa jamii na malipo ya kusitisha ajira kuliko walivyofanya kwa sasa na kusababisha familia zetu kuteseka kwa njaa," walisema.

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao, baadhi ya wafanyakazi waliofukuzwa kazi, Grayson Mwanga na Kisuno Bernard, walidai kwamba uongozi wa hoteli umeshindwa kuwalipa stahiki zao na wamekuwa wakiwadharau wafanyakazi pindi wanapoulizia malipo ya mishahara yao.

"Hapa tulipo hatujalipwa mishahara ya miezi minne. Makato ya NSSF ambayo wamekuwa wakikatwa kila mwezi lakini mwajiri wao hapeleki kwenye mfuko huo jambo ambalo tunaomba Rais Magufuli aingilie kati," alisema Mwanga.

Alisema mbaya kabisa wanakosa msaada Idara ya Kazi kutokana na Mkurugenzi kudaiwa kuwa na uhusiano na kiongozi wa idara hiyo, jambo ambalo wamekosa mtu wa kusikiliza kilio chao.

Kutokana na hali hiyo, alisema wamemwomba Rais Magufuli, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na taasisi zingine zenye dhamana ya kazi, kuingilia kati na kuchunguza jambo hilo.

"Awali Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqaro, alitusaidia sana na kuwezesha kulipwa kwa mishahara ya nyuma lakini kwa sasa tunakosa hata mtu mmoja wa kutusaidia," alisema Mwanga

Ofisa Kazi Mkoa wa Arusha, Wilfred Mdumi, anayedaiwa kuwekwa mfukoni na mkurugenzi wa Naura ambaye pia anamiliki hoteli ya Impala, amekanusha kurubuniwa kwa kitita cha fedha ili apindishe haki ya walalamikaji.

Hata hivyo, Mduma alisema suala hilo analishughulikia kwa umakini mkubwa kwa mujibu wa sheria za kazi.

"Tumefanya mazungumzo na uongozi wa hoteli hiyo na kutoa maelekezo lakini kumekuwapo na suala la utovu wa nidhamu kwa wamiliki kukiuka makubaliano ya wazi," alisema Mdumi.

"Ofisi yangu imewashauri wafanyakazi hao pamoja na wale walioachishwa kazi kufungua kesi mahakamani kulalamikia kuachishwa kazi bila kupewa stahiki zao ikiwemo kukatwa makato ya NSSF bila kupelekwa katika mfuko huo," alisema.

Mrema alipofuatwa kupata ufafanuzi wa jambo hilo, hakutoa ushirikiano badala yake alitimua mbio na kuingia kwenye gari na kutokomea kusikojulikana na kuwaacha waandishi waliokuwa wamejazana katika hoteli ya Impala wakishangaa.



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wakipanga bidhaa zao chini, katika eneo la Mianzini, jijini Arusha jana, kwa ajili ya kuwauzia wapita njia. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wafanyakazi serikalini wapewa somo

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

WAFANYAKAZI serikalini wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kuwaheshimu wananchi wanaowahudumia ili kuleta ufanisi kwenye miradi ya maendeleo ya taifa.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alisema jana wakati wa semina ya Kaizen iliyofanyika mkoani hapa.

Semina hiyo iliwashirikisha viongozi mbalimbali kutoka ofisi ya mkoa wa Arusha na halmashauri zote saba za mkoa kwa lengo la kuwapa mbinu za ufanisi kazini na kupunguza mianya ya rushwa kwa kuwapa mbinu za kujiongezea kipato.

"Acheni kutegemea mishahara nawataka mje Sido kupata uelewa na mafunzo ya kuwa mjasiriamali mzuri," alisema Nchimbi.

Aliongeza kuwa Kaizen ni neno la Kijapani lenye maana ya maboresho endelevu, hivyo lazima wafanyakazi waendane na falsafa hiyo kutimiza vyema wajibu wao na kwa ufanisi zaidi.

Akizungumza na wafanyakazi hao, Nchimbi alisema Sido wanatoa mafunzo ya aina mbalimbali ya kumsaidia mjasiriamali kupata masoko ya bidhaa zake hali ambayo itasaidia kuboresha Tanzania ya viwanda, kuongeza ajira na kusaidia familia zao.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Sifaeli Kulanga, alisema mafunzo hayo ni mazuri na watayafanyia kazi kwa vitendo, ili yawe na matokeo chanya kwa wafanyakazi wa serikali.

"Tumekuja kupata mafunzo ya mabadiliko ambayo tutaenda kuyafanyia kazi kwa vitendo na tutaenda kuwaelimisha na wengine," alisema Kulanga.

Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza tija, ubora na ufanisi katika ofisi na taasisi zote za serikali ili kupunguza mianya ya rushwa, ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za umma.

# Diwani awataka wazazi kuwapa motisha watoto

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

DIWANI wa Ambureni wilayani Arumeru, Japhet Jackson. ameitaka jamii kujijengea desturi ya kutoa motisha kwa watoto wao wanapofanya vizuri katika masomo yao, ili kuongeza ari ya kupenda kusoma kwa bidii zaidi na kufaulu.

Alisema kuwa jamii nyingi huwa hawana desturi ya kufanya hivyo hali ambayo inachangia watoto wengi kutokuwa na kasi ya kupenda masomo na hata wengine kukataa shule kutokana na kuona masomo magumu.

Jackson aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na suala la motisha kwa wanafunzi wanapofanya vizuri katika masomo yao.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapatia watoto zawadi yoyote mara kwa mara pindi wanapofanya vizuri katika masomo yao ili kuwasaidia kuongeza kasi kupenda kusoma kwa bidii na kufikia malengo yao.

"Wazazi wengi hawaelewi tu namna ya kumsaidia mtoto kuongeza kiwango cha ufaulu ,kwa kumpa motisha ya chochote ili kuona anaweza na kuzidi kuongeza bidii zaidi na mwisho wa siku kukuta anafaulu vizuri tofauti na awali na hii ndiyo siri pekee. Nawashauri wazazi wenzangu muitumie mtaona faida yake,"alisema Jackson.

alitumia fursa hiyo kuwataka wanafunzi hao kuendelea na bidii ya masomo kama ambavyo walikuwa wakifanya shuleni hapo pindi wawapo sekondari huku wakiwa mabalozi wazuri wa kuitangaza shule hiyo.

Pia aliwasihi wazazi mbali na kuwapa zawadi watoto wao, vema wakajenga tabia pia ya kufuatilia mwenendo wa masomo yao shuleni ili kufahamu masomo anayopata shida mtoto.

**"Wazazi wengi hawaelewi tu namna ya kumsaidia mtoto kuongeza kiwango cha ufaulu ,kwa kumpa motisha ya chochote ili kuona anaweza na kuzidi kuongeza bidii zaidi na mwisho wa siku kukuta anafaulu vizuri tofauti na awali na hii ndiyo siri pekee. Nawashauri wazazi wenzangu muitumie mtaona faida yake,"alisema Jackson.**

# Hatimaye shule yapatiwa usajili

**Na Godfrey Mushi, HAI**

HATIMAYE Halmashauri ya Wilaya ya Hai, imetekeleza amri ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, ya kataka kuondolewa kwa urasimu katika usajili wa Shule ya Msingi Mtakuja.

Kwa miaka 12 iliyopita, shule hiyo ilikuwa ikipambana kutafuta usajili bila mafanikio, huku Ofisi ya Elimu ya Halmashauri hiyo ikiwa haina majibu sahihi ya sababu za kushindwa kusajiliwa.

Mkuu wa Habari na Mawasiliano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Riziki Lesuya, alisema jana kuwa tayari agizo hilo limetekelezwa na kwa sasa ofisi ya idara ya elimu inakamilisha taratibu za mwisho ili kuruhusu wanafunzi kuanza masomo mwaka ujao.

Mwezi uliopita, Ole Sabaya alitaka shule hiyo isajiliwe mapema ili kuwapunguzia adha wanafunzi wake kutembea umbali mrefu kufuata masomo.

Alitoa amri hiyo baada ya kwenda katika Kijiji cha Mtakuja, baada ya wananchi wake kumweleza kuwa pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo miaka 12 iliyopita, bado shule hiyo haisajiliwa.

Wananchi hao walimweleza Mkuu huyo wa Wilaya walisema kuwa watoto wao wanatembea umbali wa kilometa 32 kwenda Shule ya Sekondari ya Kia kila siku na kurudi nyumbani.

Mmoja wa wananchi hao, Saufa Shaban, alisema shule hiyo ilijengwa miaka 12 iliyopita imekamilika miundo mbinu yote, lakini tatizo ni usajili umekwama.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), kutokana na umbali huo watoto wetu hawapati elimu yenye manufaa kabisa, wanaishia kupata ujauzito wengine wanaacha shule kabisa na wale wanafanikiwa kumaliza shule hawana ufaulu mzuri, hivyo kusababisha kijiji chetu kuendelea kuwa maskini," alisema Saufa.

Baada ya kauli hiyo, Mkuu huyo wa Wilaya alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, kuhakikisha shule hiyo inapata usajili ndani ya siku 90 ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea umbali huo.

Akijibu hoja iliyoelekezwa na Mkuu huyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Elia Machange, alisema shule hiyo imechelewa kusajiliwa kutoka na kuwepo na mapungufu machache ikiwamo kukosa maabara za sayansi.

"Nikuhakikishie Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwamba mwaka huu, Sekondari ya Mtakuja itasajiliwa na wanafunzi watakaohitimu darasa la saba mwaka 2019 watapangiwa shule hiyo," alieleza Machange.

# Vyandarua uvuvi haramu vyateketezwa

**Na Godfrey Mushi, MWANGA**

MATUMIZI mabaya ya vyandarua vya kujikinga na malaria ambavyo vinatumiwa na baadhi ya wavuvi kuvua mazalia ya samaki wachanga katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, vimeharibiwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson.

Vyandarua hivyo ambavyo hugeuzwa kama nyavu za kuvulia samaki, vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 39.3.

Mkuu wa Wilaya hiyo, alithibitisha jana kwamba pamoja na vyandarua hivyo kukamatwa na kuteketezwa, pia serikali imeharibu makokoro ambayo yalikuwa yakitumiwa kwa siri.

"Hivyo vyandarua wa kujikinga na malaria pamoja na makokoro ni kweli tumevikamata katika operesheni Sangara na Jodari inayoendelea katika vijiji vinavyolizunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu," alisema Apson.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, katika operesheni hiyo wavuvi haramu 14 wamekamatwa kutokana na tuhuma za kujihusisha na matumizi ya vyandarua hivyo.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa katika operesheni hiyo, wavuvi hao baada ya kutiwa mbaroni wanadaiwa kuwatishia Polisi wenye silaha waliokuwa doria na wakiwataka waweke silaha chini ili wazichape ngumi kavu kavu.

Akizungumzia operesheni hiyo, Ofisa Tarafa ya Lembeni, Gikila Salisali alisema baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu wamekuwa kikwazo katika vita hivyo, kwa kuwa wanashirikiana na wavuvi haramu kuihujumu serikali.

Kutokana na hali hiyo, Salisali ameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuiongezea nguvu operesheni hiyo kwa kizipatia za kisasa kwa ajili ya kuimarisha doria ndani ya bwawa hilo.

Aidha, wananchi wanaolizunguka bwawa hilo, wakiwamo Eda Eliakimu na Bakari Kingazi, walieleza imani yao kwa serikali kwa kutangaza upya vita hiyo.

Katika maoni yake, Kingazi alisema operesheni hiyo inaweza kusaidia kupunguza kasi ya uvuvi huo ambao umekuwa tishio kwa samaki wachanga.



Wanawake wachuuzi wa ndizi, wakisubiri wateja katika Soko la Mamsera, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro juzi. Idadi kubwa ya wanawake wilayani humo ndio hujishughulisha na biashara hiyo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# CCM yatamba kushinda kwa asilimia 80

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAKATI vyama vya upinzani nchini vikilalamikia rafu zinazoendelea kila kona katika mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, kimetamba kushinda kwa asilimia 80.

Siku mbili zilizopita Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania na Mwenyekiti wa Taifa wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alilia kuhusu rafu za uchaguzi akidai kwamba katika Jimbo la Vunjo, vituo vyote vilikuwa vimefungwa kwa siku nzima Novemba Mosi, mwaka huu, huku wagombea wake wakinyimwa fomu.

Jana, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, akizungumzia mchakato huo wa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, alisema hawana shaka na ushindi mnono katika majimbo ya wapinzani mkoani hapa.

Majimbo yanayoshikiliwa na wapinzani Kilimanjaro ni Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Same Mashariki, Vunjo, Rombo na Hai.

"Wagombea wetu wote safari hii ni wale wanaouzika majukwaani, walioteuliwa wana sifa nzuri na hao ndio kisu cha wapinzani," alisema Boisafi.

Alisema CCM itawaunga mkono wagombea wake wote na kwamba wanatambua inakwenda vitani kupambana na vyama vya upinzani katika uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ni kipimo cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 utakaowahusisha rais, wabunge na madiwani.

Alisema CCM wakiongozwa na Rais John Magufuli watawaeleza wananchi mambo yote yaliyofanywa kuanzia mwaka 2016 hadi 2020, hasa katika sekta za afya, elimu, afya, maji na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Boisafi alisema mambo mengine ni juu ya kufufuliwa kwa usafiri wa anga ambao hadi sasa serikali imekwisha nunua ndege kadhaa, ujenzi wa reli ya kisasa inayotumia umeme, ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Rufiji na kwamba jitihada hizo zimetokana na Rais Magufuli.

Alitaja sababu zingine za CCM kushinda uchaguzi huo kuwa ni pamoja na wananchi kuridhishwa na utendaji kazi wa Rais Magufuli na kwamba wanaomba wananchi waichague tena CCM ili waendelee kupata maendeleo.

Mwenyekiti huyo alisema jitihada hizo pia zimechangiwa na Rais kuwaelimisha wananchi kulipa kodi na kukemea rushwa waziwazi na kuwachukulia hatua wezi na mafisadi wa mali za umma.

Boisafi alisema jitihada hizo zimekwenda pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya kuwa wazalendo kwa taifa lao na kuwahamasisha kupenda vitu ama bidhaa na kutambua haki na wajibu wao.

Alisema CCM imeonyesha inauwezo wa kuongoza na kuwapeleka wananchi katika uchumi wa kati na CCM imeshika hatamu hakuna kiongozi anayelala na badala yake sasa wanachapa kazi.



Ukurasa 14

Kasafisha kila mahali alikonuia, kisha anatimiza kwa rekodi TRA

Profesa Mpanduji: Sido Tumerejesha ubatizo 1973 'Mzazi wa Wazalishaji'



Ukurasa 16



Ukurasa 18

Ameweka msingi wa kufaidi Tanzania ijayo yenye neema

Nipashe JUMANNE NOVEMBA 5, 2019



Distributed via ippmedia

# MIAKA MINNE YA RAIS JPM KUELEKEA UCHUMI WA KATI

Mnec CCM anayejinasibu kumuona JPM kila kona ya ufanisi Mwanza Ukurasa 15

MIAKA MINNE SAFARI YA JPM

# Kasafisha kila mahali alikonuia, kisha anatimiza kwa rekodi TRA

• Ahadi ya bungeni imegeuka ushuhuda


Distributed via ippmedia

Rais John Magufuli, alipohutubia Bunge. Kushoto kwake ni Spika Job Ndugai. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jovina Bujulu,** MAELEZO

ALIPOZINDUA Bunge la Jamhuri wa Muungano, jijini Dodoma, Novemba 2015, Rais Dk. John Magufuli, aliwakumbusha wabunge kwamba, wananchi waliwachagua kwa matarajio makubwa na watawapima kwa namna watakavyokidhi kiu yao. Ni tarehe inayotimu mwaka mmoja kuanzia sasa.

"Wananchi wamewapa imani na ridhaa ya kuwawakilisha katika kipindi cha Awamu ya Tano, matarajio yao ni makubwa sana.

"Sote tuliahidi kuwatumikia na kutokana na utumishi wetu kwao, tuweze kutatua matatizo yao mbalimbali na kuongoza mabadiliko makubwa ya kiutendaji" alisema Rais Dk. Magufuli.

"Mimi na Mhesmiwa Samia (Suluhu Hassan), Makamu wa Rais, tuliwaahidi wananchi tutawatumikia na kuhakikisha kuwa katika utumishi wetu, tutawajali wananchi wote, lakini zaidi wananchi wa kawaida" alieleza.

Ni dhahiri kuna ushuhuda wa maneno hayo, katika ngazi mbalimbali za utendaji nchini, kuanzia juu katika Baraza la Mawaziri, hadi watendaji kata.

Hivyo, mkutano kati ya Rais na watendaji kata, ulikuwa mwendelezo wa mikutano na watendaji wa serikali, wakiwamo wakuu wa mikoa, makatibu tawala mikoa na wilaya, wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali na makatibu watendaji wa tarafa.

"Ninyi ni wawakilishi wangu ngazi ya kata. Tunapozungumzia mafanikio ya serikali, ninyi ndio wasimamizi wa mwanzo wa mafanikio hayo," aliwaambia.

> Serikali iliridhia kumega misitu 14 kwa ajili ya kilimo na mifugo na kufuta mashamba 16 yasiyoendelezwa, ili yapangiwe matumizi ya kilimo na mifugo.

Hatua ya kuweka kikao na watendaji ngazi ya chini ni ishara anavyowajali mahali waliko kwenye shina ya tija ya umma.

Alipokuwa bungeni, aliahidi kusimamia matumizi ya mali za umma na rasilimali za Taifa, ili inufaishe umma na kamwe si mtu binafsi, ikienda na kuhakikisha rasilimali hizo kwa haki.

**ALIPOANZIA MADINI**

Rais Dk. Magufuli, alianza kazi kwa kufuatilia rasilimali alipounda kamati maalum ya kuchunguza mchanga na madini yaliyosafirishwa nje ya nchi. Kamati ilibaini upotevu mkubwa wa mapato na rasilimali za nchi inayokadiriwa kati ya Sh. bilioni 829.4 hadi Sh. trilioni 1.439, kwa kusafirisha mchanga nje ya nchi, kila mwaka.

Kamati ilitoa mapendekezo kadhaa, ambayo Rais Dk. Magufuli, aliyakubali: Usitishwaji kusafirisha mchanga hadi mrabaha stahiki utakapolipwa na kujengwa vinu vya kuchakata madini nchini, ili usahihi ujulikane na kutozwa kodi.

Aidha, Rais aliwaagiza wakuu wa mikoa inayozalisha madini kuanzisha masoko yanayodhibiti utoroshaji na uuzaji holela wa madini hayo.

Hadi sasa baadhi ya masoko yamekwishaanzishwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Mtwara, Manyara, Morogoro, Kagera na Arusha. Pia, zipo katika Wilaya za Simanjiro na Chunya.

Ufunguzi wake unaelezwa kuleta neema si kwa serikali tu, bali hata wauzaji madini hayo kwa wanunuzi wakubwa, ambao awali waliambulia bei ya kudhulumiwa. Ni udibiti unaoiongeza mno pato la taifa kupitia madini.

**UKUSANYAJI MAPATO**

Eneo lingine aliloahidi ni kusimamia ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za umma. Tayari kuna ushuhuda wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuzindua Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhi Mifumo ya Ukusanyaji wa mapato kwa Njia ya Elektroniki, ambayo ni mlinzi wa fedha za umma.

Ni makusanyo ambayo Septemba mwaka huu yalikuwa Sh. trilioni 1.7 sawa na asilimia 97.20 ya makadirio, kiasi ambacho hakijawahi kukusanywa na TRA tangu ilipoanzishwa, Julai Mosi, 1996.

Dhamira ya TRA kukusanya mapato kwa utaratibu rahisi na wazi ili walipa kodi wapate urahisi wa huduma kwa wakati, hali inayofungua mlango wa taasisi kukubalika.

Msingi wa kituo hicho, upo katika ushirikiano kati ya TRA na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), kikiundwa kusaidia kuondoa mianya ya uvujaji mapato ya serikali mbili; Muungano na Mapinduzi (SMZ).

Akizindua kituo hicho, Rais Dk. Magufuli, alizitaka taasisi mbalimbali zikiwamo za serikali, kampuni na benki kujisajili katika kituo hicho, zikusanye kodi kwa ufanisi.

Rais alisema:"Kituo hicho ni muhimu sana kwa ustawi wa maendeleo ya nchi, ili kulinda usalama wa taifa, taasisi za serikali na kampuni binafsi zinazoendesha shughuli zake nchini na kukuza sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo ni kichocheo kikubwa cha maendeleo."

**VITA RUSHWA**

Kuhusu utawala bora, Dk. Magufuli vita dhidi ya rushwa na ufisadi, akiwaambia wabunge pindi alipowahutubia kwamba, mojawapo ya maeneo yaliyolalamikiwa na wananchi wakati wa kampeni ni rushwa, kwa maana ni kero kubwa kwao.

Katika vita hiyo anasema kumeimarishwa ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) hadi ngazi za wilaya na serikali inajipambanua kwa uwazi na uwajibikaji kwa umma, kupitia elimu inayohusu rushwa na madhara yake.

Katika mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika (AU) uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia mwaka juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema Tanzania ilitajwa kuwa nchi inayofanya vizuri katika ufuatiliaji na utekelezaji mapambano dhidi ya rushwa.

Taasisi ya Transparency International imesifu juhudi za Rais Dk. Magufuli, ikiitaja Tanzania ni ya pili kwa kupunguza rushwa na kufanikiwa kuifanyia kazi mianya mingi ya rushwa.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Kamishna Diwani Athuman, anasema utafiti uliofanywa na taasisi za kimataifa inayoitwa Global Corruption Barometer Africa 2019, iliyofanuliwa na asasi za Transparency International na Afro Barometer, anasema Tanzania ni ya kwanza kati ya nchi 35 za Afrika, katika kipengele cha juhudi za serikali kupambana na rushwa mwaka 2019.

Diwani alitaja maeneo ya ufanisi ni: Utendaji mzuri wa serikali; na kukuza imani kwa wananchi.

**ARDHI JE?**

Hivi karibuni, Serikali ya Awamu ya Tano imefuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,659.94, yalipoteza sifa na kuyagawa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za makazi, kilimo na ufugaji, na misitu 7 yenye ukubwa wa ekari 46,715 kurudi kwa wananchi.

Ni hatua itokanayo na kuwapo vijiji 975 vyenye migogoro, kati yake 920 vilitakiwa kubaki viliko, mipaka yao ikirejewa upya kupatiwa vibali vya ardhi vya kijiji.

Serikali iliridhia kumega misitu 14 kwa ajili ya kilimo na kufuta mashamba 16 yasiyoendelezwa, ili yapangiwe matumizi ya kilimo na mifugo.

Pia, kunatajwa mafanikio katika sekta za afya na elimu, ambayo sasa ni bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne, hali iliyoamsha ari kwenda shule.

Sekta ya elimu imeshuhudiwa maboresho ya vifaa vya kufundisha na kujifunza vikiongezwa, michango isiyo ya lazima imeondolewa, kuongezwa samani na majengo, ikiwamo nyumba za walimu.

Sekta ya Afya, dhamira ya Rais Dk. Magufuli kujenga uchumi wa kisasa na suala la kupambana na umaskini, amelipa msukumo wenye tija, ili kuwa na wananchi wenye afya bora.

Hospitali, vituo vya afya na zahanati zinapata mahitaji muhimu, kwa lengo la kuwaondolea wananchi usumbufu usio wa lazima katika afya.

JAMAL ABDUL

# Mnec CCM anayejinasibu kumwona JPM kila kona ya ufanisi Mwanza

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

LEO ni miaka minne kamili tangu kukaribishwa rasmi ofisini kutokana na ushindi aliyoupata kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2005, baada ya kuzunguka na kaulimbiu yake 'hapa kazi tu.' Kwa waliokuwa na hamu ya kujua hiyo 'hapa kazi tu' ikoje, walipata majibu ndani ya muda mfupi tu.

Huyo ni Rais Dk. John Magufuli, aliyechelea kuchagua safu ya wakuu hasa wa wizara baada ya kuingia ofisini, kwa matarajio ya kutekeleza nao 'hapa kazi tu' kwa kasi aliyoitaka, ili kuisogeza nchi katika maono yake ya Tanzania ya Viwanda; Watanzania waifike kwa udi na uvumba. .

Ni ndani ya siku chache akiwa ofisini ya Ikulu, alitumia staili ya aina yake, alipofanya ziara ya kushitukiza katika ofisi kuu za wizara kupata uhalisia wa kazi zinavyoendana na akaondoka na picha fulani ya ushuhuda.

Si haba, hata ndani ya chama kinachopeperusha bendera yake kuusaka uongozi, Chama Cha Mapinduzi (CCM), anafahamika vyema kwa hilo, akiwa katika cheo cha uenyekiti. Anakalia kiti hicho ikiwa ni utaratibu wa ndani aliojipangia, mkuu wa nchi anavishwa pia kofia kuu katika chama.

Ilikuwa salamu tosha hata uteuzi wa wasaidizi wake ulipochukua nafasi, kila mteule alibeba tahadhari ya 'hapa kazi tu' na wapo waliofkiwa na salamu za 'kutumbuliwa' kwa kisa cha kutoridhisha kiutendaji.

#### M-NEC AFUNGUKA

Kwa mantiki hiyo, wenye chama chao wanaielezaje miaka hiyo minne ya 'hapa kazi tu' inayotimizwa kufikia leo? Kama waswahili wanavyonena 'mwenye kabila lake ndiye fundi wa kuicheza ngoma' Nipashe ilimtafuta mwana - CCM, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (Nec) ya CCM Mkoa wa Mwanza, Jamal Abdul, aanike simulizi ya ushuhuda wake.

Anaanza kwa kujigamba mkoani kwake Mwanza, ndani ya miaka hiyo minne, ahadi za kampeni ya uchaguzi mkuu uliopita ziko dhahiri zikitekelezwa na wananchi wanashuhudia kilichopo.

Mnec - Abdul anazieleza kupitia ilani yao ya uchaguzi, kwamba walichoahidi kuwatumikia Watanzania katika miaka mitano ya sasa zinatekelezeka; vijijini hadi mjini, akitaja baadhi zinahusu kuimarisha ujenzi wa huduma za afya, elimu, barabara, usafiri wa majini na anga.

Abdul anasema CCM ilibaini baadhi ya mali zake zilizoporwa na wajanja, hatua zilichukuliwa kuzidishwa kwenye himaya zake, kwa kuweka mfumo maalum kutunza kumbukumbu za mali hizo.

#### MAKUU ELIMU

Anataja miradi ya elimu Mwanza, kwamba Dk. Magufuli, ameiboresha mjini hadi vijijini, kwa kujengwa madarasa shule za msingi na sekondari ngazi ya kata, huku ikitolewa bure kuanzia elimu ya msingi, hadi sekondari kidato cha nne.



Rais John Magufuli, aliposalimiana na wakazi wa Mwanza. **PICHA: MTANDAO**

Distributed via ippmedia

> Nampongeza Rais Magufuli kusimamia serikali na kutekeleza ilani ya chama, katika miaka minne aliyotimiza hadi sasa, makubwa aliyoyafanya ya kiufanisi hayana mfano kwa Watanzania.

Jana ndio mara ya kwanza waliojiunga na sekondari kwa mfumo wa bure, walianza mtihani wa kuhitimu kidato cha nne.

Abdul mafanikio hadi sasa, ni kuongezeka alama chanya darasani, pia wanaojiunga shule za msingi kuogezeka maradufu, katika baadhi ya sehemu inavuka asilimia.

"Bajeti ya elimu katika wizara hiyo ilikuwa Sh. bilioni 18 tu, lakini Rais Magufuli aliongeza hadi kufikia bilioni 23," anasema Abdul.

"Nampongeza Rais Magufuli kusimamia serikali na kutekeleza ilani ya chama, katika miaka minne aliyotimiza hadi sasa, makubwa aliyoyafanya ya kiufanisi hayana mfano kwa Watanzania. Mengi yaliyofanyika ni ya kihistoria hata wananchi wanashuhudia," anasema.

#### UJENZI& MAWASILIANO

M-Nec huyo anataja wanyojivunia katika sekta za Ujenzi na Mawasiliano kitaifa, ni reli ya kisasa na ununuzi wa ndege kuliimarisha Shirika la Ndege la Taifa (ATCL), ambayo siku chache zilizopita, ilipokea ndege mpya aina ya Boeing.

Anafafanua: "Ujenzi wa meli mpya kubwa kuliko ya zamani MV Victoria, ambayo hufanya safari zake kati ya Mwanza na Bukoba."

Miundombinu iliyojengwa kupitia mageuzi ya Dk. Magufuli, Mwanza ukarabati wa chelezo na kujenga daraja kubwa la Busisi -Kigogo, wilayani Misungwi na kujengwa meli mpya.

Kwa mujibu wa Abdul, kuna ujenzi wa kiwango cha lami barabara kutoka Sabasaba, Nyasaka - Buswelu, hadi Nyakato na upanuzi wa barabara kilomita tisa kutoka Uwanja wa Ndege Ilemela, inayotokana na fedha za bajeti sherehe za Muungano, ikifanana na bajeti iliyoboresha barabara Dar es Salaam, kati ya Morocco na Mwenge.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (Nec) CCM, Mkoa wa Mwanza, Jamal Abdul Babu. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

#### AFYA BORA

Maboresho sekta ya afya iko chini ya Mpango wa Maendeleo ya Afya (MAAM), iliyoanza mwaka 2008 na Abdul anasema kwao CCM- Mwanza, imeifanikishwa kwa kujengwa zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila kata.

Mwongozo MMAM unaelekeza kijiji au kitongoji kuwa na zahanati na kata ipewe kituo cha afya; wilaya iwe na hospitali; wakati mkoa na kanda ni hospitali za rufani; zote zikibebwa na Hospitali Kuu ya Taifa Muhimbili.

Anasema,hivi sasa wizi wa dawa serikalini zilizouzwa kiholela kwenye maduka binafsi, hata kuwaacha wananchi wagonjwa kwenye lindi la ukosefu wa dawa umedhibitiwa.

Pia, serikali imepunguza gharama za ununuzi wa dawa, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) sasa inaagiza dawa moja kutoka kwa mtegenezaji na zinakuwa na nembo ya serikali.

Kiongozi huyo wa CCM Taifa, anataja cha kujivunia, Rais Dk. Magufuli hajawaacha nyuma wazee wenye umri kuanzia miaka 60, sera iliyoasisiwa na watangulizi wake, kuwadumia bure na kutengewa dirisha lao la dawa na daktari.

Abdul anataja Bajeti ya Afya, imepanda zaidi ya mara nane aliyoikuta madarakani, akipigania tija ya afya kwa anaowaongoza.

#### VITA UFISADI

Mwana- CCM huyo anamwagia sifa mwenyekiti wake wa taifa, alipoahidi kupambana na alichokiita 'kansa ya rushwa' kwa kuwakamata mafisadi, kisha kuanzisha Mahakama ya Mafisadi.

Anasema, Rais Dk. Magufuli, ametimza kwa kuwakamata na kuwachukulia hatua wanaotuhumiwa, huku baadhi walioko katika mikono ya sheria, wanajisalimisha kurudisha fedha za walipa kodi nchini, kupitia msamaha maalum wa kiserikali.

Anataja mengine, ni kupambana katika vita ya kihistoria ya dawa za kulevya; kuondoa wimbi la watumishi hewa waliolipwa mishahara kutoka bajeti ya walipa kodi; pia kuwapo kundi kubwa la wenye vyeti feki katika utumishi wa umma.

#### VILIVYOMKUNA M-NEC

Abdul anaeleza kwamba 'haijawahi kutokea' kuwasamehe kodi wajasiriamali wadogo walipe Sh.20,000 tu kwa mwaka, kwamba ni jambo la kujivunia.

Pia, anazungumzia uenyekiti wake katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), pale alipofanikisha kuiingiza Kiswahili kuwa lugha rasmi ya mawasiliano.

Katika anachokiita 'kufuata nyayo' za Hayati Mwalimu Nyerere, M-nec Abdul, anasema Dk. Magufuli yuko naye kupitia miradi mbalimbali ya kitaifa, ikiwamo mradi wa Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere (Stigglers Gorge), ambalo ukikamilika unatarajiwa kuzalisha megawati zaidi ya 2000.

# Profesa Mpanduji: Sido Tumerejesha ubatizo 1973 'Mzazi wa Wazalishaji'

## • Wajasiriamali juu, bidhaa bora, majirani EAC wanatugongea hodi

**Na Beatrice Philemon**



Bidhaa zitokanazo na Sido zikiwa katika soko la maonyesho. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

KUZALIWA Shirika Ia Kuhudumia Viwanda Vidogo Nchini (SIDO) ni zao agizo la iliyokuwa chama tawala TANU, mnamo Machi, 1973. Ilitakiwa kusimamia uendelezaji viwanda vidogo, kutoa huduma shirikishi kijinsia katika sekta za vijijini na mijini. Ilikuwa katika zama, Tanzania inatekekeza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa.

Huduma hizo zinalenga uanzishwaji na ukuaji viwanda vidogo vinavyozingatia kuongeza thamani ya rasilimali nchini, kuendeleza na kutumia teknolojia rahisi inayopatikana.

Hadi sasa SIDO inawajibika kutoa kipaumbele kwa miradi ya uzalishaji na huduma kuwezesha utengenezaji bidhaa zinazokidhi mahitaji ya wananchi na ziada kuuzwa nje, ikifanyika kupitia kushawishi, kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji na uendelezaji viwanda vidogo nchini.

### KUNAKOZALIWA VIWANDA

Mkurugenzi Mkuu, Prof. Sylvester Mpanduji, anasema katika miaka minne sasa, SIDO imeshaanda majengo 12 ya viwanda ( Industrial Sheds ) katika mikoa ya Mtwara, Dodoma, Manyara na wilaya Chato.

Ni maeneo vituo vinavyohusika na kuwakuza wajasiriamali wadogo na wakati huohuo kuanzisha viwanda vinavyotumia teknolojia ya kisasa katika mazingira bora.

Prof. Mpanduji anasema, mwaka huu SIDO imepokea Sh. bilioni moja kutoka serikalini za kuandaa majengo manne ya viwanda katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Mtwara, kuwaendeleza wajasiriamali wadogo.

"Fedha hizi zilitolewa na serikali mwaka wa fedha ulioisha wa 2018/2019 na tulizipata mwezi Juni mwaka huu na sasa hivi tupo kwenye hatua za maongezi na kampuni ya SUMA JKT, ili kuanza ujenzi katika mikoa hiyo," anasema, katika matarajio ujenzi utaanza mwezi huu na kukamilika ndani ya miezi mitano.

Anasema mkoani Kigoma kutakuwapo wataalamu wa kutoa mafunzo, teknolojia ya kisasa na ushauri kwa ajili ya kupata nembo za Shirika la Viango la Taifa (TBS), ikilengwa zaidi ufanisi katika uzalishaji michikichi.

Akizungumzia Mtwara, anasema SIDO imefanikiwa kuwa na jengo la viwanda kuwaandaa wajasiriamali wadogo, na wapate fursa ya kuanzisha viwanda vidogo ndani yake.

"Mpaka sasa katika jengo hilo kuna kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua korosho tani mbili kwa siku kimeanzishwa katika jengo hilo na tayari kimeajiri wafanyakazi 220, kati ya wafanyakazi hao asilimia 98 ni kinamama," anasema.

Manyara, anasema kuna viwanda vinne vinayojumuisha cha kutengeneza mvinyo, vifungashio, mikate na pampu za kuendeshwa na nguvu jua.

> Bidhaa za viwanda vidogo nchini zinaboreka kupitia maonyesho mbalimbali, utangazaji na uhamasishaji.

Anataja mkoa Dodoma na wilaya Chato, hivi sasa zipo kwenye hatua za mwisho kuchagua wajasiriamali watakaoingia kwenye majengo hayo na kunatarajiwa kuanzishwa viwanda vinne vya: kuchakata mvinyo, kutengeneza vitafunwa na viungo.

Prof. Mpanduji anasema, SIDO imefungua ofisi nne katika mikoa mipya; Simiyu, Katavi, Geita na wilayani Chato, ambako huduma zote zinatolewa, akitaja baadhi ni mafunzo, mikopo, ushauri wa teknolojia na kuunganisha wajasiriamali sokoni.

Mkurugenzi anasema miaka minne inatimu, wameshawafunza wajasiriamali 86, 458, kati yao wanawake 51,873, walionolewa kuanzisha na kuimarisha miradi, huduma na kuongeza thamani mazao.

"Katika mafunzo hayo walifundishwa uchakataji wa asali, utengenezaji wa 'Peanut Butter,' ubanguaji korosho, utengenezaji chaki, utengenezaji sabuni, viungo na bidhaa zingine," anasema.

Anataja mafanikio, kuna viwanda vidogo 1,758 vimeanzishwa vilivyoanzisha ajira za kudumu 44,024 katika maeneo ya ubanguaji korosho, usindikaji mihogo na ukamuaji mafuta ya mawese.





Baadhi ya wahitimu wa mafunzo maalumu ya ujasiriamali yanayoendeshwa na SIDO.

Pia, anataja uanzishaji viwanda vya teknolojia za usindikaji vyakula, kupunguza matumizi ya miti na mazao yake kama nishati, kufungasha vyakula vilivyosindikwa, na vifaa vya ujenzi kama matofali, chokaa na chaki.

Aidha, kuna ukamuaji mafuta ya kula kutokana na michikichi; kutengeneza sabuni; kutengeneza na kusindika bidhaa ya ngozi kwa njia za asili.

### MIKOPO

Prof.Mpanduji anasema, tangu Rais alipoingia madarakani, SIDO imetoa mikopo kwa wajasiriamali 21,211 yenye thamani Sh. bilioni 28.503, kati yake kinamama 10,806 walipata Sh. bilioni 13.265, sawa na asilimia 51, kupitia Mfuko wa Mitaji kwa Biashara Ndogo (NEDF).

Prof. Mpanduji anasema SIDO imepata Sh. bilioni moja kutoka JICA (Shirika la Maendeleo Kimataifa Japan) na benki CRDB iliyoiongezwa Sh. bilioni mbilii kusaidia mikopo ya wajasiriamali

" Sisi kama SIDO Sh. bilioni moja tuliyoipata kutoka JICA tutaitumia kama dhamana kwa wajasiriamali wadogo ambao wana viwanda vya kuchakata mazao, ili waweze kupata mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 10 hadi milioni 50," anatamka hatua iliyopo sasa, Sh. bilioni 1.72 zimeelekezwa kwa wajasiriamali.

Mkurugenzi Mkuu anasema, sasa SIDO inajadiliana na Shirika la Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuona uwezekano wa kukopesha wajasiriamali wadogo kuanzia Sh. milioni 80 hadi 300 kwa mtu mmoja.

Ushauri wake ni wenye viwanda vidogo vinavyoanza, watembelee ofisi za SIDO kutambue changamoto zaona wahudumiwe, kulingana na mahitaji yao.

### HATUA ZA TEKNOLOJIA

Katika teknolojia, anasema ndani ya miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Magufuli, SIDO imeshabuni vituo vilivyotengeneza mashine 13,856 walizouziwa wateja wa mikoa saba: Lindi, Iringa, Mbeya, Moshi, Arusha, Shinyanga na Kigoma.

Anazitaja kuwa ni za kubangua korosho, usindikaji mafuta mawese, alizeti, utengenezaji matofali, chaki, kucharaza mbao na kuchakata asali, ikiwamo 'peanut butter.'

### MASOKO & SOKO

Prof. Mpanduji anadokeza mafanikio yaliyopatikana kutoka jitihada hizo, ni kuchochea uanzishwaji na uboreshaji viwanda vya kusindika mbegu za mafuta, nafaka, mazao misitu, bidhaa za ngozi na madini.

"Pia serikali imetupatia Sh. bilioni moja, kwa ajili ya kuboresha vituo vyetu vitatu katika mikoa ya Lindi, Kigoma na Shinyanga, ili viwe na mashine za kisasa kabisa kuturahisishia utengenezaji wa mashine," anasema, akitaja kuwa fedha zilotolewa mwezi mwa mwaka huu.

Katika eneo la soko ndani ya miaka minne iliyopita, Prof.Mpanduji anasema, SIDO iliandaa maonyesho ya kitaifa mara mbili katika mikoa ya Singida na Simiyu, ambayo yamekuwa hamasa katika uanzishwaji viwanda.

> Maonyesho ya Singida yamefanikisha mauzo na miada (order) za mashine na bidhaa za wajasiliamali zenye thamani ya Sh. 450,360,000 na jumla ya wajasiriamali 548 kutoka mikoa 22 na nchi ya Burundi walishiriki.

"Maonyesho ya Singida yamefanikisha mauzo na miada (order) za mashine na bidhaa za wajasiliamali zenye thamani ya Sh. 450,360,000 na jumla ya wajasiriamali 548 kutoka mikoa 22 na nchi ya Burundi walishiriki," anasema.

Pia, anataja mkoani Simiyu walishiriki wajasiriamali 433 kutoka mikoa 21, pia nchi jirani; Burundi, Kenya na Uganda.

Anataja msingi wa maonyesho hayo ni kuitambulisha SIDO kiuchumi na kutoa fursa kwa wajasiliamali wa ndani na nje kutangaza bidhaa na huduma zao, pia wenye viwanda kubadilishana uzoefu na teknolojia.

Mengine yanahusu kujifunza mbinu za kuendesha biashara zao, kutangaza soko la biashara na kutambulisha bidhaa za viwanda vidogo na vya kati, pia mashine na mitambo iliyobuniwa na kuzalishwa kutoka SIDO na karakana zake

### MABADILIKO

Prof. Mpanduji anasema bidhaa za viwanda vidogo nchini zinaboreka kupitia maonyesho mbalimbali, utangazaji na uhamasishaji.

Pia anataja mvuto mwingine unaanzia katika ubora sokoni unaoleta ushindani katika soko hususani bidhaa za mafuta ya kula, viungo na nafaka.

## MIAKA MINNE SAFARI YA JPM

# Ameweka msingi wa kufaidi Tanzania ijayo yenye neema



Rais Dk. John Magufuli akizindua ujenzi wa Daraja la Mfugale jijini Dar es Salaam, ambalo ujenzi wale ulianza akiwa Waziri wa Ujenzi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Dk. Felician Kilahama**

NAKUMBUKA siku kama ya leo, mwaka 2015 aliapishwa Dk. John Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika awamu ya tano tangu tupate Uhuru.

Kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika 2015, kati ya mwaka 2010 na 2015, ilifanya kazi mzuri kuelimisha na kuweka bayana bila ya kificho, maovu yaliyolisibu taifa wakati huo. Kelele zao bungeni na kwingineko; Watanzania walifahamu taifa linachokosa.

Kwa kipindi hicho (2010 hadi 2015) shughuli zilinipa fursa nyingi za kutembelea nchi nzima.

Nilifika Kusini, Kanda za Kati, Nyanda za Juu Kusini, Magharibi na Ziwa na wakati za kampeni za uchaguzi (2015), nilikuwa katika mikoa ya Kaskazini na Kaskazini Mashariki.

Nilifanya uchambuzi wa haraka na kuona uchaguzi mkuu 2015, haukuwa laini kisiasa kwa chama tawala kutetea nafasi, huenda kungekuwapo wakati mgumu.

Hiyo ilikuwa mijini, vijijini ambako kuna Watanzania wengi, bado waliipenda CCM kutokana na mchango nzuri wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere.

Sintofahamu kwa upande wa wapinzani ilijitokeza wakati wa kumteua mgombea urais 2015. Katika harakati hizo wakabadilisha 'gia hewani' na wakampata mgombea waliyemtaka.

Uamuzi wa CCM kimkakati kuweka mgombea asiye na makundi nyuma yake; ulizifanya fikra za baadhi ya waliojipanga kupiga kura kwa upinzani kubadili mtazamo wafanye tofauti.

> Kimsingi, Rais amefanya mengi ya miaka minne, kiasi cha kushangaza wengi katika hali ambayo haikuaminika rasilimali fedha kupatikana.

Hivyo, baada ya kura kuhesabiwa mgombea, CCM akawa kidedea na kutangazwa mshindi Novemba 5, 2015 kuwa na Rais wa tano.

**PA KUIVUNIA**

NI miaka minne tangu Rais Dk. Johm Magufuli awe madarakani. Je, Watanzania wanajivunia nini kuwepo kwake madarakani?

Kwanza, ni Rais anayeweza kuivusha nchi kutoka tulipokuwa na kutupeleka kwenye hali ya matumaini ya "maisha bora kwa kila Mtanzania".

Ni kawaida wanasiasa wengi kusema kuliko kufanya kivitendo, tofauti na Rais Dk Magufuli; anayetekeleza ahadi alizozitoa kupitia ilani ya uchaguzi ya chama chake, siyo kwa maneno tu bali vitendo kama kaulimbiu ilivyokuwa wakati wa kampeni 'hapa kazi tu,'

**HAPA KAZI TU**

Baada ya kuapishwa hakuchelewa, aliwaeleza Watanzania azma yake kuliona taifa linastawi kupitia Sera ya Uchumi wa Viwanda, ifikapo mwaka 2025.

Kwanza, kwa nia nzuri aliamua serikali ihamie Dodoma kama ilivyodhamiriwa tangu utawala wa Hayati Mwalimu Nyerere, kupafanya makao makuu ya nchi.

Pia alitangaza kununua ndege za kulifufua Shirika la Ndege Tanzania (Air Tanzania Company Limited - ATCL), ambalo huduma zake kitaifa zilisuasua sana.

Vilevile, akatangaza jitihada kupunguza foleni barabarani, jijini Dar-es-Salaam, kwa kuendeleza mpango wa kujenga barabara za juu eneo la Ubungo na kupanua barabara kutoka Kimara mpaka Kibaha, kuwa njia sita.

Wakati yanatekelezwa, ikashuhudiwa kuanza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), pia kuimarisha Reli zilizopo: ya Kati (DSM mpaka Mwanza na Kigoma; Kaliua kwenda Mpanda na Tanga kwenda Moshi.

Vilevile, upanuzi wa bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, zitoe kipaumbele, usafiri wa majini unaoimarishwa.

Wakati huohuo, Rais akaendelea na mipango ya kuboresha huduma za afya na usambazaji maji mijini na vijijini.

Serikali iliamua kutoa elimu bure hadi kidato cha sita na kufanya ukarabati kwa majengo ya shule za zamani; kuboresha miundombinu kwenye zahanati na vituo vya afya, kujengwa na kuimarishwa miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege, katika sehemu mbalimbali nchini.

Hadi sasa kila makao makuu ya mikoa imeunganishwa na barabara za lami na Rais Dk. Magufuli alitoa wito kuwekezwa ujenzi wa viwanda nchini, ili dhamira ya uchumi wa viwanda itimie na kuondoa umaskini kwe matokeo makubwa.

Ili viwanda vifanye kazi vizuri, akaona umuhimu nchi kuwa na umeme wa kutosha na endelevu. Ndipo mradi wa bwawa kwenye Mto Rufiji "Stiegler's Gorge" la kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji.

Ni suala ambalo Hayati Mwalimu Nyerere, alikukusudia kulitekeleza, lakini haikufanyika kutokana na sababu nyingi za msingi, ikiwamo vita vya Kagera.

**USHUHUDA**

Mwanzoni mwa uongozi wake, wapo waliodhani 'nguvu ya soda' lakini ushuhuda unajidhihirisha baada ya muda mfupi.

Kwanza, serikali kuhamia Dodoma ikawa kweli.

Pili. ndege mpya zikaletwa aina ya Bombardier kumilikiwa na Tanzania, Julai 8, 2018 majira ya saa 11 jioni ikapokelewa Ndege kubwa aina ya Boeing 787-8 kwa shangwe na nderemo. Zote ni kwa pesa ya ndani, huku nyimgine zikisubiriwa.

Hayo yanaendelea, kukiwapo ujenzi wa barabara za juu eneo la Ubungo kuanzia Kimara mpaka Kibaha, vivyo hivyo reli ujenzi reli ya kisasa umeshika kasi.

Haikupita muda mrefu kunashuhudiwa kutiwa saini mkataba wa kujenga bwawa la maji katika Mto Rufiji, lifue umeme wa uhakika wa megawati zaidi ya 2000 na sasa kazi inaendelea kwa kasi.

Kwa usafiri wa anga lengo ni kupata Ndege 11 na Oktoba 26, 2019 majira ya alasiri, mamia ya Watanzania wakiongozwa na Rais Magufuli, walishuhudia Boeing 787-8 nyingine ikiwasili Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Madini nayo mambo yanawaka moto, kumejengwa ukuta kuzunguka eneo lote lenye madini ya Tanzanite yanayoyopatikana nchini pekee, huku kukijengwa sera, sheria, kanuni na masoko ya kuuzia madini, kwenye mikoa na wilaya husika.

Hiyo imefanya mapato kutokana na rasilimali madini kupanda, ikizaa. Hii ni faraja kubwa kwa Watanzania, kwani inaboresha huduma za kijamii.

Hadi sasa kuna juhudi kubwa za kupambana na rushwa, ufisadi, dawa za kulevya na kuimarisha utumishi wa umma kwa kuzingatia maadili na tunu za taifa kwa faida ya wote.

Kwa sasa hakuna kufanya kazi kimazoea ila "hapa kazi tu" inayowafanya watumishi serikalini na sekta binafsi kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

Rais Dk, Magufuli anakazania Watanzania kuishi kwa amani na upendo na wanyonge wasinyanyaswe, bali wahudumiwe ipasavyo kwa kupunguza kero za jamii.

Kimsingi, Rais amefanya mengi ya miaka minne, kiasi cha kushangaza wengi katika hali ambayo haikuaminika rasilimali fedha kupatikana.

Kumbe hakuna lisilowezekana iwapo dhamira ya kweli ipo na utashi mkubwa wa kisiasa ukawepo; hata kama wachache watapinga mambo yatafanyika kwa faida ya wengi.

Hata nchi zilizoendelea zilipitia hali ngumu, lakini wanafurahia matunda ya waliowatangulia. Hivyo nasi tukazane ili kuwarithishe kilicho kizuri watakaotufuata.

Pongezi nyingi kwa Rais Dk. Magufuli kwa kazi zake nzuri ndani ya miaka minne. Ni mwanzo mzuri.

***Mwandishi anapatikana kwa barua pepe: fkilahama@gmail.com; na simu, (+255) 0756007400 na (+255) 0714 250050.***

# RPC Mwaibambe: Kanda maalum imekomesha mapigano ya koo

**• Yaliponukia tena 2017, yaliteketezwa • Bangi, ng'ombe wa wizi hakuna tena • Waingia ubia wa damu na TRA Sirari**

**Na Anthony Gervas**, ALIYEKUWA TARIME



Kamanda wa Polisi, SACP Henry Mwaibambe, akionyesha viroba wakati wa kuteketeza shehena za bangi mwaka huu, Tarime. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

IMEBAKI historia au simulizi pale miaka kadhaa iliyopita katika Wilaya za Tarime na Rorya mkoani Mara yalipoibuka mapigano makali dhidi ya koo za jamii moja.

Wilaya hizo zimepakana na Ziwa Victoria upande wa Kaskazini, pia vipenyo vingi vya kuingia nchini jirani na mwingiliano wa kikabila, walioko Kenya na Tanzania.

Mapigano hayo yaliibuka kuanzia mwaka 2001 hadi 2006 yaliposhamiri, hivyo serikali ililazimika kuanzisha Kanda Maalum ya Mkoa wa Kipolisi Tarime na Rorya, kwa lengo kutatua changamoto hizo.

Mapigano yaliibuka baina ya koo hizo, ambazo ni jamii ya Wakurya; Wanchari dhidi Warenchoka; Wakira walipigana na Wanyabasi; Wasweta na Wahunyaga; Wamera na Wahunyaga; Wamera na Wajaluo; Wanyabasi na Wailege, pamoja na Wanyamongo na Wailege.

Koo zingine ni Wanyamongo walipigana na Watimbaru; Wangurimi na Wairege; Wakira na Wanchar, waliopigana kwa miaka kadhaa.

Vita hivyo vilipamba katika koo hizo vilivyotokana na kuibiana mifugo,hasa ng'ombe, ugomvi wa ardhi na mwingiliano mipaka na mashamba.

### JPM ALIPOINGIA

Rais Dk. John Magufuli, alipoingia madarakani mwaka 2015, mapigano hayo yalikwishakoma, lakini dalili zingine zilijitokeza katika miaka ya 2017 na 2018, lakini Jeshi la Polisi Kanda Maalum, Tarime na Rorya, halikuyapa nafasi, ikayazima.

Walio na historia wanaeleza, mapigano ya koo hizo yalianza zamani tangu zama za Awamu ya Kwanza, kati ya mwaka 1978 na 1980 yaliibuka na kutulia, baada ya vita vya Uganda na Tanzania.

Chanzo chake ni kilekile kinachotajwa kuwa kuibiana mifugo, kuingiliana mipaka ya ardhi na mashamba, wakipigana kwa kutumia silaha za moto na jadi, ikiwamo mishale na mapanga, wengi walipoteza maisha.

Hadi sasa katika Awamu ya Tano hakuna mapigano yaliyoendelea Kamanda wa Polisi Kanda maalum, Mkoa wa Kipolisi Tarime na Rorya, SACP Henry Mwaibambe, anaieleza Nipashe, kwamba kwa sasa hali ni shwari na imebaki historia ya mapigano katika koo, ambazo kwa sasa zinaelezwa kuelewana kwa kiasi kikubwa.

"Dalili zingine za kutaka kuanza mapigano zilianza kujitokeza mwaka 2017, 2018, chanzo chake ni kilekile cha kupigania mipaka ya ardhi, mashamba na wizi wa mifugo kutoka koo hizo.

"Lakini kwa vile serikali tayari ilianzisha Mkoa wa Kipolisi Kanda Maalum Tarime na Rorya, vita hivyo havikuwa na nafasi tena," SACP Mwaibambe, anaieleza Nipashe na kuongeza:

"Tulianza kuwachukulia hatua kali wahusika, ikiwamo kuwafikisha katika vyombo vya dola na wengine kufungwa jela wenye hatia. Kwa sasa changamoto hiyo imekwisha kabisa na kubaki historia tu,au simulizi".

> Dalili zingine za kutaka kuanza mapigano zilianza kujitokeza mwaka 2017, 2018, chanzo chake ni kilekile cha kupigania mipaka ya ardhi, mashamba na wizi wa mifugo kutoka koo hizo.

### MGODI NORTH MARA

SACP Mwaibambe, anasema mgodi wa North Mara (Acacia) ulikuwa moja ya vyanzo kuchangia uhalifu wa watu kuvamiwa katika makazi yao na kuuawa, mifugo ikibiuwa.

"Mgodi wa North Mara (Acacia) uko kati kati ya makazi ya watu, hivyo uvamizi na uharifu hapo awali ulikuwa mkubwa kwa watu kuuawa, lakini hivi sasa ushirikiano wa polisi na wananchi ni mzuri, pamoja na mgodi huo, matukio hayo yameisha kiasi kikubwa," anasema SACP Mwaibambe.

### MAUAJI YA ARDHI

Anasema mauaji ya silaha za moto na jadi, mishale na mapanga yashika nafasi kubwa, lakini safari kuanza mwaka 2009 ilipoanzishwa Kanda Maalum hadi kufika mwaka 2019, silaha hizo zimekosa nafasi.

"Kuanzia mwezi mei mwaka huu mauaji ya kutumia silaha za moto na jadi hayana nafasi tena, tofauti na miaka ya nyuma. Hata mwaka 2017 na 2018, dalili za mapigano zilipoanza kujitokeza, tulizizima na kuchukua hatua," anasema, akisisitiza sheria imechukua mkondo wake, huku elimu kwa umma ikitolewa; mauaji yamepungua kwa asilimia 80.

### WIZI MIFUGO

Anasema wizi wa mifugo hivi sasa umebaki kidogo tofauti na zamani kulikuwapo uporaji wa kutumia silaha za moto na sasa kampeni za kudhibiti wizi huo imeshaanzishwa Tarime na Rorya, kwa kushirikiana na wananchi, Polisi wanatoa elimu, wizi wa ng'ombe ukipungua kwa asilimia 90.

Ansema ni mkakati ulioko hadi kwenye machinjio ya nyama, ng'ombe kabla ya kuchinjwa ni sharti akaguliwe na taarifa hutolewa na wananchi Polisi, wizi unapobainika.

### MAGENDO MPAKANI

Anafafanua kuwa uvushaji wa magendo mpakani anakiri upo, hasa ikizingatia kuwapo undugu uhusiano wa pande mbili za mpakani.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Mpakani Sirari, Mara, anasema wamekuwa wakishirikiana na Polisi Kanda Maalum Tarime na Rorya, kudhibiti magendo hayo ya mpakani na katika njia za panya.

"Hivi sasa tumekabidhiwa zawadi ya gari la kufanyia doria na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Charles Kichele(Hivi sasa Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG)," anasema SACP Mwaibambe na kuongeza:

"Ni kutokana na kuwapo kwa shughuli hizo zinazofanana katika makosa ya jinai ili tuweze kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaojihusisha na matukio ya kupitisha magendo mpakani."

### ULIMAJI BANGI

Katika kilimo cha bangi na biashara na dawa nyingine za kulevya, Polisi inasema havina nafasi tena kutokana na wahusika kukamatwa na wamechukuliwa hatua za kisheria.

"Kesi kubwa zilizoko mahakamani ni dawa za kulevya,mirungi na kilimo cha bangi ambazo zinachukua nafasi kubwa zaidi, lakini pia uharifu ziwani umepungua,' anahitimisha SACP Mwaibambe.

Pia, anasema ukatili wa kijinsia, mwingiliano wa makabila bado imekuwa kawaida yake pamoja na jamii kuwaficha wahalifu ingawa jeshi la Polisi linatumia mbinu kubwa kuhakikisha linawafichua wahalifu hao na kuwachukulia hatua za kisheria.

Hata hivyo, Kamanda Mwaibambe, anasema wamefanikiwa kutoa elimu kupitia mikutano ya wananchi, uti wa sheria bila shuruti, kuondoa mfumo dume, ukatili wa kijinsia pamoja na ufichuaji wa uhalifu.

Analisifu jeshi lake kupitia Kanda Maalum ya Tarime na Rorya, kwamba limekuwa mkombozi wa wananchi katika usalama wao na mali zao na tayari wameshajenga makao makuu ya mkoa wa kipolisi na baadhi ya makazi ya askari, baada serikali kutoa fedha za ujenzi.

"Katika ujenzi huo wadau nao wamechangia pamoja na halmashauri ya mji wa Tarime, ambayo ndiyo ilitupa eneo la kujenga, lenye ukubwa wa ekari 20 lililopo Nyandoto nje kidogo ya mjini Tarime," anasema SACP Mwaibambe..

# Kinamama wampigia saluti Magufuli miaka 4



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI Rais John Magufuli leo anatimiza miaka minne ya uongozi, vikundi vya kijinsia, watetezi wa haki za binadamu na wasomi wanapaza sauti za kumsifu kuwajali kinamama katika nafasi za uongozi wanazostahili.

Hiyo inachukua nafasi, huku taifa nalo likiweka historia kwa mara ya kwanza kuwa na Makamu wa Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan, katika awamu tano za uongozi kitaifa.

Anaemy Sillayo, Meneja Utafutaji Rasilimali wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), anasifu hatua hizo zimeenda sambamba na udhibiti wa vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini.

> “Nafasi hizi huwa zinatolewa kutokana na utashi wa kiongozi husika aliye madarakani kwa wakati huo.

“Tumeona madawati ya jinsia kupitia Jeshi la Polisi yameanzishwa nchi nzima na tumekuwa tukishirikiana nao vizuri sana na wao wenyewe wanapokutana na masuala yanayohitaji kutatuliwa kisheria zaidi huwa wanatuletea, Sillayo anasema.

Mwanazuoni maarufu kutoka Kenya, Prof. Patrice Lumumba, katika moja ya mihadhara yake, alitamka alichokitamani akikipa jina la ‘Magufulification of Afrika’, akimaanisha Bara la Afrika linapaswa kuongozwa kwa mfumo anaoutumia Rais Magufuli nchini.

Hata hivyo, baadhi ya wadau watetezi wa haki za binadamu na jinsia, wana maoni kwamba bado kuna haja ya kinamama kupewa fursa za uongozi zaidi ya zilizopo sasa.

“Uchaguzi wa mwaka 2015 ulivunja rekodi ya kumteua Makamu wa Rais mwanamke tangu tupate uhuru, tutaendelea kuipongeza serikali ya awamu ya tano kwa hatua hii, ambayo imeweka historia katika nchi yetu,” Deo Temba, Ofisa Programu Mwandamizi kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), anasema.

Kwa mujibu wa mtandao huo, katika miaka minne ya serikali hiyo, wanawake walioko katika nafasi za juu za uongozi: Mawaziri asilimia 17 na makatibu wakuu wa wizara asilimia 11.

Kwa upande wa wakuu wa mikoa, mtandao huo unabainisha kuwa wako asilimia 23 wakati wakuu wa wilaya asilimia 28.

Katika ushiriki uongozi ndani ya vyama vya siasa, TGNP inasema bado kuna tatizo la idadi ya wanaoteuliwa kuwania nafasi mbalimbali za juu.

Temba anarejea takwimu za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, wanawake walioteuliwa kuwania ubunge ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni asilimia tisa; Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema) asilimia sita; Chama cha Wananchi (CUF) asilimia 11; na ACT-Wazalendo ambacho kilikuwa na kiwango kikubwa cha asilimia 15.

Kuhusu udiwani, anasema kati ya wagombea 10,879, wanawake walikuwa 679, sawa na asilimia 6.24. Bila ya kutaja takwimu, LHRC inaeleza kwamba, uwakilishi huo wa kinamama umepungua katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, huku Meneja Utafutaji Rasilimali wa LHRC, Sillayo, akiitolea ufafanuzi:

“Hatuwezi kulaumu, kwa sababu hatuna sheria ambayo imeelekeza kwamba nafasi za wanawake katika uongozi na hasa wa kuteuliwa ziweje. Nafasi hizi huwa zinatolewa kutokana na utashi wa kiongozi husika aliye madarakani kwa wakati huo.

“Kwa upande wa wabunge pekee, Katiba ndiyo inazungumzia wanawake wasipungue asilimia 30, lakini katika maeneo mengine hasa ambayo yanahitaji uteuzi kama mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya na makatibu wakuu, Katiba haizungumzi chochote.”

Anatoa mfano wa wizara takriban 20 zilizopo, lakini mawaziri wanawake ni wanne tu, ambao ni: Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu; Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; Prof. Joyce Ndalichako; Waziri wa Uwekezaji, Angela Kairuki; na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama.

Sillayo anasema kukosekana kwa idadi kubwa ya wanawake katika nafasi za juu za uamuzi, kunachangia kusuasua kwa mambo mbalimbali, hususani yanayolenga usawa wa kijinsia.

“Japokuwa tunashukuru kwamba kitendo cha kumpatia mwanamke katika nafasi moja hiyo kubwa ya kuwa msaidizi wa Rais, kimetupa nguvu kubwa na tumeshuhudia mchango mkubwa anaouonyesha katika kutetea wanawake na kuwapa moyo kupambana katika kupata nafasi mbalimbali za uongozi,” anasema.

Pia, anataja vita binafsi ya Rais Magufuli anapokemea hadharani vitendo vya unyanyasaji na kutolea maelekezo ya kutekelezwa na viongozi mbalimbali, wakiwamo wakuu wa mikoa katika suala la mimba za wanafunzi.

# Miundombinu, usafiri JPM kaenea kila kona

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA miaka minne inayofanyiwa sherehe leo, Rais John Magufuli na timu yake ya uongozi, tayari wameshabeba sifa kemkem ya ustawi wa miundombinu kitaifa.

Ni zao la kinachoitwa ‘uamuzi mgumu’ wa kuasisiwa na kuendelezwa kwa miradi mikubwa, ikiwamo ya reli, barabara na vivuko na kuiweka nchi katika sifa ya kimataifa, uelekeo inaoulenga ifikapo mwaka 2025.

Tangu kipindi hicho hadi leo, utawala huo umeshafanya mambo kadhaa, ambayo ni pamoja na ujenzi wa barabara za juu ‘flyover’ jijini Dar es Salaam, akianza na ukamilishaji wa liliyopo eneo la Tazara iliyogharimu Sh. bilioni 94.03. Wakati inaanza, alikuwa waziri msimamizi wa mradi huo.

Ni mfumo wa barabara kuruhusu magari kupishana, ili kupunguza adha ya msongamano uliofanya magari kutumia muda mrefu barabarani jijini.

Hivi sasa, Rais Magufuli anaendelea na mradi mwingine kama huo eneo la Ubungo katika makutano ya Barabara za Mandela na Morogoro, unaogharimu Sh. bilioni 177.42, ukienda sambamba na upanuzi wa barabara kati ya Kimara na Kibaha mkoani Pwani.

Pia kuna ujenzi wa Daraja la Selander kuvuka bahari, kuunganisha eneo la Ocean Road na Oysterbay jijini; wakati jijini Mwanza kuna mradi wa ujenzi wa daraja Ziwa Victoria kutoka Kigongo hadi Busisi, ambao usanifu wake unaendelea.

Siku chache zilizopita, Rais Magufuli alizindua hatua za kwanza za ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa maji katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler’s Gorge, unaotarajiwa utakapokamilika, utafua umeme wa zaidi ya Megawati 2,000.

Ujenzi wa reli ya kisasa, maarufu Standard Gauge, umo katika orodha ya miradi mikubwa zaidi ya kitaifa utakaochukua miaka sita na kugharimu kiasi kikubwa cha fedha, inaingia katika rekodi kubwa zinazogusa utendaji wake.

Hata hivyo, mpangokazi wa mradi huo unaohusu ujenzi wa reli yenye urefu wa kilometa 1,219 kati ya Dar es Salaam na Mwanza, ukitekelezwa kwa awamu, ulianza zamani. Unatarajiwa kuwa na treni za kisasa zenye mwendokasi wa kilometa 160 kwa saa.

Sifa nyingine katika eneo hilo la usafiri ni kulipa uhai mpya Shirika la Ndege (ATCL) ambalo lilikuwa taabani na sasa linaendelea kupatiwa ndege mpya, ukarabati wa bandari, meli na vivuko mbalimbali.





# Wapewa elimu ya thamani maarifa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalowezesha utoaji wa taarifa zenye umahiri katika nyanja za uelimishaji, kujenga uwezo na kuleta matokeo chanya kwa jamii (Elimisha), limeanzisha mpango bunifu wa kuongeza thamani ya maarifa ili kuiwezesha jamii kufikia maisha yenye furaha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake juu ya mafanikio ya shirika hilo katika kusaidia wananchi kuongeza thamani ya maarifa ili kuleta furaha ndani ya familia.

Alisema Mpango unalengo la kuhakikisha kila mwananchi ana uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya bajeti kuanzisha ngazi ya familia hadi taifa alisema watahakikisha wanaelimisha jamii kujua mapato na matumizi yanayopatikana ili kusaidia kufanya shughuli zingine za maendeleo.

"Tumeamua kuanzisha mpango huu bunifu wa kimkakati ambao ni endelevu kwa lengo la kuhakikisha jamii inafikia furaha ya maisha kwa kufahamu mapato na matumizi yanayopatikana.

"Hii itasaidia kila mmoja kufahamu anatumia kiasi gani cha fedha na anaingiza shilingi ngapi kwa siku. Mkakati huu utamwezesha kila mmoja kuwa na matumizi sahihi ya fedha atakazokuwa anazipata," alisema Sikagonamo.

Alisema katika utafiti waliofanya kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe, ulibaini wananchi kuwa na uelewa mdogo kuhusu bajeti wengi hawajui kiasi cha fedha wanachokipata na wachokitumia, lakini hawana vipaumbele vya mahitaji yao badala yake mtu hununua au hutumia kitu pale anapokiona.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa zipo faida mbalimbali zinapatikana kwa sababu ya kuzingatia bajeti ambayo inahusisha mapato na matumizi miongoni ni kupunguza vitendo vya uhalifu vikiwamo rushwa na wizi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Ofisa Habari wa Elimisha, Elizabert Nyivambe, alisema mwananchi akifahamu bajeti ni rahisi kukuza uchumi wake, itamsaidia kupunguza mahitaji yasiyo ya lazima na itamletea faida pia kuongeza mapato kufungua ajira.

Alisema waathirika wa matumizi ya bajeti ni vijana kwa sababu ya changamoto ya ajira na mitaji baadhi yao hawana uelewa wa namna ya kubana matumizi kwa kiasi cha fedha kinachopatikana.

Nyivambe alisema mpango huo bunifu wa kuongeza thamani ya maarifa kwa kutumia fikra bunifu ili kuiwezesha jamii kufikia maisha yenye furaha, utapunguza vichocheo vya umaskini miongoni mwa jamii.

# Waandishi wapewa somo uchaguzi mitaa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAANDISHI wa habari nchini wameshauriwa kutoogopa kuripoti masuala mbalimbali yanayolenga kuisaidia jamii huku wakihakikisha wana uhuru wa kujieleza na kukusanyika wakati wa kutimiza majukumu yao bila kuvunja sheria na kanuni.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na wakili kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), William Mtwazi, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe yaliyolenga kufahamu uhuru wa kujieleza na kukusanyika hasa kwenye mchakato huu wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wakili Mtwazi alisema miongoni mwa sababu zinazokwamisha jitihada za wanahabari na kuwa waoga kuripoti masuala mbalimbali yanayotokea kwenye jamii ni matamko ya baadhi ya viongozi kutokuzingatia viwango vya weledi na kusababisha hofu.

Alisema matamko hayo yamekuwa kikwazo kwa wanahabari nchini kwa kuwa wanashindwa kupata uhuru wa kujieleza na kukusanyika jambo ambalo ni kinyume cha sheria na katiba ya nchi.

"Kituo cha haki za binadamu tumekuwa tukifanya kazi kwa karibu na wanahabari. Tunatoa msaada wa kisheria au elimu pindi wanapokumbwa na madhila wakati wa kutimiza majukumu yao.

Taaluma ya habari ni daraja kati ya wananchi na serikali na wadau wengine na ili watimize majukumu yao lazima wapewe uhuru wa kujieleza na kukusanyika kusaidia kuibua masuala mbalimbali ambayo yako kinyume na sheria au kupongeza mazuri yanayofanywa," alisema Mtwazi.

Aliongeza kuwa si kundi la wanahabari pekee ambao wanakumbana na changamoto katika kutekeleza majukumu yao, lakini watetezi wa haki za binadamu nao wanakabiliwa na vikwazo ikiwamo kudhaniwa wako kinyume na serikali pindi wanapokosoa au kuishauri serikali.

Mwanasheria kutoka LHRC, Fortunata Ntwale, aliwasisitiza wanahabari kutokuwa sehemu ya uvunjifu wa sheria na kanuni za nchi badala yake watimize majukumu yao kwa majibu wa taaluma yao.

Mwandishi nguli nchini, Felix Mwakyembe, alisema miongoni mwa sababu zinasababisha wanahabari kufanya kazi kwenye mazingira magumu ni wao wenyewe kutofahamu mipaka yao.

Alisema wanahabari wengi wamesahau misingi ya kazi zao na badala yake kukubali kutumika na watu wachache wenye malengo binafsi na matokeo yake kuleta chuki ndani ya jamii.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuchimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Kata ya Itezi, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki, wakati wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo, pamoja na Maofisa wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) mkoa, walipotembelea na kukagua baadhi ya miradi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mpango kumsaidia mwanamke waiva

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASASI isiyo ya kiserikali inayotekeleza programu za kuendeleza sekta ya kilimo kwenye masuala ya masoko, utawala bora na sera (MIICO), imeanzisha mpango maalum wa kumsaidia mwanamke mjasiriamali kupaza sauti (Sauti ya Mwanamke Sokoni) ili kupinga vitendo mbalimbali vya ukatili.

Mkuu wa Programu wa MIICO, Catherine Mulaga, alisema hayo wakati wa kikao cha kujadili changamoto zinazowakabili wanawake sokoni na kuweka mpango kazi wa namna ya kukabiliana nazo.

Alisema walianzisha programu ya Sauti ya Mwanamke Sokoni baada ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake wajasiriamali wanaojitafutia riziki.

Mulaga alisema katika utafiti walioufanya kwenye sekta isiyo rasmi, walibaini tatizo la ushiriki mdogo wa wanawake katika nafasi za uongozi kwenye masoko jambo linalosababisha kushindwa kushughulikia masuala yao.


Alisema tatizo lingine ni kushamishiri kwa ukatili wa kijinsia ambao husababisha wanawake kutukanwa, kudhalilishwa, uonevu na adha ya upatikanaji wa maji hali inayosababisha kinamama kupata shida wanapokuwa hedhi.

"Tumelenga kufikia masoko manane yakiwamo ya Ilomba, Soweto, Mabatini, Uyole na Uhindini katika Jiji la Mbeya kutoa elimu ya kutambua haki zao na kuimarisha shughuli zao na kuongeza kipato," alisema Catherine.

Aliongeza kuwa watahakikisha wanawafikia wafanyabiashara wote walioko masokoni na kuwahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili kuanzisha miradi ya pamoja, kukopesheka kwenye taasisi za kibenki na kupata mafunzo mbalimbali.

Ofisa Maendeleo Jiji la Mbeya, Magdalena Ngenzi, alisema MIICO imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mwanamke anayefanya biashara zake sokoni anatimiza majukumu yake bila kupata changamoto.

Alisema asasi hiyo imewapa nguvu kinamama kujiamini na kufanya shughuli zake, lakini kuunganishwa na huduma za kisheria kutetea haki zao kutetea maslahi yao pindi wanapoonewa.





# Mbaroni madai kuiba umeme Tanesco

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WATEJA 13 wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, wamebainika kuiba umeme na wakilisababishia hasara ya zaidi ya Sh. milioni 12 .9.

Meneja wa Wateja Wakubwa wa Tanesco Makao Makuu, Fredrick Njavike, alisema hayo jana, watu hao walibambwa wakati wa ukaguzi uliofanyika katika baadhi ya mitaa jijiji hapa mwisho wa wiki.

Njavike alisema katika ukaguzi huo, wateja 13 walibainika kuliibia shirika hilo, hivyo kusababisha hasara ya Sh. milioni 12.9 kutokana na wizi huo. Alisema watu hao ni miongoni mwa wateja 810 waliokaguliwa.

Njavike alisema kati ya wateja hao waliobainika kuiibia Tanesco, walishaanza kulipa faini na gharama hizo na kwamba Sh. 2,404,000 zimelipwa na zilizobaki ni Sh. milioni 10.5.

Aliongeza kuwa wateja wengi waliokamatwa kuiba umeme ni wale wenye biashara za maduka, kuchomelea na bucha za samaki.

Aidha, aliwatahadharisha wateja wa shirika hilo kuacha wizi wa umeme kwa sababu watakapobainika watatozwa faini na watasitishiwa huduma.

Alisema ukaguzi huo ni endelevu na utaendelea kufanyika kwa awamu katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Meneja huyo aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Tanesco kwa kuwapa taarifa za siri kuhusu wezi wa umeme katika ofisi za shirika hilo wilayani na mikoani

Mkazi wa Mtaa wa Mji Mpya jijini hapa, Aman Simon, alipongeza hatua hiyo kutokana na kufanyika kwa utaalamu wa hali ya juu.

"Kuna baadhi ya watu humu mitaani tunawaona wanaendesha biashara zao kumbe wanaliibia shirika, hao tunaomba washughulikiwe ili iwe fundisho kwa wengine," alisema.

Simon alisema Tanesco walikuwa kimya ndiyo maana wateja wasio waaminifu wametumia nafasi hiyo kufanya uhalifu huo wa kuiba umeme.



Mchuuzi wa vyungu vya kuwekea maua akisaka wateja katika Mtaa wa Makole jijini Dodoma wikiendi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ataka nguvu zaidi vita ukatili watoto

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKURUGENZI wa Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), Koshuma Mtengeti, amewataka wadau wa ustawi wa haki za watoto kupinga ukatili dhidi ya watoto unaoendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Mtengeti alisema hayo juzi katika mkutano wa mwaka uliofanyika wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma baada ya kuwapo kwa matukio mabaya ya ukatili wa watoto yanayofanyika katika jamii.

Alisema wanaofanya ukatili kwa asilimia kubwa ni watu wa jamii inayozunguka eneo husika jambo ambalo ni tatizo kubwa linalohitaji kufanyiwa kazi haraka ili litokomezwe.

"Naomba wazazi mjitahidi kulea watoto katika maadili mazuri, tuandae taifa la watoto wanaojitambua ili kuepusha kufanya ukatili hapo baadaye," alisema Mtengeti.

Mkurugenzi huyo alisema ukatili ni janga la kidunia na kuna mikoa ambayo tatizo hilo ni kubwa, hivyo juhudi zinapaswa kuonyeshwa na kila mmoja ili kudhibiti vitendo hivyo.

"Tanzania tuna mipango mikakati, mikataba mbalimbali, tumetia saini sheria na miongozo ambayo itasaidia kupiga ukatili," alisema.

Kutokana na hilo alisema wadau wa ulinzi wa haki na ustawi wa mtoto katika Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma wanatakiwa kushirikiana na kupunguza vitendo vinavyochochea ukatili wa kijinsia.

Alisema ni lazima kuangalia mila na desturi, malezi, usimamizi hafifu wa sheria na ukimya dhidi ya ukatili na kutafuta namna ya kukabiliana nalo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kumekuwa na msisitizo wa sheria kuliko wajibu, sheria inasema hakuna kutumikisha watoto inatakiwa kuiheshimu kuanzia mamlaka hadi kwa watu wazima.

Mtengeti alisema kuna gharama kubwa kutibu wahanga kutokana na kuwapo kwa gharama za familia na zile za serikali.

"Kuna mashirika mengi na wadau wengi wanaohusika na masuala ya lishe, pia kuna suala zima la kujengea watoto uwezo watambue afya ya uzazi na wazazi waongee na watoto na kuweka elimu ya kujitegemea shuleni," alisema.

Kwa upande wake, Hakimu Mkazi Debora Mnyabahi wa Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa alisema ushahidi ni tatizo kubwa katika kesi zinazohusikana na ukatili kwa kuwa wazazi wanakubaliana na mwisho wa siku hawapeleki mashahidi.

"Kesi za jinai zinahitaji ushahidi uliothibitika usioacha mashaka yoyote, wakati mwingine fomu za matibabu PF3 hazijazwi vizuri, madaktari wanajaza tu kwa ujumla huwezi kuitumia kumshawishi mtu." Alisema.

Alisema pia kumekuwa na changamoto kwenye kesi za utelekezaji familia, mwanaume anapofikishwa mahakamani akiachiwa na kurudi nyumbani anaenda kumrubuni mkewe anarudi kufuta kesi.

"Sheria inaruhusu mlalamikaji kuondoa kesi yake, ukifuatilia kwa umakini kesi hizi utaona washtakiwa wanatakiwa kuwajibishwa.

## Watoa huduma afya wafundwa

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WATOA huduma za afya wametakiwa kujitoa katika kuwahuduma wagonjwa na kufanya kazi kwa kujituma zaidi kwenye maeneo yao ya kazi ili kufikia malengo na mikakati ya serikali kuhusu kuwahudumia wananchi wake.

Mkurugenzi wa Afya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Ntuli Kapologwe, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo elekezi na ukamilishaji wa ajira kwa watumishi wapya wa afya chini.

Mafunzo hayo yako chini ya mradi wa RSSH, Global Fund na kutekelezwa na Taasisi ya Mkapa Foundation kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tamisemi na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Dk. Kapologwe aliwataka watoa huduma hao wa afya kujitoa katika kuwahudumia wagonjwa na kufanya kazi kwa kujituma zaidi kwenye maeneo yao ya kazi ili kufikia malengo na mikakati ya serikali katika kuwahudumia wananchi wake.

"Ndugu zangu kazi hii inahitaji kujitoa zaidi katika kuwahudumia wagonjwa wanaofika kupata huduma kwenu, naomba iwe kama ibada ya kutoa sadaka, msitoe huduma hiyo kwa kutegemea malipo," alisema .

Aliwapongeza vijana hao kwa kupata kazi hiyo kutokana na ukweli kwamba Julai, mwaka huu, serikali ilipotangaza nafasi za ajira za afya waliojitokeza watu 20,000, na hatimaye wakachukuliwa 550 tu.

Dk. Kapologwe alisema kati ya ajira hizo ajira 170 wataajiriwa na Taasisi ya Benjamin Mkapa (BMF) kwa mkataba na baadaye vibali vikitoka serikalini wataajiriwa moja kwa moja.

Aliwataka kwenda kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za kazi lakini wasiache kazi wanapokumbwa na changamoto katika maeneo yao ya utumishi wa umma.

Aidha, aliwakumbusha kwamba kufanya kazi kwa bidii na wakawe chachu ya maendeleo kwa kutoa huduma bora kwa wananchi kwenye maeneo watakayopangiwa.

"Hakuna njia ya mkato, mkafanye kazi kwa weledi na bidii, wagonjwa wafurahie huduma zenu na wala msichukue fedha za mgonjwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria utafungwa kwa kupokea rushwa," alisema.

Pia Dk. Kipologwe aliwapongeza BMF kutokana na mchango wao wa kuajiri wataalamu wa afya kwa kushirikiana na Tamisemi na Wizara ya Afya tangu kuanzishwa kwake 2006.

Alisema watoa huduma hao wamekuwa msaada mkubwa katika jamii wanapokuwa maeneo yao ya kazi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri.

Awali, Ofisa wa Programu wa Rasilimali Watu-Afya wa BMF, Christina Malembeka, alisema hadi Julai, mwaka huu, wameajiri wataalamu wa afya 1,439 katika ngazi mbalimbali mikoani.

Malembeka alisema taasisi hiyo inatekeleza mkakati wao wa tatu wa mwaka 2019 mpaka 2024 ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Kitaifa ya 2025 ya Malengo ya Maendelo Endelevu ya 2030.



# Rais Shein apongeza ushirikiano na Korea

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameipongeza Korea Kusini kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar na kusisitiza haja ya kuwapo ushirikiano katika sekta ya utalii baina ya pande mbili hizo.

Dk. Shein aliyasema hayo jana Ikulu mjini Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania, Cho Taeick.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Shein alimweleza Balozi huyo kuwa Zanzibar imeweza kuimarika katika sekta ya utalii kutokana na vivutio kadhaa vilivyopo sambamba na mikakati madhubuti iliyowekwa. Kwa mantiki hiyo, alisema ni jambo la busara iwapo watalii kutoka Korea Kusini watakuja kwa wingi kuitembelea Zanzibar.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha uhusiano na ushirikiano unaimarika zaidi kati ya pande mbili hizo hasa katika sekta ya utalii, iko haja ya kuwapo ushirikiano kati ya Zanzibar na kisiwa cha Cheju nchini Korea ambacho ni maarufu duniani kwa utalii.

Dk. Shein alisisitiza kwamba katika kuhakikisha mafanikio zaidi yanapatikana kwenye ushirikiano katika sekta ya utalii, hakuna budi kuanzishwa safari za ndege kati ya Zanzibar na Korea kupitia Shirika la nchi hiyo.

Alisema Korea Kusini imekuwa mshirika mkubwa wa maendeleo ya Zanzibar kwa kuwa imekuwa ikionyesha juhudi zake na kuwa bega kwa bega na Zanzibar katika kuimarisha miradi hiyo ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, tangu Korea kuanza ushirikiano na uhusiano wa kidiplomasia na Tanzania, ikiwamo Zanzibar mwaka 1992, imesaidia kwa kiasi kikubwa Zanzibar katika kuendeleza sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, elimu na uvuvi.

Naye Balozi Taeick aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa kuendeleza uhusiano na ushirikiano wa kidugu kati ya pande mbili hizo.

Pia alipongeza juhudi za SMZ za kuendelea kuviweka vizuri vivutio vya kitalii sambamba na mazingira ili kuwavutia wageni wanaokuja kuitembelea Zanzibar.

Alisema ni jambo la faraja iwapo ushirikiano utaimarishwa zaidi kati ya pande mbili hizo hasa katika sekta ya utalii kwa kuwa Zanzibar ina vivutio vingi vya kitalii na watu wa Korea wanapenda kuja kuviona.


Distributed via ippmedia

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Korea nchini Tanzania, Cho Taeick, Ikulu Mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# SMZ yatangazia vita wavuvi haramu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mkoa wa Kusini Unguja imesema itahakikisha inawachukulia hatua watu wote watakaojihusisha na uvuvi haramu ili kulinda rasilimali ya uvuvi.

Akizungumza wakati wa kuteketeza nyavu zinazotumika kwa uvuvi haramu katika ghuba ya Chwaka, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mohamoud, alisema iwapo uvuvi haramu utaachwa uendelee unaweza kuathiri viumbe bahari na kuharibu mazalia ya samaki.

Mkuu wa mkoa alisema ni vyema wavuvi wanapotaka kununua zana za uvuvi, wawasiliane na kamati za uvuvi ili kutambua zana sahihi ili kuepusha usumbufu na hasara baadaye kwa kuonekana hazifai.

Alisema wako baadhi ya wavuvi kwa makusudi wanajihusisha na uvuvi haramu jambo linalosababisha uharibifu wa mazingira ya bahari na mazalia ya samaki.

Pia Ayoub aliwata wazee wanaoishi katika ghuba hiyo kuwahamasisha vijana wanaojishughulisha na uvuvi kuacha uvuvi haramu kwa kuwa wao ndio washirki wakubwa wa uvuvi huo ambao unamadhara kwao na taifa kwa ujumla

Ili kuhakikisha uvuvi haramu unamalizika, alisema inahitajika kila mmoja kuondoa muhali huku akiahidi kwa upande wake hatokuwa na muhali na atamchukulia hatua kila atakayejihusisha na uvuvu haramu

Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, alisema serikali ya wilaya kwa kushirikiana na kamati za uvuvi, imendaa mikakati madhubuti wa kukabiliana na uvuvi haramu ili kulinda rasiliamali ya bahari.

Mkuu wa Doria Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Haji Shomari Haji, alisema miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni pamoja na gharama katika doria jambo ambalo linaleta ugumu katika utendaji wa kazi zao.

Nyavu 28 zenye thamani ya Sh. milioni 18 zimeteketezwa katika ghuba ya chwaka inahusisha kwenye Shehia za Uroa, Chwaka, Marumbi, Pongwe, Pwani Charawe, Ukongoroni na Michamvi.

# UWT yataka ujenzi wa ofisi za kisasa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UMOJA wa Wanawake wa Tanzania (UWT) umewataka wanachama wa jumuiya hiyo kuwaruhusu viongozi na wanachama kutoa michango mbalimbali katika kuchangia maendeleo ya ujenzi wa majengo ya jumuiya kwa mujibu wa utaratibu.

UWT imesema si viongozi tu bali hata wanachama wowote wanaruhusiwa kutoa michango hiyo ili mradi wapitie katika utaratibu ambao umewekwa ili kundoa sitofahamu.

Makamu Mwenyekiti UWT, Thuwayba Kisasi, alisema hayo jana wakati akipokea mifuko 200 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za jumuiya hiyo katika mkoa wa Kaskazini Unguja, wenye thamani ya Sh. milioni tatu ambao umetolewa na Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa huo, Angelina Malembeka.

Alisema hazuiwi mwanachama yeyote wa UWT katika kuchangia maendeleo kwa dhamira ya kuijenga jumuiya ili mradi kamati za utekelezaji za jumiya na Chama zifahamu suala hilo.

"Katika suala la kuendeleza ofisi za jumuiya ili ziwe za kisasa, ni vyema wanachama na viongozi wa CCM kwa pamoja wakaendelea kushirikiana kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika utoaji wa misaada," alisema.

"Chama si wanachama tu bali pia majengo ya kisasa kutokana na kuwa chama hiki kina hadhi yake. Lazima jumuiya hii iwe na majengo ya hadhi ya kisasa, hivyo ninampongeza Mbunge kwa kutoa mchango huu kwa ajili ya kukijenga chama," alisema.

Aliongeza kuwa kinachotakiwa kwa kipindi hiki ni kuongeza kasi ya kuzitatua changamoto za wananchi kama CCM ilivyoelekeza ili kuipatia ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kisasi alisema ni vyema wanachama wa CCM kwa pamoja wakashirikiana na kuacha tofauti zao na mivutano ambayo haileti maana katika kuhakikisha chama kinashinda kwa kishindo mwaka 2020.

Malembeka kwa upande wake alisema mchango huo ameutoa kutokana na kuunga mkono chama katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa vitendo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya UWT kuwa ya kisasa.

Alisema UWT mkoa wa Kaskazini imejenga jengo la ofisi yake lakini imeishia hatua ya mwanzo na kwamba mchango wake huo utasaidia kuendeleza ujenzi huo ambao ulisimama kwa muda.

# Korti yamtia hatiani mtendaji

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, imemhukumu adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya Sh. 500,000, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Igurubi, Ntemi James (50), baada ya kupatikana na hatia ya kushindwa kutoa hati za vielelezo kwa ajili ya uchunguzi.

Mwendesha Mashtaka, Elimajid Kweyamba, alidai kwamba mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 10(2) na 24 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai sura ya 20 mapitio ya 2002 inayosomeka pamoja na kifungu cha 8(1) (3) (6) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya 2007.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Lydia Ilunda, mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Septemba 8, mwaka 2017 na Oktoba 11, mwaka 2017 katika Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mjini Igunga, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kama ofisa mtendaji Kata ya Igurubi, huku akifahamu kuwa vitabu pamoja na hati mbalimbali vinahitajika kwa ajili ya ushahidi mahakamani, kwa makusudi na bila halali alishindwa kutoa vielelezo hivyo akiwa na nia ya kufanya visitumike wakati wa shauri la jinai.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo baada ya kusomewa shtaka hilo alikana, ndipo upande wa mashtaka ulipopeleka mashahidi wanne wakiwa na vielelezo mbalimbali.

Hata hivyo, baada ya hakimu kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, ndipo alisema mahakama imeridhishwa na ushahidi uliotolewa pasipo shaka yeyote, hivyo imemuona mshtakiwa ana hatia kisha kumuhukumu adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya Sh. 500,000.

Hata hivyo, mshtakiwa alifanikiwa kulipa kiasi hicho cha fedha na kuachiwa huru.

# Ajinyonga kisa wivu wa mapenzi

**Na Gurian Adolf, NKASI**

KIJANA Musiba Marko (26), mkazi wa Kijiji cha Kasu Kata ya Milundikwa wilayani Nkasi mkoani Rukwa, amejinyonga kwa kutumia kamba ya katani baada ya kumkuta mpenzi wake akiwa na mwanaume mwingine.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Benaziri Kalamba, alisema kuwa tukio hilo likitokea jana asubuhi baada ya majirani kugundua kuwa alijitundika chumbani kwake.

Baada ya taarifa kuenea kijijini hapo zilifika katika ofisi ya mtendaji huyo kisha aliamua kwenda kuangalia na kutoa taarifa polisi.

Alisema kuwa kijana huyo ni mwenyeji wa mkoa wa Geita ambapo alifika kijijini hapo kwa muda, akifanya kazi za ufundi ujenzi.

Ilielezwa kuwa baada ya kufika Kijijini Happy alianza mahusiano ya kimapenzi na msichana mmoja.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Justin Mangazini, alisema kuwa licha ya kutoacha ujumbe baada ya kujinyonga, lakini rafiki zake walidai siku tatu kabla ya tukio hilo, alimkuta mpenzi wake huyo akiwa na mwanaume mwingine ambaye alidaiwa kuwa naye kimapenzi, kitendo kilichomkasirisha.

Alisema tangu alipomkuta mpenzi wake huyo na mwanaume mwingine ghafla mawasiliano baina yake yalipotea bila sababu, kitendo ambacho kilimuudhi na kuwalalamikia rafiki zake hao.

Mtendaji huyo alisema kuwa huenda ndiyo sababu ya kuchukua maamuzi hayo ya kujinyonga.

Hata hivyo, baada ya uchunguzi wa polisi, waliruhusu kufanya maziko na waliwasiliana na familia yake iliyopo mkoani Geita, ambao pia waliruhusu mazishi kufanyika katika kijiji hicho cha Kasu.

Katibu Tawala wa Wilaya Nkasi, Cosmas Kuyela, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, ingawa alisema hajui sababu za kijana huyo kuchukua maamuzi hayo magumu ya kujinyonga.

Hata hivyo, aliitaka jamii wilayani humo kuwashirikisha watu wengine matatizo yao ili kupata ufumbuzi kwani kukaa kimya kunasababisha kushindwa kuhimili na kufikia kuchukua maamuzi kama hayo.




Mafundi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), wakiendelea na ujenzi wa jengo la machanjio ya kisasa, iliyopo eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viongozi ushirika pamba kizimbani

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, imewapandisha kizimbani viongozi sita wa chama cha msingi cha wakulima wa pamba (AMCOS ) wa Kijiji cha Choma katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wakulima wa zao hilo.

Waliopandishwa kizimbani ni Mwenyekiti wa Baumu Amcos, Nyolobi Nangale (36), Sylivester Masanyigule (46), Andrew Senga(49), Iwize Masanja(37), Martine Silas (31), Elias Kelege (25), wote wakazi wa Kijiji cha Choma Kata ya Choma Tarafa ya Manonga.

Mapema Mwendesha Mashtaka wa Takukuru wa Wilaya ya Nzega, Mazengo Joseph, alidai washtakiwa wote walitenda makosa hayo kinyume cha kifungu cha 15(1) na 3 (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya 2007.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Lydia Ilunda Joseph, alidai kwamba washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu likiwamo la kwanza linalodai kuwa kati ya Agosti 01, mwaka huu kwa muda tofauti katika Kijiji cha Choma waliomba rushwa ya Sh. 800,000 kutoka kwa Kulwa Mabula ili kumlipa Sh. 8,345,220 alizokuwa akidai Kampuni ya OLAM inayonunua pamba.

Katika shtaka la pili kwa washtakiwa hao inadaiwa pia kuwa katika tarehe hiyo na muda tofauti washtakiwa wote kwa pamoja waliomba rushwa ya Sh. 600,000 kutoka kwa Shimbi Ganja ili waweze kumlipa Sh. milioni 6,536,400 alizokuwa ameuza pamba kwenye kampuni inayonunua zao hilo ya OLAM.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka huyo, katika shtaka la tatu inadaiwa washtakiwa hao katika tarehe hiyo na muda tofauti waliomba ruhswa ya Sh. 600,000 kutoka kwa Shimbi Kadengu ili waweze kumlipa Sh. 6,220,680 alizokuwa ameuza pamba kwenye Kampuni inayonunua zao hilo ya OLAM.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka yote walikana, na kesi hiyo imeahirishwa hadi Novemba 6, mwaka huu itakapotajwa tena, huku washtakiwa wawili wakipata dhamana ya Sh. milioni tano kila mmoja na washtakiwa wanne wamepelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.

## HABARI KITAIFA

# Biteko aonya rushwa kwa wawekezaji

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amewaonya watendaji watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kuomba rushwa kwa wawekezaji wa madini na kusisitiza hataki kuona wawekezaji wakisumbuliwa.

Biteko alitoa onyo hilo jana kwa nyakati tofauti wilayani Nyang'hwale, Geita alipotembelea na kukagua kiwanda cha uchenjuaji wa marudio katika mgodi wa wachimbaji wadogo Nyamigogo na mgodi wa Bululu ambao uko mbioni kupata leseni ya uchimbaji.

Alisema uwekezaji katika sekta ya madini hauna urasimu, hivyo serikali haipendi kuona wawekezaji wakisumbuliwa kwa kuombwa rushwa.

"Sitaki kuona wawekezaji kwenye sekta ya madini wa kisumbuliwa kwa rushwa na sitaki kusikia kuna urasimu wa aina yoyote," alisema.

Waziri huyo alitumia fursa hiyo kuwataka Watanzania hususani wafanyabiashara kuwekeza katika sekta ya madini nchini kwa kuwa wanaweza kuwekeza kwa gharama kidogo na kupata faida kubwa.

Katika hatua nyingine, Biteko aliwaagiza maofisa wa serikali wanaokwenda kusimamia uchomaji, usimamizi na uzalishaji wa madini ya dhahabu kuwa mstari wa mbele kuhakikisha taarifa na kumbukumbu zinajazwa vizuri.

Pia aliwataka wamiliki wa viwanda vya kuchenjua marudio na viwanda vya kuyeyushia dhahabu kutekeleza matakwa yao ya kisheria. Alisema kutokuwapo kwa taarifa na kumbukumbu zilizoandikwa vizuri kunaashiria kuwapo nia mbaya na udanganyifu.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Tanzania (Femata), John Bina, kwa niaba ya wachimbaji wadogo, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwaruhusu kuchimba kwenye maeneo yao bila kubughudhiwa.

Alisema Rais Magufuli ameonyesha nia nzuri ya kutaka wachimbaji wadogo nao wainuke kiuchumi, hivyo kuwataka wachimbaji hao kubadilika.

# Prof. Assad akosoa huduma taasisi za fedha za kiislamu

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema taasisi za kiislamu za fedha hazitekelezi matakwa ya jamii ikilinganishwa na benki za kawaida.

Prof. Assad aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza katika mkutano wa sita wa Taasisi za fedha za Kiislamu za Afrika.

"Natolea mfano mdogo wavuvi wa samaki tangu miaka ya nyuma watu wanakaanga samaki hadi sasa ni lazima tuwe na mipango ya kuwezesha watu wetu wanapokwenda kuvua samaki basi wawe na vyombo vikubwa kama boti wakishavua wanawahifadhi katika boti wanapofika wanawatengeneza kwa ajili ya kuwasafirisha nje ya nchi," alisema Prof. Assad.

Assad alisema benki ikiweze kufanya uwezeshaji wa aina hiyo itasaidia kuwainua hata kama watakuwa katika vikundi na kuanza kuzirejesha fedha hizo.

Alisema tatizo kubwa la wajasiriamali waliopo wengi wao hawana uelewa kwani wanafika na kuomba mkopo na baada ya kuupata wanautumia katika matumizi mengine.

"Akiwa anahitaji mkopo atakuambia atafanya hivi na hivi, lakini akipata huo mkopo hafanyi kile ambacho amekieleza utaona kaenda kununua land Rover yake na mkewe amemnunulia Subaru zinazobaki anapeleka anapojua baada ya muda anajikuta amepata hasara," alisema.

Alisema jambo ambalo amelishauri ni watu kuwa waaminifu yaani wafanyabiashara wanatakiwa kuwa wakweli ukipewa fedha fanya kile ambacho umekikusudia ili kujenga uaminifu mzuri na benki iliyokupatia mkopo.

Alisema ambaye anakwenda kinyume husababisha janga la kutokuaminika.

"Yaani benki haikuamini wewe kwa sababu ukipewa hela unatumia tofauti na makubaliano tukitatua tatizo hilo basi mambo yatakwenda vizuri kwani suala la uaminifu ni tatizo katika benki inavyoanzishwa," alisema.

Aidha, alisema kumekuwa na dhana potofu kuwa taasisi za fedha za kiislamu ni kwa ajili ya kutoa huduma kwa waislamu tu jambo ambalo sio la kila kwani huduma zinazotolewa ni sawa na taasisi nyingine za kifedha kwa kila mtu bila kuangalia dini.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adof Ndunguru, aliwashauri wajadiliane kwa kina katika mkutano huo ili kuona ni namna gani ya kushughulikia changamoto zilizopo.

Alisema kuna changamoto ya uelewa katika jamii kuhusiana na huduma za kibenki zinazotolewa na taasisi za fedha za kiislamu ikilinganishwa na benki zingine.




Baadhi ya wasichana waliokimbia vitendo vya ukatili nyumbani kwao na kulelewa na Shirika la Matumaini kwa Wanawake na Wasichana Tanzania (Hope For Girls And Women Tanzania), lililopo Mugumu Serengeti mkoani Mara, wakijifunza kushona nguo juzi. **NA MPIGA PICHA WETU**

# 'Ushirikiano kiutafiti sekta binafsi, watunga sera muhimu'

**Na Mathias Canal,** ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema kuwa ushirikiano wa kiutafiti, kati ya sekta binafsi na watunga sera, ni muhimu katika kufanikisha mageuzi ya kilimo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Mkutano wa kwanza wa Afrika wa kudhibiti Sumukuvu kwenye vyakula uliofanyika jijim Arusha.

Waziri Hasunga alisema kuwa tangu kuibuka kwa tatizo la sumukuvu mwaka 2016, Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kupunguza kusambaa kwa sumukuvu nchini.

Alisema kwa kutambua changamoto za kukabili sumukuvu, kunahitajika kutumia njia mbalimbali kuanzia kwenye hatua za uzalishaji, uvunaji, uhifadhi, usindikaji na kuhusisha sekta za umma na binafsi katika kupunguza upotevu wa chakula na kuongeza upatikanaji wa chakula salama na lishe bora.

Alisema Tanzania imeanzisha Kamati Jumuishi ya Uendeshaji inayohusisha sekta na taaluma kutoka taasisi mbalimbali chini ya uenyekiti wa Wizara ya Kilimo ambayo ina mamlaka ya kusimamia masuala yote yanayohusu sumukuvu.

Aliwahakikishia washiriki kuwa kinga ya sumukuvu - Alfasafe TZ01; imeshasajiliwa kwa matumizi nchini Tanzania. "Aidha, nimefarijika kuwa kazi hii inafanywa na Kampuni Binafsi ambayo imewekeza katika uzalishaji, na usambazaji wa bidhaa hii ambayo itaokoa maisha ya watu nchini," alisisitiza

"Napenda kuwahakikishia utayari wa Wizara yangu katika kuyatumia maazimio mtakayokubaliana katika mkutano huu. Aidha, Serikali ya Tanzania inatilia maanani na inaunga mkono hatua zinazochukuliwa katika kuhimiza biashara ya chakula salama, usalama wa chakula na lishe."

Tanzania kwa sasa inatekeleza Awamu ya Pili Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo (ASDP II) yenye lengo la kuleta mageuzi ya sekta ya kilimo kuwa na kilimo chenye tija na kibiashara, pamoja na kukuza uchumi wa wakulima wadogo na kuboresha maisha, uhakika wa chakula na lishe bora.

Uhakika wa chakula na lishe ni mhimili ambao ni muhimu wa ASDP II Katika kufikia malengo hayo, uwekezaji katika utafiti wa kilimo ni muhimu katika kuleta matokeo kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani.

Waziri Hasunga alisema kuwa kutokana na takwimu za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) za mwaka 2017, Tanzania inaongoza katika uzalishaji wa mahindi na karanga katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki, kwa kuzalisha tani milioni 6 na tani milioni moja mtawalia.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio hayo, Serikali inatambua kuwa ingawa mazao hayo ni muhimu kwa chakula cha kila siku, lakini yanakabiliwa na ukubwa wa tatizo la sumukuvu ambalo linahatarisha usalama wa chakula na kuwa kikwazo cha biashara ya mazao hayo kwa nchi jirani na Tanzania.

Mkutano huu uliwakutanisha watafiti, wafanyabiashara, watunga sera na wadau wa maendeleo, ambao unalenga kupanga mikakati ya kuongeza kasi ya matumizi ya kinga ya sumukuvu, na kukabili sumukuvu barani Afrika.

# Uboreshaji mazingira biashara kichocheo cha uwekezaji EPZ

**Na Mwandishi Wetu**

UBORESHAJI wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, umeongeza hamasa ya uwekezaji wa viwanda katika maeneo maalum ya uwekezaji ya EPZ unaofanywa na wawekezaji wa ndani kufikia zaidi ya asilimia 43.

"Hamasa imekuwa kubwa sana kwa wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa mbalimbali na vivutio vinavyotolewa na mamlaka ya ukanda maalumu wa uwekezaji nchini EPZA," alisema Ofisa Mwandamizi Uwezeshaji, Uwekezaji wa EPZA, Nakadongo Fares.

Alisema hayo wakati akifanya wasilisho katika kongamano la biashara na uwekezaji linalofanyika mkoani Mtwara mwisho wa wiki.

Alisema uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara nchini inayofanywa na serikali kwa kuondoa na kupunguza kodi mbalimbali imeongeza hamasa kubwa sana kwa wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa za uwekezaji katika viwanda.

Uwekezaji katika viwnda unaofanywa na wawekezaji wa ndani ni kichocheo kikubwa sana katika kujenga uchumi wa viwanda katika juhudi za taifa kumfanya Mtanzania afikie kipato cha kati mwaka 2015.

Alisema viwanda hivi ambavyo vipo katika sekta mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa kuzalisha ajira nyingi kwa Watanzania hatua ambayo imepungua umaskini wa kipato kwa mtu mmoja mmoja.

Kwa mfano kuna fursa kubwa sana katika uzalishaji wa korosho ambapo wawekezaji wa ndani wanahimizwa kuchangamkia fursa hii kwa kuwekeza katika viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya korosho.

Kuna bidhaa nyingi sana zinaweza kutengenezwa kutokana na korosho na mabibo yake na kuweza kuingizia wawekezaji wa ndani na kuchangia ongezeko la pato la taifa.

"Kupitia kongamano hili la biashara na uwekezaji hapa mkoani Mtwara tunawahimiza wawekezaji wa ndani kutumia nafasi hii na fursa inayotolewa na mamlaka ya EZPA kuwekeza katika viwanda vya kuchakata korosho na mazao mengine," alisema.

Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya ajira 50,000 zimetengenezwa kupitia uwekezaji katika viwanda chini ya EPZA tangu ilipoanzishwa zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Pia uwekezaji katika maeneo ya ukanda maalumu umeingia taifa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 1.3 na kuvutia uwekezaji wenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 2.6.


Distributed via ippmedia

Mwenyekiti wa Bodi ya T-PESA, Brigedia Generali mstaafu, Ramadhan Kimweri (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, katika uzinduzi wa huduma mpya ya Bando la TamTam, ambalo linampa uhuru zaidi mteja wa TTCL kufurahia mawasiliano nafuu ya huduma za maongezi, intaneti pamoja na ujumbe mfupi (SMS). Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Corporation, Waziri Kindamba na Ofisa Mkuu wa T-Pesa, Lulu Mkudde. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi ushirika mikononi Takukuru

**Na Halima Ikunji,** TABORA

VIONGOZI wa vyama vinne vya msingi vya ushirika vya Mitowo, Balimi, Mole na Urafiki wilayani Sikonge, wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa tuhuma za rushwa.

Watu hao ni pamoja na mwenyekiti na wajumbe wanne ambao wanadaiwa kujihusisha na rushwa, ufujaji na ubadhirifu wa Sh. milioni 29 za malipo ya wakulima wa tumbaku katika msimu wa mwaka 2018/19.

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Tabora, Musa Chaulo, alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya kufanya uchunguzi dhidi ya viongozi hao baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wakulima kwamba hawajalipwa fedha za soko la pili la tumbaku.

Aliwataja viongozi wanaoshikiliwa na taasisi hiyo kuwa ni Mwenyekiti Nyarobi James, wajumbe Sylvester Manyigule, Andrea Sengamiti, Lwize Masanja na Martime Kilege.

Chaulo alisema baada ya kufanya uchunguzi wa kina, walibaini zaidi ya Sh. milioni 29 zinadaiwa na wakulima 51 na zimerejeshwa Sh. milioni 17 katika akaunti ya Mitowo Amcos kwa ajili ya kuwalipa wakulima hao.

Alisema uchunguzi wa taasisi hiyo, ulibaini viongozi wa Mole Amcos walitumia madaraka yao vibaya kwa kumlipa Sh. milioni 22 mkulima mmoja (jina limehifadhiwa) wakati si mwanachama.

Chaulo alisema malipo hayo yalifanywa kinyume cha taratibu kwa kuwa fedha hizo zilikuwa za mkopo wa pembejeo wa wanachama wa Mole walipata kutoka Benki ya NMB.

Awali, alisema taasisi hiyo ilipokea malalamiko kuwa viongozi hao wanajihusisha na kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wakulima wa kijiji cha Choma wilayani Igunga kwa sharti la kuwalipa madeni yao kutokana na pamba waliyouza.

# PM ataka asasi kuhamasisha wapigakura

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka asasi za kiraia kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Majaliwa alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizindua Wiki ya Azaki iliyoanza jana hadi jijini hapa.

Alisema wananchi wengi wamejiandikisha kupiga kura hivyo ni wajibu wa asasi kuhimiza kujitokeza kupiga kura.

"Tumeweza kuandikisha wapigakura 19,681,259 sawa na asilimia 86 ya makadirio ya kuandikisha wapigakura 22,916,412, uandikishaji wa mwaka huu umekuwa na mafanikio makubwa sana ikilinganishwa na mwaka 2014 ambao ulifika asilimia 63 ya makadirio," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania wote wenye sifa kujiandaa kushiriki kupiga kura kwa kuwa ni haki yao ya kikatiba kwa kuzingatia misingi ya demokrasia.

Waziri Mkuu alisema serikali imejipanga kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu.

Sambamba na hilo, Majaliwa alizitaka azaki kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo.

Aidha, alizitoa hofu asasi hizo kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika kusukumu gurudumu la maendeleo nchini.

Alisema kuwa serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi ya utendaji kazi wa azaki ili kushiriki ipasavyo katika agenda ya maendeleo na iko tayari muda wote kushirikiana nazo katika kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Waziri Mkuu alisema azaki zimeanzishwa kwa mujibu wa sheria, hivyo zihakikishe wanatekeleza majukumu kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo iliyopo.

Aliwataka wanapotekeleza majukumu yao kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji na katika utekelezaji wa miradi na programu wabainishe vyanzo vyao vya fedha.

"Nawaasa muepuke kujihusisha na mambo ambayo ni kinyume na sheria na taratibu za nchi na badala yake mjikite kwenye mipango, miradi na mikakati kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa mkiongozwa na nia njema kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa letu," alisema.

Aidha, serikali itaendelea kuondoa vikwazo vinavyochangia kukwamisha dhamira ya kuboresha maisha ya wananchi na hasa wanyonge.

Aliziagiza asasi za kiraia zinazofanya kazi nchini kuhakikisha fedha zinazotolewa na wafahadhili zinatumika kuibua miradi shirikishi ya maendeleo kwenye jamii badala ya kufanya semina na makongamano ambayo mengi yamekosa tija na kuishia kunufaisha watu wachache.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema serikali inatambua mchango wa asasi hizo hasa kipindi hiki cha uchaguzi wa serikali za mitaa vijiji na vitongoji.

Kwa upande wake, Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema wizara yake ambayo ndio msimamizi kuu wa mashirika yasiyo ya kiserikali inahakikisha yanafanya kazi kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu kulingana na utamaduni wa Watanzania.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

**2 ACRE YARD FOR RENT Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: gold@goldtz.net**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI


**TAKAWEDO INVESTMENTS COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY yenye namba za usajili T610 BSW Chassis namba **DC51T352470** Engine no **F6AJAA1005931.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/435354/2019.**

215500302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA**
**NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI MADOGO NA: 264/2019.**
**BENEDICTO MULINDA................ MDAI**
**DHIDI YA**
**DICKSON MWILUKI................ MDAIWA**

**KWA: DICKSON MWILUKI**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Madai Na: 264/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 28.11.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi. Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa. AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 04.11.2019



115499502

## KUPOTEA KWA KADI

**YOHANA FAIDA MWASHIOZYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.482 BYG aina ya ERF** rangi nyeupe.chassis namba **SAF25C3RT05067134** Engine namba **6CTAA21073589.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/292062/2019**

115499602

## KUPOTEA KWA CHETI



115498702

**EMMANUEL MARCELY MADUBI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma kilichotolewa na Chuo cha St. Joseph University in Tanzania College of Engineering and Techology mwaka 2016. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **NZ/RB/6187/2019**

## KUPOTEA KWA CHETI



115499302

**ORANY CHONGERA** anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu daraja la IIIC chenye index namba **E524/64** kilichotolewa na Mpuguso TCC mwaka 1986. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KPS/RB/79/2019**

Distributed via ippmedia

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# ARSENAL YAKANA KUMTAKA MOURINHO

**LONDON,** England

ARSENAL imejiweka mbali yenyewe na uwezekano wa kumchukua Jose Mourinho, huku Unai Emery akiwa bado ana sapoti kubwa ya vigogo wa klabu hiyo, kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN FC.

Mourinho amekuwa akitajwa kwamba anapewa nafasi kubwa ya kuchukua mikoba ya Emery pale Arsenal, lakini vyanzo kutoka ndani ya klabu hiyo vimeutonya mtandao wa ESPN FC kwamba kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Manchester United hana nafasi hiyo.

Ilidaiwa kwamba, Mourinho alikutana na Raul Sanllehi, mkuu wa soka wa Arsenal, kwa ajili ya chakula cha usiku, lakini vyanzo kutoka ndani ya klabu hiyo, zimeiambia ESPN FC kwamba, hakukuwa na kikao kama hicho.

Kwani watu hao wawili hawajawahi kuonana kwa muda mrefu na kwamba huo ulikuwa ni uvumi na upuuzwe tu.

Arsenal imepoteza mechi zake mbili msimu huu, lakini bado ina mechi 27 za kucheza ambapo vigogo hao wanaona timu hiyo inaweza kuimarika.

Baada ya sare ya bao 1-1 nyumbani na Wolves Jumamosi, vijana hao wa Emery wamepitwa pointi sita katika nne bora ya Ligi Kuu England.

"Ninajitathimini mimi mwenyewe na nahisi kwamba bado nina kazi na majukumu ya kufanya vizuri zaidi," alisema Emery baada ya mchezo huo.

Distributed via ippmedia

# Schmeichel: Kikosi cha United cha kawaida sana

**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester United, Peter Schmeichel amesema kikosi cha sasa cha klabu hiyo ni "cha wastani" na kuwabwatukia wachezaji kwa kutoonyesha kujutia baada ya kufungwa na Bournemouth.

Bao la Josh King liliiacha klabu hiyo ikiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo na kuwa na mwanzo mbaya zaidi wa Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka 33.

Golikipa huyo mstaafu anahisi kwamba, kocha Ole Gunnar Solskjaer ana kazi kubwa na ya ziada ya kufanya ili kuiwezeha timu hiyo kurudi kileleni mwa msimamo.

Schmeichel aliuambia mtandao wa Ligi Kuu: "Kwa uhakika kabisa haikuwa poa, wachezaji 'walizingua' na wakachukulia poa bila kujali.

"Na nikimwangalia Ole, nafikiria imeishiwa kabisa mbinu na hana cha ziada cha kufanya kwa sasa.

"Kwa uhakika kabisa kuna vitu vingi vinatakiwa kufanywa kwenye klabu hii. Ukweli ni kwamba kikosi hicho ni cha wastani na ni cha kawaida sana. Kuna wachezaji hawastahili kuichezea timu kubwa kama Manchester United."





# Vigo watimua kocha

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Celta Vigo ambayo inasuasua kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, imemfukuzia mbali kocha wake, Fran Escriba baada ya kuchapwa na Getafe.

Celta ilitangaza kumfukuza kocha huyo baada ya mchezo wa juzi Jumapili ambapo walifungwa bao 1-0 nyumbani na Getafe - kikiwa ni kichapo chao cha nne mfululizo.

Matokeo hayo yameiacha Celta ikiwa kwenye ukanda wa kushuka daraja baada ya mechi 12 za LaLiga.

"Fran Escriba hataendelea kuwa kocha wa Celta. Klabu inapenda kumshukuru yeye na benchi lake la ufundi kwa kazi kubwa waliyoifanya na tunawatakia mafanikio mema," taarifa ya Celta ilisema.

Kocha huyo wa zamani wa Elche, Getafe na Villarreal, Escriba aliteuliwa kuinoa Celta Machi mwaka huu na kuwa kocha wa tatu kwa msimu wa 2018-19.

Escriba aliisaidia Celta kutoshuka daraja msimu uliopita, hata hivyo, kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, ameshinda mechi mbili tu msimu huu.

## Kocha Everton amliilia Gomes

**LONDON,** England

KOCHA wa Everton, Marco Silva amesisitiza kwamba, Andre Gomes atarudi uwanjani akiwa imara baada ya kuumia vibaya kifundo cha mguu kwenye mchezo dhidi ya Tottenham.

Gomes atafanyiwa upasuaji wa 'enka' hiyo baada ya kuumia wakati timu hizo zikitoka sare ya kufungana bao 1-1 kwenye mchezo wa Ligi kuu pale katika dimba la Goodison Park.


Everton walionekana kupagawa wakati Gomes alipobebwa kwa machela kutoka uwanjani kipindi cha pili baada ya kukwatuliwa na nyota wa Tottenham, Son Heung-min na baadaye raia huyo wa ureno akajigonga kwa Serge Aurier.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Silva aliwaambia waandishi wa habari: "Ulikuwa ni wakati mgumu kwa upande wetu, tukasahau mchezo na matokeo.

"Andre atahitaji sapoti kubwa kutoka kwetu. Ameumia vibaya, lakini nina uhakika kwa asilimia 100 atarudi uwanjani akiwa imara zaidi.

"Wachezaji wetu wanahuzuni kubwa, ni wakati mgumu kwako na kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, lakini hamasa waliyoonyesha kwa wakati huu ni nzuri. Ingawa ulikuwa wakati mgumu zaidi kwa upande wetu."

Son alionyeshwa kadi nyekundu baada ya mwamuzi, Martin Atkinson kwenda kujiridhisha kwenye teknolonia ya maamuzi ya usaidiaji wa video, VAR, kwa kumchezea faulo Gomes.




## BALOTELLI AITWA NYANI, AWAPIGA KWA MPIRA




Distributed via ippmedia

**ROME,** Italia

MSHAMBULIAJI 'mtata' wa Brescia, Mario Balotelli juzi alikumbana na adha ya kuzomewa na mashabiki wa klabu ya Verona kwa kumuita nyani uwanjani, wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya Italia baina ya timu hizo.

Mashabiki wa Verona walimdhihaki Balotelli kwa kumuita nyani katika mchezo huo ambao Verona ilishinda mabao 2-1 dhidi ya Brescia.

Akionyesha kukasirishwa na kitendo hicho, Balotelli aliudaka mpira wakati mchezo ukiendelea na kuupiga kwenda kwa mashabiki jukwaani, kabla ya kuchukua uamuzi wa kutoka uwanjani.

Baada ya kubembelezwa na wachezaji wenzake, Balotelli mchezaji wa zamani wa Manchester City na Liverpool za England alirudi uwanjani na kufunga bao hilo moja kwa Brescia.

Mwamuzi wa mchezo huo Maurizio Mariani alitaka hatua zichukuliwe na alitishia kusitisha mchezohuo endapo vitendo vya mashabiki hao vingeendelea.

## *Kovac atupiwa virago Bayern*

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imemtupia virago kocha wake, Niko Kovac baada ya timu hiyo kufungwa mabao 5-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Ujerumani uliocheza juzi, dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Kocha huyo alifukuzwa kazi muda mfupi baada ya Bayern kucharazwa mabao 5-1 dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Bayern inashika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani matokeo ambayo yamewachefua vigogo wa klabu hiyo ya Allianz Arena.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 48, kiungo wa zamani wa timu ya Taifa ya Croatia, alipewa jukumu la kuinoa timu hiyo tangu Julai 2018 na kuiongoza Bayern kutwaa taji la ligi na lile cha Chama cha Soka cha Ujerumani msimu uliopita.

Kovac ameshinda mechi 45 kati ya 65 tangu akabidhiwe mikoba ya kuinoa Bayern, lakini kipigo cha Jumamosi kilikuwa kikubwa zaidi kwa klabu hiyo kwenye mchezo wa Bundesliga kwa kipindi cha miaka 10.

Bayern ilisema katika taarifa yake kwamba maamuzi hayo yamekuja baada ya "matokeo ya makubaliano ya kuachana na Niko Kovac yaliyofanyika Jumapili."

Ofisa Mtendaji Karl-Heinz Rummenigge, alisema: "Kiwango cha timu yetu katika wiki za hivi karibuni na matokeo yameonyesha kuwa kulitakiwa kuchukuliwa hatua.

Timu hiyo itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Hans Flick atakayeiongoza katika mechi mbili dhidi ya Olympiakos na Borussia Dortmund.

Kovac, aliyecheza mechi 51 kati ya mwaka 2001 na 2003, alianza kuwekwa kikaangoni tangu mwanzoni mwa msimu huu kutokana na mwenendo mbaya.



# DONDOO ZA
# MAGAZETI YA



# ‘MBAPPE KAPANGA KUJIUNGA NA MADRID’

## Aliniambia nadhani ni mapema sana, mimi ni Mparis, sitaki kuondoka nchini mwangu kama...

**LIVERPOOL,** England

KYLIAN Mbappe ana mpango wa kujiunga na Real Madrid baada ya kukataa nafasi hiyo wakati akiwa Monaco, kwa mujibu wa Makamu wa Rais wa zamani, Vadim Vasilyev.

**Mbappe awali alijiunga na miamba ya Ligue 1, Paris Saint-Germain kwa mkopo akitokea kwa mahasimu zao Monaco mwaka 2017 kabla ya kukamilisha uhamisho huo kuwa wa jumla kwa dili la euro milioni 145 mwaka uliofuata.**

Madrid ilivutiwa na Mbappe kabla ya Mfaransa huyo kuondoka Monaco na kujiunga na Paris, na matajiri hao wa LaLiga wameendelea kuhusishwa na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

Vasilyev, ambaye anamjua Mbappe vizuri sana kuanzia wakati wakiwa pamoja Uwanja wa Stade Louis II, anaamini mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2018, hatimaye atakamisha uhamisho wake wa kujiunga na Madrid.

“Kwa nini hakusaini Real?,” Vasilyev aliiambia Telefoot.” Aliniambia: ‘Vadim, nadhani ni mapema sana, Mimi ni Mparis, sitaki kuondoka nchini mwangu kama hivyo, ninataka kuwa mchezaji mkubwa hapa. Real Madrid itasubiri, hicho ndicho ninachokisubiri’.

“Nilimwambia, ‘Kylian, upo sahihi’. Anataka kushinda. Na bila shaka Ligi ya Mabingwa lazima itwaliwe na mchezaji kama hivyo. Kama hilo litatimia na Paris, ni vizuri.”

Vasilyev aliongeza: “Wao [Real Madrid] watagonga mlangoni kwako. Estadio Santiago Bernabeu watakupongeza wakati utakapofika.”

“Amebaki kuwa mtu yule yule, na Kylian yule yule. Ni kwamba amepata umuhimu, nguvu katika mazingira ya kiulimwengu,” Vasilyev alisema.

“Ninamjua Cristiano Ronaldo vizuri sana, na mara zote anataka kuvunja rekodi zote, kusonga mbele. Kylian naye yupo hivyo.”

Mbappe, ambaye alitwaa ubingwa wa Ligue 1 katika mwaka wake wa mwisho akiwa Monaco, ameng’ara akiwa na PSG katika jiji hilo la Ufaransa. Ametwaa ubingwa wa Ligue 1 mara mbili mfululizo, pamoja na Kombe la Coupe de France, Coupe de la Ligue na Kome la Mabingwa.

Baada kufunga mabao 39 kwenye mashindano yote msimu wa 2018-19, Mbappe ametupia mara tisa kwenye kikosi hicho cha Thomas Tuchel, PSG msimu huu.

## ZISIKUPITE

### LALLANA AWINDWA CHINA

KIUNGO Muingereza Adam Lallana, 31, anawindwa na klabu kutoka Ligi Kuu China wakati huu mkataba wake na Liverpool ukimalizika majira ya joto. ***(Telegraph)***

### KOEMAN AJIPELEKA BARCA

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman amethibitisha kuna kipengele katika mkataba wake kinachomruhusu kujiunga na Barcelona, ambayo aliichezea kuanzia 1989 hadi 1995, lakini baada tu ya michuano ya Euro 2020. ***(Goal.com)***

### EMERY APEWA MWEZI ARSENAL

UNAI Emery amepewa mwezi mmoja kuokoa kibarua chake kama kocha wa Arsenal. ***(Mirror)***

### SILVA KUIKOSA LIVERPOOL

KIUNGO wa Manchester City, Mhispania David Silva, 33, anatarajiwa kukosa safari muhimu ya kwenda kuwavaa vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool kwa sababu ya majeraha ya misuli. ***(Mirror)***

### ALLEGRI SASA ANUKIA BAYERN

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, ambaye karibuni alihusishwa na Arsenal, anapewa nafasi ya kuinoa Bayern Munich kufuatia kutimuliwa kwa Niko Kovac. ***(Bild, via Football Italia)***

### MOURINHO YUMO BAYERN

KOCHA wa RB Leipzig, Ralf Rangnick pia amekuwa akipewa nafasi kubwa ya kuinoa Bayern Munich - na Jose Mourinho ni mtu mwingine anayehusishwa. ***(London Evening Standard)***

### ‘HAALAND HAJATOLEWA OFA’

RED Bull Salzburg bado haijapokea ofa yoyote kwa straika wao, Mnorway Erling Braut Haaland, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Real Madrid na Juventus. ***(Mirror)***

### ZIDANE AMTAKA BEKI ARSENAL

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane yupo tayari kumsajili beki Mfaransa wa Arsenal mwenye umri wa miaka 20 anayecheza kwa mkopo Saint-Etienne. ***(Express)***

### KUTUA ALENA KWA MKOPO

KIUNGO wa Barcelona, Mhispania Carles Alena, 21 - anayewindwa na Tottenham Hotspur - anaweza kuruhusiwa kuondoka La Liga kwa mkopo ifikapo Januari. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### ARSENAL MBALI NA MOURINHO

ARSENAL wanajiweka mbali wenyewe kutoka uwezekano wa kumwajiri Kocha wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Mreno Jose Mourinho. ***(ESPN)***

### SMALLING AIPAGAWISHA ROMA

ROMA inajiandaa kukutana zaidi na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumsajili jumla beki Muingereza Chris Smalling, 29 - anayeichezea miamba hiyo ya Serie A kwa mkopo - na ipo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 8.6. ***(Calciomercato)***

HABARI MICHEZO

## Singida United yajitambua ikiifuata Lipuli

**Na Focus Nicus**

WAKATI kesho ikiwa na kibarua kigumu kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa dhidi ya Lipuli FC, Singida United imejitazama kwa kina na kubaini umakini ndicho kitu kilichowanyima ushindi katika mechi 10 za Ligi Kuu Bara ilizocheza hadi sasa.

Katika michezo hiyo 10 Singida United, imeambulia sare nne na kupoteza mechi sita msimu huu, jambo ambalo Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ramadhani Nswazurimo, analia na kikosi chake kushindwa kujiamini hususan safu ya ushambuliaji.

Nswazurimo aliambia gazeti hili kuwa tatizo kubwa ni washambuliaji wake kushindwa kujiamini wanaponasa mpira eneo sahihi, hivyo kushindwa kucheka na nyavu.

"Wachezaji wangu wanashindwa kufanya maamuzi wanapokuwa na mpira ndani ya 18, hicho ndicho kinachotunyima ushindi, hata hivyo nimegundua nini cha kufanya ili kurejesha ubora wao," alisema Nswanzurimo.

Jumamosi Singida United ililazimisha sare tasa dhidi ya Mtibwar Sugar katika Uwanja wa Jamhuri Morogoro ikiwa ni baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 dhihi ya JKT Tanzania kwenye dimba lake la nyumbani la Sheikh Amri Abeid jijni Arusha.

## Kocha JKU ataja wanapokosea

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya JKU, Omar Khamis Othman, amesema ana kazi kubwa ya kukisuka kikosi chake ili kiweze kuwa na umakini pindi wanapokaribia katika lango la wapinzani wao.

Baada ya kushuka dimbani mara saba msimu huu kwenye Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16, JKU ipo nafasi ya tatu na alama zake 15.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo alisema kikosi chake kinacheza vizuri, lakini tatizo kubwa lililopo ni wachezaji kutokuwa makini katika umaliziaji hali inayosababisha kukosa mabao mengi ya wazi.

Alisema hivi sasa katika mazoezi ya timu hiyo, nguvu kubwa anapaswa kuzielekeza kwa washambuliaji wake ili waweze kuwa makini hususan kwa pasi ambazo zipo wazi kuzaa matunda ya bao.

Aidha, akizungumzia juu ya kadi za onyo zinazomiminika kwa wachezaji wake katika michezo mbalimbali ya Ligi Kuu ya Zanzibar, alisema tatizo hilo ameliona na tayari ameshakaa na wachezaji kuwapa mawaidha juu ya nizamu na kuepuka faulo ambazo zinaweza kuepukika.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa JKU kuendelea kumiminika viwanjani pindi wanaposhuka dimbani ili kuipa hamasa timu yao iweze kufanya vizuri zaidi katika ligi hiyo yenye upinzani wa hali ya juu hadi hivi sasa ambapo ipo katika mzunguko wake wa nane.

# MRUNDI WA SIMBA AIFURAHIA KILIMANJARO QUEENS CECAFA

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba Queens kutoka Burundi, Joelle Bukuru, amefurahia timu yake ya Taifa ya Wanawake kupangwa kundi moja na wenyeji Kilimanjaro Queens katika mashindano ya Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika hapa nchini hivi karibuni.

Mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yanatarajiwa kufanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex kuanzia Novemba 14 hadi 23, mwaka huu na yatashirikisha nchi nane.

Kilimanjaro Queens kutoka Tanzania Bara imepangwa Kundi A pamoja na Burundi, Sudan Kusini na ndugu zao Zanzibar Queens wakati Kundi B linaundwa na Uganda, Ethiopia, Kenya na Eritrea.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Joelle, alisema kwake itakuwa rahisi kucheza na Kilimanjaro Queens kwa sababu anawafahamu wachezaji wake kutokana na kushiriki katika ligi moja hapa nchini.**

Joelle alisema kuwa ataisaidia timu yake kuipa mbinu zinazotumiwa na wachezaji wa Kilimanjaro Queens kwa malengo ya kupata matokeo mazuri katika mchezo ambao utawakutanisha katika hatua hiyo ya makundi kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

"Tutajipanga kuhakikisha tunafanya vema mwaka huu, timu yetu ya Burundi inaundwa na wachezaji wengi wanaocheza Ligi ya Wanawake hapa Tanzania, hii itatusaidia kuwabana kwa sababu ya kufahamu mbinu za wachezaji, kwa kifupi tutaingia kushindana," alisema kiungo huyo.

Hata hivyo, Burundi haikushiriki katika mashindano yaliyofanyika mwaka jana jijini Kigali, Rwanda kutokana na tofauti za kisiasa zilizopo baina ya nchi hizo mbili.

Kilimanjaro Queens ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambayo mwaka huu inafanyika kwa mara ya tatu.




Wachezaji wa timu ya watoto ya Capstone ('waliovaa bips'), na wachezaji wa timu ya Bleubulnec, wa chini ya umri wa miaka 13, wakiwania mpira wakati wa mashindano ya Day Youth Cup, yaliofanyika katika viwanja vya Gymkhana Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mwadui yatamba kuifumulia Mtibwa Sugar Uwanja wa Gairo*

**Na Somoe Ng'itu**

HAKUNA kulala! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaochezwa kesho kwenye Uwanja mpya wa Gairo mkoani Morogoro.

Hiyo ndio mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa katika uwanja huo ambao unamilikiwa na manispaa ya wilaya hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Khalid, alisema kila mchezo kwake ni sawa na fainali na amewaandaa wachezaji wake kupambana kuhakikisha wanafanya vema katika mchezo huo na kusahau matokeo ya nyuma.

Khalid alisema kuwa wamefika mapema Morogoro kwa sababu wanahitaji kupumzika na kuingia uwanjani hapo kesho wakiwa imara kusaka pointi tatu.

"Tumeshafika Morogoro, tumekuja kuendelea kupambana, tunahitaji kupata matokeo mazuri ili kujiweka nafasi salama, tunajua huko mbele vita zitakuwa kubwa, hii inasababishwa na idadi ya timu sita kushuka daraja," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema wanajiandaa kupambana kuhakikisha wanaanza na rekodi nzuri katika uwanja huo mpya.

Katwila alisema anakifahamu vema kikosi cha Mwadui, hivyo wataingia kwa tahadhari na umakini mkubwa katika mchezo huo ambao awali ulipangwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

"Tumejiandaa vema, mechi zote ni ngumu, kama tunavyojiandaa sisi, na wenzetu pia wanajiandaa hivyo hivyo kupata matokeo bora, tunaomba Mungu vijana wafanye vile tunavyowaelekeza," Katwila alisema.

Michezo
Jumanne Novemba 5, 2019
Nipashe



'Mbappe kapanga kujiunga na Madrid' UKURASA 30



Mshambuliaji 'mtata' wa Brescia, Mario Balotelli akijaribu kufunga kwenye mechi ya Serie A wakati wakilala 2-1 dhidi ya Verona, na kukasirika kwa kitendo cha kuitwa nyani juzi. **HABARI UK. 29**.

Distributed via ippmedia

# Yanga kimyakimya, Zahera sasa atetewa

## ●●● Mwakyembe aomba asitimuliwe kwa kuwa amepambana katika shida na raha, timu kujichimbia leo kwa...

**Focus Nicus na Shufaa Lyimo**

WAKATI Yanga ikirejea jijini Dar es Salaam jana kimyakimya baada ya kukubali kipigo cha mabao 3-0 nchini Misri dhidi ya Pyramids FC huku joto la mashabiki na wanachama bado likiendelea kufukuta wakitaka mkataba wa Kocha Mkuu Mwinyi Zahera sasa uhitimishwe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harisson Mwakyembe, ameitahadharisha klabu hiyo kuhusu kumtimua.

**Matokeo hayo ya juzi, yanaifanya Yanga kuungana na watani na ndugu zao nchini, Simba, Azam, KMC, KMKM na Malindi kuiaga michuano ya kimataifa msimu huu baada ya kutolewa kwa jumla ya mabao 5-1 kwenye mechi hiyo ya mchujo ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Hiyo ni baada ya mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, Yanga kukubali kichapo cha mabao 2-1, ambapo vuguvugu la baadhi ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo lilianzia hapo wakitaka Zahera atimuliwe huku wakimrushia chupa za maji kwa kile walichodai timu kucheza bila kuelewana na kushindwa kuonyesha mchezo mzuri.

Juzi licha ya kusubiri kuiona mechi hiyo ambayo ilitarajiwa kuonyeshwa kupitia Azam TV kabla ya dakika 10 baada ya mechi kuanza kutangaza kutokana na sababu zilizopo nje ya uwezo wao mchezo huo hautaonyeshwa, mashabiki sehemu mbalimbali na hata jana waliendelea kudai Zahera hastahili tena kukinoa kikosi hicho.

"Yaani tumepigwa ndani nje, na kutolewa kwa mabao mengi hivyo, lakini kubwa timu yetu ikishindwa kuelewana uwanjani hadi leo, kocha huyu wa nini sasa," alisema Juma Abubakar, mkazi wa Mbezi Luis jijini Dar es Salaam.

John Mathias wa Ubungo jijini Dar es Salaam, alidakia kwa kueleza: "Kuna haja ya kulibomoa benchi zima la ufundi kwani kocha kapewa nafasi ya kusajili wachezaji anaowataka na ameshindwa kupata matokeo huku timu ikicheza ovyo."

Hata hivyo, wakati hayo yakiendelea mara tu ya kichapo cha kwanza na vuguvugu la Zahera kutaka kutimuliwa kuibuka, Waziri Mwakyembe aliliambia Nipashe kuwa Yanga haina budi kuachana na dhana hiyo kwa kuwa kocha huyo ni miongoni mwa makocha bora hapa nchini, ambaye ana kila sababu ya kupewa pongezi kwa kile anachokifanya.

Dk. Mwakyembe alisema hakuna sababu ya kutafuta mchawi wala kumtupia lawama kocha, bali wachezaji wanapaswa kujituma zaidi.

"Sioni sababu ya Watanzania kusema hawamtaki Zahera, ikumbukwe amepambana na Yanga katika kipindi cha shida na raha mpaka kuifikisha ilipo sasa," alisema Dk. Mwakyembe.

Katika hatua nyingine, baada ya Yanga kurejea jana mchana, wachezaji walipewa mapumziko kabla ya leo kuingia kambini kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ndanda FC Ijumaa wiki hii.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia Nipashe: "Timu imesharejea na inaingia kambini kesho [leo] kwa ajili ya safari ya Mtwara."

# Aussems: Subirini mabao zaidi

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Aussems, amesema kikosi chake kimejipanga kuendeleza wimbi la ushindi na kucheza katika kiwango cha juu kwenye kila mchezo unaofuata.

Mabingwa hao watetezi wanatarajia kuwakaribisha "Maafande" wa Tanzania Prisons kutoka Mbeya katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa keshokutwa Alhamisi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa katika mchezo uliopita na anaahidi kikosi chake kitaendelea kujifua ili kipate ushindi katika kila mechi watakayocheza ya ligi hiyo.

Aussems alisema kuwa anafahamu ligi hiyo ni ngumu na yenye ushindani, lakini watatumia uzoefu walionao ili kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri na kukaa kileleni katika msimamo wa ligi.

"Nimeridhishwa na matokeo ya mechi yetu dhidi ya Mbeya City, pia nimefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wangu katika mchezo huo, nina matumaini kwamba tutaendelea na kasi hii, tunahitaji kuendelea kujituma na kupambana, tucheze katika morali ya juu," alisema Aussems.

Kocha huyo aliongeza kuwa anaamini kila mchezaji anayepata nafasi ya kucheza katika kikosi hicho, ataonyesha ubora wa hali ya juu kwa sababu malengo yao ni kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, ameliambia gazeti hili kuwa bado kikosi chake kiko kwenye hatua ya kujengwa na kitaendelea kupambana ili kuhakikisha wanabaki kwenye ligi hiyo msimu ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >